

**KUCHUNGUZA DHAMIRA YA MAPENZI KATIKA RIWAYA YA
KAMWE SI MBALI TENA YA SAID AHMED MOHAMED**

AISHA MOHAMED ALI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU
YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A
KISWAHILI) CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2019

ITHIBATI

Aliyeweka saini hapo chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo:
“Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena”,
na anapendekeza kuwa ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya
kutimiza sharti la kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu
Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya kazi hii, kutunza katika mfumo utakaowezesha kunakiliwa au kuisambaza kwa namna yoyote ile iwe kieletroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vyenginevyo bila ya kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi Aisha Mohamed Ali, nathibitisha kuwa kazi hii ni yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kile kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii ya uzamili au shahada nyengine yoyote ile.

.....

Saini

.....

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, mume wangu pamoja na watoto wetu.

SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Allah (SW) mlezi wa viumbe vyote, aliyenijaalia afya njema na uzima hadi kufikia tamati ya kazi hii. Kisha rehma na amani ziwe juu ya Mtume Muhammad (SAW) pamoja na watu wake na maswahaba zake. Baada ya kumshukuru Allah (SW) shukrani kwa wazazi wangu mama yangu mpenzi Mariyam Moh'd Ali na marehemu baba yangu Mohamed Ali Mohamed kwa malezi yao mema na yaliyotukuka pasi na kuwasahau walezi wangu wote, Allah (SW) awajaze kheri na awajaalie mionganini mwa watu wa Peponi. Aidha natoa shukrani za dhati kwa wale wote waliochangia katika kuniongoza, kunipa moyo pamoja na kunisaidia mengi yaliyowezesha kukamilika kwa kazi hii. Sina malipo ya kuwalipa isipokuwa namuomba Allah (SW) awape kheri za dunia na akhera. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote katika ukurasa huu nachukua fursa hii adhimu kuwataja baadhi yao:

Kwanza, shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Mohamed Omary Maguo, licha ya kukabiliwa na majukumu mazito lakini alitenga muda wake kuitalii kazi yangu na kutoa mwongozo pale palipostahiki. Pili, naushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hususan walimu wangu ambao nimevuna mengi kutoka kwao. Mionganini mwao: Prof. Emmanuel Mbogo, Dkt. Mohamed Omary, Dkt. Zelda Elisifa, na Dkt. Hilda Pembe. Tatu, shukrani kwa Mwalimu Bakar Kombo Bakar na Mwalimu Sharif Juma Fakih kwa kutoa ushirikiano usio kifani kwangu katika uandaaji wa kazi hii hadi kufikia tamati. Nne, shukrani za pekee kwa familia, mume wangu mpenzi Bwana Suleiman Saleh Abrahman. Kazi hii ni matunda ya juhudini zake, pamoja na watoto wetu Saleh Suleiman Saleh, Swafaa

Suleiman Saleh na Sahil Suleiman Saleh. Kwa utukufu wake Allah (SW) awakuze katika makuzi mema na awaongoze katika njia iliyonyooka.

Mwisho nitakuwa mchache wa fadhila nisipotoa shukurani zangu kwa walimu wangu wapenzi: Mwalimu Muhammed Ali Salim, Mwalimu Suleiman Abdalla Ali, Mwalimu Ayoub Ussi Hassan, Mwalimu Ali Said Haji kwa mchangano wao mkubwa wa kitaaluma. Vilevile shukurani adhimu ziwafikie wanafunzi wenzangu wote tuliokuwa pamoja katika gurudumu hili kwa kipindi chote cha masomo. Fundi wangu wa kompyuta Bwana Abdallah Shaibu Kheri na Bibi Sauda Hamad Salim nawashukuru sana kwa msaada wao. Hawa wote niliowataja na wale ambao sikuwataja nathamini mawazo, fikra, ushauri na michango yao ya hali na mali. Allah (SW) kwa mapenzi yake awalipe malipo mema hapa duniani na kesho akhera.(Amiin)

IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza dhamira ya mapenzi katika Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed. Ili kutimiza lengo kuu hili kulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni: Kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* na Kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Ili kupata data toshelevu zenyekukidhi haja ya matumizi, data za utafiti huu zilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji makini matini na upitiaji wa nyaraka. Data hizo zilichambuliwa kwa njia ya maeleo kulingana na malengo mahsususi yaliyotajwa kwa kuongozwa na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji kwa lengo la kwanza na nadharia ya Simiotiki kwa lengo la pili. Hatimae matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa dhamira ya mapenzi katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena* imeweza kujitokeza katika namna tofauti ikiwemo: Mapenzi ya nchi, mapenzi ya familia, mapenzi ya ndoa, mapenzi ya udugu, mapenzi ya urafiki, mapenzi ya dini/imani, mapenzi ya mazingira, mapenzi ya elimu, mapenzi ya mali/pesa na mapenzi ya kazi. Pamoja na hayo pia utafiti umebaini mbinu za kisanaa ambazo zilitumika katika kuwasilisha dhamira hiyo ya mapenzi nazo ni: mbinu ya matumizi ya wahusika, mbinu ya matumizi ya lugha na mbinu ya matumizi ya mandhari. Na mwisho mtafiti amehitimisha kazi yake kwa kutoa mapendekezo faafu kwa walimu, wanafunzi, watafiti wajao na wanajamii kwa ujumla.

YALIYOMO

ITHIBATI.....	ii
HAKI MILIKI.....	iii
TAMKO.....	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI.....	viii
YALIYOMO.....	ix
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xv
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xvi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tatizo la Utafiti	7
1.4 Malengo ya Utafiti	8
1.4.1 Lengo Kuu	8
1.4. 2 Malengo Mahsus.....	8
1.5 Maswali ya Utafiti.....	9
1.6 Umuhimu wa Utafiti	9
1.7 Vikwazo vyta Utafiti	10
1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo vyta Utafiti.....	10
1.8 Mipaka ya Utafiti	10
1.9 Mpangilio wa Tasnifu	11

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA	
KINADHARIA	13
2.1 Utangulizi.....	13
2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu	13
2.2.1 Maana ya Riwaya.....	13
2.2.2 Historia na Chimbuko la Riwaya	14
2.2.3 Maana ya Dhamira.....	17
2.2.4 Maana ya Mapenzi	18
2.2.5 Mbinu za Kisanaa	18
2.2.5.1 Wahusika.....	19
2.2.5.2 Matumizi ya Lughya	20
2.2.5.3 Mandhari	21
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi	21
2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Dhamira katika Riwaya kwa Ujumla .	22
2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.....	27
2.4 Pengo la Maarifa	31
2.5 Mkabala wa Kinadharia	31
2.5.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji	32
2.5.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji	33
2.5.2 Nadharia ya Simiotiki	35
2.5.2.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki	36
2.6 Hitimisho.....	37

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	38
3.1 Utangulizi.....	38
3.2 Eneo la Utafiti	38
3.3 Usanifu wa Utafiti.....	38
3.4 Kundi Lengwa.....	39
3.5 Sampuli na Usampulishaji	40
3.5.1 Sampuli ya Utafiti	40
3.5.2 Usampulishaji	40
3.6 Aina za Data.....	41
3.6.1 Data za Awali.....	41
3.6.2 Data za Upili	41
3.7 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data.....	42
3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini	42
3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka.....	43
3.8 Uchambuzi wa Data za Utafiti	43
3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo.....	44
3.9 Zana za Utafiti.....	44
3.9.1 Kompyuta.....	44
3.9.2 Kalamu na Karatasi	45
3.10 Hitimisho.....	45
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI.....	46
4.1 Utangulizi.....	46

4.2	Muhtasari wa Riwaya Teule ya <i>Kamwe si Mbali Tena</i>	46
4.3	Usuli wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed	48
4.4	Kubainisha Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya <i>Kamwe si Mbali Tena</i>	50
4.4.1	Dhamira ya Mapenzi ya Nchi/Uzalendo	51
4.4.2	Dhamira ya Mapenzi ya Familia	53
4.4.3	Dhamira ya Mapenzi ya Ndoa	56
4.4.3.1	Mapenzi ya Dhati	57
4.4.3.2	Mapenzi ya Uongo	59
4.4.4	Dhamira ya Mapenzi ya Udugu	60
4.4.5	Dhamira ya Mapenzi ya Urafiki	61
4.4.6	Dhamira ya Mapenzi ya Dini/Imani	63
4.4.7	Dhamira ya Mapenzi ya Mazingira	65
4.4.8	Dhamira ya Mapenzi ya Kazi	66
4.4.9	Dhamira ya Mapenzi ya Pesa/Mali	67
4.4.10	Dhamira ya Mapenzi ya Elimu	69
4.5	Kuchambua Mbinu za Kisanaa Zilizotumika Kuwasilisha Dhamira ya Mapenzi	71
4.5.1	Mbinu ya Matumizi ya Wahusika	72
4.5.1.1	Tambo	73
4.5.1.2	Mwavile	74
4.5.1.3	Janet	76
4.5.1.4	Bwana Hassani na Bi Halima	76
4.5.1.5	Sele (Msurupwete)	77

4.5.1.6	Jokha	79
4.5.2	Mbinu ya Matumizi ya Lughा.....	80
4.5.3	Matumizi ya Tamathali za Semi	80
4.5.3.1.1	Matumizi ya Tashbiha.....	81
4.5.3.1.2	Matumizi ya Tashhisi.....	85
4.5.3.1.3	Matumizi ya Sitiari	88
4.5.3.1.4	Matumizi ya Misemo	89
4.5.3.1.5	Matumizi ya Methali	91
4.5.3.1.6	Matumizi ya Taswira	94
4.5.3.2	Matumizi ya Mbinu Nyengine za Kisanaa.....	95
4.5.3.2.1	Matumizi ya Mubalaghа/Chuku	96
4.5.3.2.2	Matumizi ya Takriri	97
4.5.4	Mbinu ya Matumizi ya Mandhari	98
4.5.4.1	Mandhari ya Pwani/Ufukweni	99
4.5.4.2	Mandhari ya Nyumbani	100
4.6	Hitimisho.....	102

SURA YA TANO: HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO 103

5.1	Utangulizi.....	103
5.2	Muhtasari wa Utafiti	103
5.3	Matokeo ya Utafiti	105
5.3.1	Lengo la Kwanza	106
5.3.2	Lengo la Pili	106
5.4	Mapendekezo ya Utafiti	107

5.5	Hitimisho.....	107
MAREJELEO.....	108	

ORODHA YA MAJEDWALI

Jadweli 01:	Muhtasari wa Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya <i>Kamwe si Mbali Tena</i>	51
Jedwali 02:	Muhtasari wa Mbinu za Kisanaa katika Riwaya ya <i>Kamwe si Mbali Tena</i>	72

ORODHA YA VIFUPISHO

AS:	Alayhi Ssalaamu
B.A:	Bacholer of Art
BAKIZA:	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
BBC:	British Broadcasting Cooparation
Dkt:	Daktari
DW:	Deustche Welle
IPC:	Islamic Propagation Center
KG:	King George
M.A:	Master of Art
OUT:	Open University of Tanzania
PhD:	Doctor of Philosophy
Prof:	Profesa
SAW:	Swallallahu Alayhi Wasallamu
SUZA:	State University of Zanzibar
SW:	Subhanahu Wataala
TAKILUKI:	Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar
TUKI:	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TY:	Tafsiri Yangu
UDSM:	University of Dar es Salaam
Uk:	Ukurasa
Yoh:	Yohana.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahu su Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed. Katika kufanikisha utafiti huu, sura hii imejikita katika ufanuzi wa vipengele muhimu ambavyo ndio msingi mkuu wa utafiti wowote wa kitaaluma. Miongoni mwa vipengele ambavyo vimeelezewa katika sura hii ya utangulizi ni pamoja na: usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vyia utafiti na utatuzi wake, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

1.2 Usuli wa Mada

Fasihi kama chuo au taasisi inayotumika katika kutoa mafunzo kwa jamii huakisi na kusawiri mfumo mzima wa maisha halisi ya jamii, kwa sababu huenda sambamba kulingana na harakati za maisha ya watu wa jamii husika katika nyanja zote: kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Kwa hivyo, fasihi haitoki katika ombwe tupu, bali ni zao la jamii ambalo limejengeka na hali halisi ya maisha ya jamii.

Fasihi ni sanaa yenyeye mkusanyiko wa kazi mbalimbali zinazosanifiwa kwa kutumia lugha. Hutumia zaidi maneno na kujishughulisha na jinsi binadamu anavyoitambua mwenyewe binafsi na jinsi anavyoathiriwa na binadamu wenzake aidha na viumbe vingine aina kwa aina katika mazingira mbalimbali ya maisha (Nkwera, 2003). Wamitila (2004) anasema fasihi ni sanaa ya lugha inayoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu, matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake, na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake. Anaendelea kufafanua kuwa

binaadamu alipopata lugha alihitaji kujieleza, kuyaeleza mazingira yake, kuzieleza kero zake na hofu zake, kuzifichua hisia na matamanio yake, huu unakuwa ndio msingi muhimu wa kukua kwa fasihi. Kwa mantiki hii ni wazi kuwa fasihi hutumia lugha kueleza mazingira yanayomzunguka mwanadamu katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa fasihi huwasilishwa kwa njia mbili, njia ya mdomo (masimulizi) na njia ya maandishi. Fasihi andishi ni sanaa ambayo hutumia maneno yaliyoandikwa kuwasilisha ujumbe wake. Aina hii ya fasihi huzalisha kazi za kubuni zenye msingi katika maisha yanayofahamika na binaadamu. Anaendelea kusema kwamba, sanaa hii huhitaji msanii kuwa macho, yaani awe na jicho pekuzi ambalo litaweza kupenya ndani ya jamii husika ili msanii huyo aweze kutoa ama kubuni sanaa itakayosawiri na kuakisi maisha ya mwanadamu.

Utanzu wa riwaya ni mionganoni mwa tanzu za fasihi andishi ambao hueleza masuala mbalimbali yanayohusu maisha ya mwanadamu na mazingira yake kwa mawanda mapana sana. Senkoro (1982) anaeleza kuwa, riwaya ni kisa ambacho ni kirefu vya kutosha chenye zaidi ya tukio moja ndani yake, ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa uzito na undani wa mambo mbalimbali, riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi kama apendavyo mwandishi. Mulokozi (ameshatajwa) anasema riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi. Kutokana na hayo, ni dhahiri shahiri kuwa visa na matukio yanavyosawiriwa na

mwandishi/mtunzi katika kazi ya fasihi huwa yana ukaribu na ukweli wa maisha ya jamii. Hii hutokana na ubunifu wa mtunzi katika kuakisi na kusawiri uhalisia wa mambo mbalimbali ambayo hutokea katika maisha ya mwanadamu na mazingira yake.

Mapenzi katika aina zake mbalimbali husimamia mafungamano kati ya binaadamu, na kile anachokipenda. Na kutokana na umuhimu wake mkubwa kwa jamii ndio maana ni mionganini mwa maudhui anuai yanayopatikana sana katika kazi za fasihi. Dhamira ya mapenzi ni dhamira moja wapo nyeti, adhimu na muhimu kati ya dhamira mbalimbali zinazoelezwa na waandishi/watunzi wa kazi za fasihi kila uchao, katika tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi. Tukichunguza kazi za fasihi tutagundua kuwa dhamira ya mapenzi haiwezi kuepukika na huweza kusawiriwa kwa namna tofauti kwa mujibu wa madhumuni ya mwandishi/ mtunzi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira.

Istilahi hii ya mapenzi ina maana nyingi, na huweza kuelezwaa kwa namna/aina mbalimbali. Ugiriki ya kale inatambua njia mbalimbali na tofauti ambazo neno mapenzi limetumika kwa mfano *Eros, Philia, Storge, Agape na Xenia*. *Eros* ni Mapenzi ya Kimwili na hii ni aina ya mapenzi ambayo watu wengi hudhani kuwa ndio maana kamili ya mapenzi wakati dhana ya mapenzi ni pana sana. Aina hii inahusishwa na mapenzi ya kimahaba, mapenzi yaliyo na shauku na hamu, kwa mfano mwanamume kumtamani mwanamke au mwanamke kumtamani mwanamume kwa hamu ya kingono tu. Aina nyengine ni Mapenzi ya Urafiki - *Philia*, haya ni mapenzi yanayohusu kutendeana wema, mapenzi yasiyo ya uchu ama hamu ya kingono. Hii ni dhana iliyobuniwa na Aristotle ambayo inahusisha uaminifu kwa

marafiki, familia na hata jamii. Mapenzi ya aina hii huchochewa na sababu za kiutendaji pale ambapo mmoja wa wahusika kufaidika na uhusiano wa mwengine katika kutendeana mema. Aina nyengine ya mapenzi ni Mapenzi ya Familia – *Storge*. Mapenzi haya hupatikana sana kwa wazazi na watoto wao na pia watoto kwa wazazi wao. Aina hii ya mapenzi ni tofauti kidogo ikilinganishwa na ile ya kiurafiki kwa sababu aina hii haizingatii kile mtu anachotendewa bali ni kutokana na nguvu ya uhusiano wa damu. Aidha pamoja na aina hizi, aina nyengine ni Mapenzi ya Kujitolea - *Agape* haya ni mapenzi ya hisani yasiyo masharti wala ubinafsi, mapenzi ya mtu kujitolea muhanga kwa hali yejote ile. Vile vile aina nyengine ni Mapenzi ya Ukarimu - *Xenia*, hii ilikuwa ni jambo la muhimu sana katika Ugiriki ya kale kati ya mwenyeji na mgeni wake ambao hawakufahamiana hapo awali. Mwenyeji alimlisha mgeni wake na kumpatia malazi, na mgeni alipaswa kulipa shukurani pekee. Umuhimu wa jambo hili unaonekana kupitia visasili vya Kigiriki hasa vile vya Homer.

(<https://www.psychologytoday.com/blog/hide-and-seek/201606/the-7-types>)

(<https://thoughtcatalog.com/rania-naim/2016/02/the-7-kinds-of-love-and-how-they-can-help-you-define-yours-according-to-the-ancient-greeks/>)

Msingi hasa wa kuwepo mapenzi ulimwenguni ni kujenga mustakabali mwema wa maisha ya wanadamu katika nyanja zote za maisha kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Tukirejelea maandiko matakatifu ya dini kama vile *Qurani* na *Biblia* tunaona kwamba dhana ya mapenzi haikuachwa kuelezwu kutokana na nafasi na umuhimu wake kwa mwanadamu. Katika *Qurani* sura ya tatu aya ya kumi na nne (3:14) imeandikwa kuwa:

“Watu wametiwa huba ya kupenda wanawake na watoto na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi wanaotunzwa vizuri na wanyama na mashamba. Na hayo ni matumizi ya maisha katika dunia “ (3:14).

Allah anatujuza kuwa watu wametiwa huba ya kupenda, huba ni mapenzi ambapo katika aya hii mapenzi hayo yameegemezwa katika vitu tofautitofauti walivyopambiwa watu kuvipenda sana katika maisha yao. Vitu hivyo ni kama alivyovitaja mwenyewe Mwenyezi Mungu (SW) muumba wa ulimwengu na vyote vilivyomo kuwa ni wanawake, watoto, dhahabu na fedha, farasi wanaotunzwa vizuri na wanyama na mashamba. Haya yote tunaelezwa kuwa ni matumizi ya maisha katika dunia. Kwa upande wa *Biblia* suala la mapenzi/upendo pia limesisitizwa sana.

Katika waraka wa kwanza wa Yohana kwa watu wote aliandika:

“Wapenzi nampendane, kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendae amezaliwa na Mungu. Yeyote asiyependa hakumjua Mungu kwa maana Mungu ni upendo. (1Yoh. 4:7-8).

Aidha mionganini mwa amri kuu sita katika Mathayo inasema:

”Mpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako”.(Mathayo Mtakatifu, sura ya 19. Aya ya 17-19)

Kwa mujibu wa mafundisho ya maandiko haya matakatifu (Qurani na Biblia) suala la mapenzi ni muhimu na kamwe haliwezi kuepukika katika maisha. Kwa sababu upendo ni zawadi kutoka kwa Mungu muumba, Vile vile katika kuhakikisha kuwa mapenzi yana nafasi na thamani kubwa katika maisha ya mwanadamu Robert (1958), katika utangulizi wa diwani yake ya *Mapenzi Bora*: Kitabu ambacho kimeeleza dhana ya mapenzi kwa mawanda mapana sana katika mustakabali wa familia, jamii, na dunia anaeleza kuwa:

“Watu ambao wana dhana kuwa mapenzi si kitu cha maana, wanaonywa kuwa wanapatwa na hasara kubwa kwa kupidwa bila ya kujua uzuri na fahari, heshima na utukufu ambao hustahili kuwa nao wenyewe. Wanamiliki ya majohari ambayo hawajui thamani yake. Baadhi ya watu hudai kuwa mapenzi karaha kuzungumzwa. Watu hawa huwa hawawafunzi wazazi kukaa vyema na watoto wao, wala watoto kuwa wema na amini kwa wazazi wao. Vilevile hawawafunzi watu wajibu wa kutegemea katika dunia hii. Huharibu umoja na ujirani, uaminifu na urafiki, kwa fikra zao za upuuizi. Mapenzi ni jambo moja katika mambo muhimu na wajibu kwa mtu katika maisha yake...”(Robert, 1958: iii)

Maelezo haya yanatudhihirishia wazi kuwa mapenzi ni moja wapo kati ya vitu vilivyo na umuhimu mkubwa sana katika maisha ya mwanadamu, kwa hivyo si jambo la kubezwa ama kupuuzwa hata kigogo. Mapenzi ndio msingi au muhimili imara wa maisha ya watu hapa ulimwenguni. Kutokana na umuhimu wake ndio maana Robert (ameshatajwa) anayamithilisha mapenzi na johari ambayo ni kito cha thamani kubwa sana.

Mwanjoka (2011) amefafanua dhana ya mapenzi katika mashairi ya kizazi kipy. Katika ufanuzi wake Mwanjoka (ameshatajwa), anaeleza kuwa, ni ukweli usiopingika kuwa mapenzi huchukuwa sehemu kubwa ya maisha ya mwanadamu. Na imeandikwa hata kwenye vitabu vya dini (Quran na Biblia) kwamba kuna hatua tatu muhimu ambazo mwanadamu huzipitia: Moja kuzaliwa, pili mapenzi na tatu ni kifo. Hatua zote hizi ni lazima mwanadamu azipitie endapo atazaliwa na kuishi.

Mwanasaikolojia kutoka Marekani Zick (1970) anasema kuwa, mapenzi yanajengwa na vipengele vitatu navyo ni: Upendo, kujali na urafiki. Robert (1986) naye alibuni

nadharia ya miraba mitatu ya mapenzi na anaeleza kuwa, mapenzi yana vipengele vitatu tofauti ambavyo ni urafiki, kujitoa na uchu. Anaendelea kufafanua kuwa, urafiki ni aina ya mapenzi ambayo watu wawili huambiana siri na mambo kadhaa kuhusu maisha yao binafsi. Kujitoa ni kuwajibika kwa upande mwengine ni matumaini, kuwa uhusiano huo ni wa kudumu. Aina ya mwisho inayopatikana sana ni mvuto wa kingono au uchu.

Kimsingi suala la mapenzi ni la kisaikolojia na linaweza kumgusa mtu yeote katika jamii itategemea ni katika mazingira gani ambayo mapenzi hayo yameegemezwa. Masebo (2009) anasema kuwa, mapenzi ni hali ya kuingwa moyoni na kuthamini mtu au kitu zaidi ya mwengine au kingine. Kwa maana hii dhana ya mapenzi haiishii kwa mtu mmoja kumpenda mtu mwengine kwa masuala ya kingono tu laa hasha isipokuwa inahusisha na mambo mengine kama vile kuhurumiana, kuvumiliana, kuthaminiana, kusikilizana, kusaidiana na kuheshimiana baina mtu na mtu. Mapenzi yanaweza kujitokeza mionganini mwa wanandoa, wanafamilia na marafiki. Pia yapo mapenzi ya mtu kulipenda taifa/nchi yake, kabilia lake, dini yake, mali yake na kadhalika. Kwa mnasaba huo basi, mapenzi ni dhana pana sana ambayo haiwezi kuelezea kwa namna moja tu ikatosheleza. Kwa hivyo utafiti huu ulilenga katika Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ili kubaini ni kwa namna gani dhana ya mapenzi imeweza kujitokeza katika riwaya inayotafitiwa.

1.3 Tatizo la Utafiti

Dhamira katika utanzu wa riwaya imediriki kutafitiwa na watafiti wengi sana. Mionganini mwa watafiti hao ni pamoja na: Adam (2014), Msacky (2015), Haji

(2015), Ali (2017) na wengineo. Watafiti hawa wamewasilisha dhamira mbalimbali kama vile matabaka, ndoa, mapenzi, umaskini, ulevi, uvivu na uzembe, wizi na magendo, ukombozi, malezi na nyangi nyenginezo. Mathalani Ali (ameshatajwa) amechunguza dhamira katika riwaya ya *Kiu*. Pamoja na dhamira nyangi alizozieleza katika utafiti wake, alidokeza dhamira ya mapenzi yakiwemo mapenzi ya kingono, ya mali, ya mtu na mtu, ya mtu na nchi yake na mapenzi ya mtu na familia yake ambapo katika utafiti huo ameeleza zaidi mapenzi ya kingono peke yake. Kutokana na hayo, inaonekana kuwa, dhamira ya mapenzi katika riwaya haijaguswa vyakutosha kiutafiti. Kwa hiyo, utafiti huu una lengo la kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed ambayo ni ya miaka ya hivi karibuni (2014).

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu na malengo mahsus mawili yafuatayo:

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed.

1.4.2 Malengo Mahsus

- i. Kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.
- ii. Kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

1.5 Maswali ya Utafiti

- i. Ni kwa namna gani dhamira ya mapenzi imejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*?
- ii. Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti wowote huwa na umuhimu wake kwa namna moja ama nyengine. Kwa mnasaba huo utafiti huu umekuwa na umuhimu katika maeneo yafuatayo:

Kitaaluma: Utafiti huu ni dira katika kutoa taaluma kwa wasomaji, watafiti na wahakiki wajao. Wasomaji na wahakiki hao wataweza kufahamu zaidi dhana ya mapenzi ilivyokuwa na mawanda mapana sana tofauti na ilivyozoleka na kwa hivyo inaweza kuelezwu katika miktadha tofauti. Licha ya hayo, utafiti huu pia umekuwa ni moja wapo ya marejeleo muhimu kwa walimu pamoja na wanafunzi wa sekondari na vyuo wanaosoma somo la fasihi ya Kiswahili hususani katika utanzu wa Riwaya.

Kijamii: Utafiti huu pia ni mwanga utakaoangazia katika kutoa maadili mema hasa ikizingatiwa kwamba suala la mapenzi ni kipengele muhimu sana katika mustakbali mzima wa maisha ya wanajamii. Jamii ye yeyote ile haiwezi kuendelea katika nyanja zote za maisha pasi na kuwepo mapenzi ambayo hujenga ule moyo wa kupendana, kusaidiana na kushirikiana katika kutatua matatizo mbalimbali ya kijamii na ya mtu binafsi.

1.7 Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vya utafiti ni jumla ya mambo ambayo husababisha ugumu katika utafiti wa kielimu na kupelekea kutokukamilika kwa wakati muafaka unaotarajiwa. Miongoni mwa vikwazo ambavyo mtafiti alikutana navyo ni pamoja na ukosefu wa marejeleo hususan kazi tangulizi zikiwemo tasnifu na makala nyenginezo zenye uhusiano na mada ya utafiti.

1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti

Utatuzi wa vikwazo vya utafiti ni jambo muhimu katika kufanikisha suala zima la utafiti. Hivyo katika kuhakikisha kazi hii imekamilika kwa wakati, mtafiti alitumia muda wake mwingi katika kutalii mapitio ya maandishi kupitia vyanzo mbalimbali kama vile katika mtandao na maktabani. Kusoma kazi mbalimbali ambazo zilimkinaisha na hatimae kupata taarifa sahihi zilikazohusiana na utafiti wake. Ili kupata taarifa hizo mtafiti alilazimika kusoma machapisho mbalimbali katika Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Maktaba Kuu ya Zanzibar katika matawi yake ya Pemba, pamoja na matumizi ya mitandao/tovuti/wavutti.

1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unahu: *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed. Riwaya kwa ujumla hujikita katika kujadili masuala muhimu yanayohusu jamii katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile kisiasa kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Hivyo utafiti huu umenuia kuchunguza dhamira ya mapenzi ambapo uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Simiotiki. Mtafiti kamwe hakuhusika na dhamira nyengine.

Dhamira iliyoshughulikiwa ni dhamira ya mapenzi pekee katika miktadha au aina zake mbalimbali.

Mbali na hilo mtafiti anatambua kuwa, Said Ahmed Mohamed ameandika riwaya mbalimbali kama vile *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988) *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) *Mkamandume* (2013) *Kamwe si Mbali Tena* (2014) na *Wenye Meno* (2018). Hivyo basi utafiti huu haukuhusika na uchunguzi wa riwaya nyengine yoyote isipokuwa riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Riwaya nyengine za mwandishi Said A. Mohamed na wengineo zimetumika kama kazi tangulizi na kuongezea maarifa kwa kadiri inavyostahili kulingana na mada ya utafiti.

1.9 Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu umejumuisha sura tano kuu. Sura ya kwanza ni ya utangulizi ambayo imejikita katika usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti pamoja na utatuzi wake mipaka ya utafiti na kumalizia na Mpangilio wa tasnifu.

Sura ya pili imehusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura hii imeangazia ufanuzi wa istilahi mbalimbali zenye uhusiano na utafiti husika, chimbuko la riwaya ya Kiswahili, mapitio ya kazi tangulizi kuhusu dhamira katika riwaya, mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za Said Ahmed Mohamed pamoja na kiunzi cha nadharia teule ambazo ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na

nadharia ya Simiotiki zimetumika katika utafiti huu na mwisho sura imemalizia na hitimisho.

Sura ya tatu imejumuisha mbinu za utafiti. Vipengele vilivyohusika ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, ukusanyaji wa data za utafiti, sampuli na usamplishaji, data za utafiti, uchambuzi wa data, mbinu za uchambuzi wa data, zana/vifaa vya utafiti na mwisho ni hitimisho.

Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Sura hii imehusisha muhtasari wa riwaya teule, historia ya mwandishi wa riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena* ambaye ni Said Ahmed Mohamed, Uwasilishaji na uchambuzi wa lengo mahsusla la kwanza na swali la kwanza la utafiti kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Sambamba na hilo uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti kwa lengo mahsusla la pili na swali la pili umefanyika ipasavyo kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki na mwisho ni hitimisho.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti kwa mujibu wa malengo mahsusla ya utafiti huu pamoja na maswali ya utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo kwa watafiti wajao. Sura inayofuata ni Mapitio ya Kazi tangulizi na Mkabala wa Kinadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alijikita zaidi katika kujadili kazi tangulizi zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali waliotangulia na kujenga hoja ambazo ziliupeleka mbele utafiti huu. Pamoja na hayo, sura hii imetoa ufanuzi wa dhana/istilahi zenye uhusiano na mada husika. Vilevile sura hii imemelea chimbuko la riwaya, pengo la utafiti, mkabala wa kinadharia pamoja na sababu za kuchaguliwa nadharia teule na kumalizia na hitimisho.

2.2 Ufanuzi wa Istilahi Muhimu

Katika utafiti huu istilahi mbalimbali muhimu zimefafanuliwa kulingana na mada ya utafiti husika.

2.2.1 Maana ya Riwaya

Dhana ya riwaya imewahi kujadiliwa kwa kina na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na: Ndungo na Mwai (1991) ambao wanaeleza kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mchangamano wa visa ambayo huchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kimaudhui na kifani.

Wamitila (2003) anasema kuwa riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchukua muda mwangi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalumu. Madumulla (2009) anaeleza kuwa, riwaya ni

masimulizi mrefu ya kubuni yaliyo katika mtindo wa nathari, yakisawiri maisha ya mtu wa wakati maalumu na kwa madhumuni maalumu.

Kwa ujumla, mtafiti wa kazi hii ameshawishika na fasili za wataalamu hawa na kumalizia kusema kuwa, riwaya ni utungo wa kinathari uliobuniwa na ulio na urefu wa kiasi cha kutosha kinachowezesha usawiri wa wahusika wake mbalimbali na matendo yao yenye kushabihiana na uhalisia wa maisha ya jamii husika. Dhana ya riwaya imelazimika kufafanuliwa katika utafiti huu, kwa kuwa ndio utanzu ambao umeshughulikiwa. Riwaya iliyoteuliwa kwa mujibu wa mada husika ni *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed.

2.2.2 Historia na Chimbuko la Riwaya

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu historia na chimbuko la riwaya, kwa mfano: Mlacha na Madumulla, (1995) wanaeleza kuwa; Historia ya riwaya ulimwenguni haina muda mrefu sana hasa inapolinganishwa na historia ya tanzu nyengine za fasihi kama vile utanzu wa ushairi, tamthilia na fasihi simulizi ambao una karibu umri sawa na historia ya mwanadamu. Madumulla (2009) anafafanua kuwa riwaya ilizuka katika kipindi cha mwamko wa sanaa huko barani Ulaya, na mionganini mwa riwaya za mwanzo ni ile ya *Robinson Crusoe* (1719) iliyoandikwa na Daniel Defoe ikifuatiwa na *Pamela* (1740) ya Samwel Richardson. Sambamba na hilo, riwaya ya mwanzo ya *Robinson Crusoe* ilizuka kutokana na maendeleo na mabadiliko ya uvumbuzi wa viwanda hali ambayo ilistawisha uandikwaji na usomaji wake kupanuka. Riwaya hizi zililetu mabadiliko makubwa na kusawiri kwa kina maisha ya jamii katika uhalisi wake, ambapo vipengele vyote vya maisha kama vile kisiasa, kiuchumi na kijamii katika uchangamano wake wa kifani na kimaudhui

vilihusishwa. Pamoja na hayo, ziliimarisha zaidi matumizi ya lugha na mazingira yaliyozoleka. Kutokana na hali hiyo uwandishi wa riwaya ulizaliwa, ukapea na kupata ukomavu katika kipindi cha robo karne.

Kwa upande wa bara la Afrika riwaya ina historia fupi sana ikilinganishwa na Ulaya, hii ni kutokana na kuchelewa kwa elimu hasa ile ya kimagharibi ambapo riwaya zote zilianza kuitumia. Kwa mujibu wa Madumulla (ameshatajwa) riwaya katika bara la Afrika ilianza Afrika Kusini na Afrika ya Magharibi na baadae iliendelea Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kati. Inasadikiwa kuwa shughuli za Kimisionari ndizo zilizoeneza elimu ya Kimagharibi katika bara la Afrika. Kuzuka kwa maandishi mnamo karne ya 19 ambapo kuliandamana na mapinduzi ya viwanda ndiko kulikopelekea maandiko ya kifasihi kama vile ngano kuanza kuandikwa, na hapa ndipo inaposadikiwa kuwa utanzu wa riwaya ya Kiswahili ulichipuka kwa sababu kuna mambo ambayo yalijitokeza na yalihitaji kuelezwu kwa mawanda mapana sana. Nchini Tanzania utanzu wa riwaya ulijitokeza katika kipindi cha ukoloni ambapo kazi ya kwanza ya nathari ya kibunifu ni *Uhuru wa Watumwa* iliyoandikwa na James Mbotela (1934) kisha zikafuata riwaya za Shaaban Robert kama vile *Kusadikika* (1951) *Adili na Nduguze* (1952) na *Kufikirika* (1952).

Msokile (1992) anaeleza chanzo cha riwaya katika fasihi ya Kiswahili imetokana na hadithi na ngano ambazo zilisimuliwa hapo kale na bibi/babu kwa nia na madhumuni ya kuitanabahisha jamii juu ya masuala mbalimbali, masimulizi hayo yalipokelewa kutoka kizazi hadi kizazi pasi na kuandikwa kama ilivyo ada ya fasihi simulizi. Madumulla (2009) anasema kuwa, riwaya ya Kiswahili chanzo chake ni nathari bunifu simulizi kama vile hadithi, hekaya na ngano zinazosimuliwa kwa mdomo.

Senkoro (2011) naye anaeleza kuwa riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kiutamaduni, uchangamano na maisha ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni yaliyopelekea haja ya kimaudhui zaidi ya ngano na hadithi fupi.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa chimbuko la riwaya lipo katika mambo mawili makuu ambayo ni fani za kijadi na mazingira ya kijamii. Anafafanua zaidi kuwa utanzu wa riwaya haukuanza hivi hivi, bali ultokana na fani za kijadi za masimulizi zilizokuwepo hapo awali yaani kabla ya utanzu huu kuwa katika hali ya maandishi. Mulokozi (ameshatajwa) anazitaja tanzu hizo za kijadi zilizochangia kuchipuka kwa riwaya ya Kiswahili kuwa ni pamoja na ngano, hekaya, tendi, visakale, tarihi/historia, insha na tafsiri, masimulizi na nyenginezo. Maelezo haya ya Mulokozi (ameshatajwa) hayapingani sana na yale ya Robert Scholes na wenzake ambaye amenukuliwa na Madumulla (2009) akisema kuwa, riwaya imetanguliwa na namna tatu za maandiko marefu ambayo ni Visasili, Romansi na Tawasifu.

Maelezo ya Senkoro (ameshatajwa) ndio ambayo yanatupa sura ama picha halisi ya riwaya ya Kiswahili ilivyo hivi sasa. Hii ni kutokana na riwaya kuchupa kwake mipaka ya kimaudhui ikilinganishwa na ngano na hadithi fupi zilivyokuwa hapo awali. Kwa mantiki hii tunaona kwamba riwaya ya Kiswahili, leo hii imevuka mipaka katika vipengele vya kifani na kimaudhui, ambapo kwa mawanda mapana zaidi hujadili masuala mbalimbali yahusuyo maisha ya mwanadanu na mazingira yake katika nyanja zote za maisha kama vile kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Katika utafiti huu riwaya iliyotafitiwa ni *Kamwe si Mbali Tena* (2014) ya Said Ahmed Mohamed

2.2.3 Maana ya Dhamira

Dhamira ni mionganini mwa kipengele kikuu cha maudhui kinachoelezwa katika tanzu za fasihi ukiwemo utanzu wa riwaya. Wanawazuoni mbalimbali wa taaluma ya fasihi ambao wameeleza maana ya dhamira ni pamoja na:

Ndungo na Wafula (1993) wanasema kuwa dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi /msanii katika kazi ya fasihi. Wanaendelea kusema waandishi huwa wanazigawa dhamira katika makundi mawili ambayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Wamitila (2008) ameifasili dhamira na kusema kuwa, ni yale mawazo makuu yanayowasilishwa na mwandishi wa kazi ya fasihi kama mafunzo, maonyo, maadili, hekima na busara zinazopaswa kuigwa na wanajamii ili kuifanya jamii kuwa na ustawi mzuri.

Kwa mantiki hiyo basi, mtafiti anahitimisha kwa kusema kuwa, dhamira ni ile azma, lengo au kusudio la mwandishi katika kazi yake ya fasihi ambalo huwa na muitiko fulani katika jamii husika. Kila mwandishi huwa amesukumwa na jambo fulani katika utunzi wake, jambo hilo linaweza kuwa zito au jepesi, zuri au baya ilimradi tu liweze kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Maana hii ya dhamira haina budi kufafanuliwa na kuelezwaa kwa sababu ndio msingi mkuu wa uchunguzi wa utafiti huu unaokusudia kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

2.2.4 Maana ya Mapenzi

Dhana ya mapenzi ni pana sana, kila mtu huweza kupata maana kulingana na uelewa wake. Wapo wanaodhani kuwa mapenzi ni ile hali ya watu kuwa na mahusiano ya kimwili tu. Kimsingi neno mapenzi lina maana nyingi kulingana na maongezi yanayozunguka neno hilo. Mapenzi ni neno la Kiswahili linalojumuisha idadi kadhaa ya hisia, kuanzia mahaba, upendo kwa mtu ama upendo kwa Mungu (www.yourdictionary.com/love). BAKIZA (2010) wamefasili mapenzi kuwa ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini, na ajali mtu, kitu au jambo fulani.

Kwa ujumla mapenzi ni tabia ya kimaumbile ya mtu kupenda kitu chochote kile kisha akakiingiza katika moyo wake wote, na kuathirika nacho kwa hisia za ndani pamoja na kuafikiana nacho kwa hali yoyote ile. Dhana ya mapenzi aidha imehusika katika ufanuzi wa istilahi muhimu kwa mintaarafu ya kuwa ndio kiini hasa cha utafiti huu.

2.2.5 Mbinu za Kisanaa

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004) anasema kuwa, kwa kawaida mbinu za kisanaa/kifani huwa na maingiliano au uhusiano mkubwa na dhamira katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008) anafasili mbinu za kisanaa kuwa ni ule ufundi ambao mwandishi wa kazi ya fasihi hutumia katika kiumba kazi yake ya kifasihi na kuipa uwezo wa kuwasilisha dhamira zilizokusudiwa kwa hadhira. Anaendelea kusema mionganii mwa mbinu za kisanaa zinazotumika katika kuwasilisha mawazo ama fikra za mwandishi kwa hadhira lengwa ni pamoja na: Wahusika na mandhari ambayo inakwenda sambamba na kile anachokieleza mwandishi, muundo, mtindo pamoja na

matumizi ya lugha teule iliyosheheni vionjo mbalimbali kama vile tamathali za usemi, methali, na mbinu nyengine za kisanaa. Ufanuzi wa mbinu hizo za kisanaa zilizotumika katika utafiti huu ni kama ifuatavyo:

2.2.5.1 Wahusika

Kazi yoyote ya fasihi huwa na wahusika ambao wamebuniwa na msanii katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Ufanisi wa uwasilishaji wa ujumbe wa msanii mbali na kutumia lugha teule vilevile hutumia usawiri wa wahusika ambao hupewa maneno, tabia, vitendo na hulka tofauti ambazo hutusaidia kubaini hali ya muhusika kama vile ni mwenye mapenzi, mpigania haki, mzalendo, jasiri na kadhalika.

Senkoro (2011) anafasili dhana ya wahusika kwa kusema kuwa, wahusika ni watu au viumbe waliokusudiwa kuwakilisha dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi ya fasihi. Wamitila (2002) anaeleza wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile, viumbe hawa huwa ni sehemu ya kazi nzima. Wamitila (ameshatajwa) anakwenda mbali zaidi na kueleza kuwa, wahusika ni binaadanu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, kifalsafa ambazo hutambulishwa na mazungumzo na matendo na pia huweza kutambulishwa na maelezo ya msimulizi. Msingi wa hisia, hali ya kimaadili, mazungumzo na matendo anayobebeshwa muhusika ndio kiini cha kumjenga muhusika katika kazi ya fasihi. Ntarangwi (ameshatajwa) anafafanua kuwa, wahusika katika kazi ya fasihi kuwa ni viumbe vya hadithini vilivyobuniwa na msanii ili kuendeleza hoja na maudhui yake katika kazi husika. Wahusika husaidia

katika kuendeleza mada nzima hususan katika mfululizo wa vitushi na visa mbalimbali katika kazi ya fasihi.

Kwa kutamatisha mtafiti anaweza kusema kuwa, wahusika ni watu ama viumbe vyengine ambavyo hutumiwa na mtunzi wa kazi ya fasihi pamoja na kubebeshwa dhima mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira inayokusudiwa. Wahusika ni muhimu sana katika kuijenga hadithi, dhamira, na maudhui ya kazi nzima ya fasihi kutokana na yale wanayoyawasilisha kwetu ambayo hutupatia ujumbe fulani. Kwa kuwa wahusika ndio wanaotumika kupaza sauti ya mwandishi kuwasilisha dhamira, dhana ya wahusika imejadiliwa kama mbinu ya kisanaa ambayo imetumika katika kufanikisha utafiti huu.

2.2.5.2 Matumizi ya Lugha

Kazi ya fasihi ni ujumbe unaotolewa na mwandishi kupitia malighafi ya lugha ambayo huwa ndio roho ama uti wa mgongo unaotumiwa na msanii katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Jilala (2014) anasema lugha ni kielelezo cha jamii na kiwakilishi cha utamaduni ambacho hubeba dhana za kiisimu kama malighafi ya jamii husika, utamaduni huweza kuelezwa kikamilifu na lugha ya jamii husika. Kwa maana hiyo, matumizi ya lugha katika kazi za fasihi huambatana na ishara, taswira na tamathali mbalimbali za usemi ambazo hupelekea msomaji wa kazi fulani ya kifasihi kuweza kupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi katika kazi husika. Hivyo basi kipengele cha lugha kina nafasi kubwa katika utafiti huu kwa sababu ndio uti wa mgongo wa kazi ya sanaa ya fasihi kwa mnasaba wa mada husika.

2.2.5.3 Mandhari

Mandhari ni mionganini mwa mbinu za kisanaa/kifani ambazo zina nafasi kubwa katika kuiumba kazi ya kifasihi. Senkoro (1982) anafafanua mandhari kuwa ni mazingira ya kazi ya fasihi, ni ile hali ya maumbile ilivyo na inavyoonekana. Mazingira hayo hutumika katika kujenga masimulizi ya riwaya, tamthilia au hadithi fupi. Njogu na Chimerah (1999) nao wanaeleza kuwa, mandhari ni kipengele kimojawapo ambacho husaidia kuibua dhamira katika kazi ya kifasihi. Inategemea muundo wa mandhari ulivyojengwa na mwandishi katika kisa anachosimulia. Wamitila (2002) anaeleza mandhari kuwa, ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Mandhari hutumiwa kuelezea sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili pia huweza kutumiwa kwa mapana kuelezea mazingira ya kisaikilajia ya tendo fulani.

Kwa ujumla mandhari ni sehemu ambayo matukio katika kazi ya kifasihi huchukuwa nafasi. Mandhari ya kazi ya kifasihi huweza kuibua dhamira kwa kuhusishwa na wahusika na matendo yao. Mtafiti ameweka bayana baadhi ya mbinu za kisanaa/kifani ambazo zilimsaidia sana katika kulifikia lengo mahsus la pili, sambamba na swalii la pili la utafiti. Mbinu hizo zilizofafanuliwa hapo juu zimetumika vyema kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni kipengele muhimu sana, na ndio uti wa mgongo wa utafiti wowote ule wa kitaaluma, ambapo huhusisha usomaji wa kina wa maandiko mbalimbali yanayolingana na mada husika ya utafiti. Omari (2012) anaeleza kuwa

kazi tangulizi hutoa ujuzi au maarifa ya wanawazuoni waliowahi kufanya kazi zenye mwelekeo na lengo la utafiti. Vile vile kazi tangulizi humsaidia mtafiti kutambua mambo yepi yamefanyiwa utafiti na yepi bado. Pia kazi tangulizi ni marejeleo yenye maono na maarifa kuhusu kweli zilizoko huko nyuma. Kwa mnasaba wa mada ya utafiti mapitio ya kazi tangulizi yamegawanywa katika sehemu mbili: Mosi; Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu dhamira katika riwaya kwa ujumla. Pili; Mapitio ya kazi tangulizi katika riwaya za Said Ahmed Mohamed.

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kuhusu Dhamira katika Riwaya kwa Ujumla

Mada ya utafiti huu: *Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*. Wanazuoni wametafiti mada mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili ikiwemo mada ya Dhamira. Mfano wa watafiti waliojikita katika tafiti za riwaya ni: Kezilahabi (1976), Adam (2014), Haji (2015), Msacky (2015) na Ali (2017).

Kezilahabi (1976) aliandika tasnifu isemayo: “*Shaaban Robert, Mwandishi wa Riwaya*” Katika kazi yake anasema kuwa dhamira ya utu, ambayo msingi wake mkuu ni mapenzi pamoja na heshima kwa mwanadamu ndio dhamira kuu katika kazi za Shaaban Robert. Kezilahabi anamsifu Shaaban Robert kuwa katika kazi zake ameweza kuyasawiri vyema masuala nyeti yahusuyo maisha ya mwanadamu. Katika tasnifu yake anaeleza kuwa kazi za Shaaban Robert huzungumzia masuala ya upendo/ mapenzi, wema, amani, busara kuwa ni mambo muhimu sana ya kujipamba nayo kila mwanadamu kutokana na umuhimu wake mkubwa katika jamii na katika dunia kwa ujumla. Maelezo haya ya Kezilahabi (ameshatajwa) yamekuwa ni msaada mkubwa katika kuupeleka mbele na kuufanikisha utafiti huu. Ni ukweli usiopingika

kwamba suala la upendo/mapenzi ndio msingi bora na imara wa maisha ya mwanadamu. Utafiti huu umemsaidia sana mtafiti katika kupata maarifa hasa kwa vile umetaja suala la mapenzi likielezwa kuwa ni pambo analostahiki kujipamba nalo kila mwanadamu. Hivyo utafiti huu unalenga katika kuchunguza dhamira hiyo ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Adam (2014) amechunguza mada “*Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya ya Kiswahili, Kuli na Vuta N’kuvute*”. Mtafiti huyo anaeleza kuwa, katika riwaya mapenzi yamesawiriwa kwa namna mbalimbali kama vile mapenzi ya mtu na mtu, mapenzi ya mke na mume na mapenzi ya mzazi na mtoto wake. Katika kazi yake ametaja dhamira ya mapenzi kuitia riwaya ya *Vuta N’kuvute* huku akionesha aina ya mapenzi yaliyomo, mfano mapenzi ya Bwana Raza kwa Yasmini, mapenzi ya Yasmini kwa Mwajuma na mapenzi ya Yasmini kwa mama yake. Kiudhati kazi hii imemsaidia sana mtafiti na kuwa ni tochi iliyomuangazia katika safari ya utafiti wake. Mawazo ya Adam (ameshatajwa) yamekuwa na umuhimu mkubwa kuzingatiwa katika utafiti huu wenyewe mada: *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*, hasa ikitiliwa maanani kama ilivyoelezwa kuwa mapenzi yanawiriwa katika namna mbalimbali. Hivyo mtafiti alidhamiria kuchunguza dhamira ya mapenzi kubaini namna ilivyojitezea katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Ali (2015) amefanya utafiti kuhusu mada: “*Kuchunguza Dhana Zilizobebwa na Wahusika na Zinavolandana na Majina yao katika Riwaya ya Kiu na Kiu ya Haki*”. Katika utafiti wake ameleeza dhamira zinazojengwa na wahusika. Miongoni mwa dhamira hizo ametaja dhamira ya mapenzi. Ameeleza kuwa katika riwaya ya *Kiu*

suala la mapenzi limejitokeza katika sura tofauti kupitia wahusika wake; ametaja mfano Bahati ambaye alipata bahati ya kupendwa na mzee Mwinyi, mzee tajiri. Vilevile Bahati anapendwa na Iddi ingawa mapenzi ya Iddi kwa bahati hayakuwa ya dhati bali ni kwa lengo la kumfanya chanzo cha mapato tu. Utafiti wa Ali (ameshatajwa) umetoa mwanga kwa kutaja sura tofauti za mapenzi na hivyo kumpa nafasi mtafiti ya kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Haji (2015) ametafiti: *Upande wa pili wa Riwaya teule za Shafi Adam: Dhamira zilizofichama katika riwaya ya Kuli na Vuta N'kuvute*. Katika tasnifu yake ameeleza dhamira mbalimbali zilizofichama kupitia vipengele kama vile methali, nyimbo, majina ya wahusika nakadhalika. Moja wapo ya dhamira hizo ni dhamira ya mapenzi ambayo imejitokeza katika miktadha tofauti mfano, ametaja mapenzi ya mama juu ya watoto wake, na mapenzi baina ya wawili wapendanao akitoa mfano wa Amina na Rashidi. katika riwaya ya *Kuli*. Vile vile amedokeza mapenzi ya mtu na nchi yake, mfano Denge na Yasmini katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Utafiti wa Haji (ameshatajwa) umemsaidia sana mtafiti wa kazi hii katika kuiendea kazi yake kwa vile amebainisha miktadha tofauti ya mapenzi kama vile mapenzi ya mama kwa watoto wake, mapenzi baina ya wawili wapendanao na mapenzi ya mtu na nchi yake. Tofauti ya utafiti wa Haji (ameshatajwa) na utafiti huu ni kuwa ye ye ameitaja dhamira ya mapenzi miongoni mwa dhamira nyingi alizozieleza katika riwaya za Shafi Adam; lakini utafiti huu umejikita kuangazia dhamira ya mapenzi peke yake katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed.

Salim (2015) naye amechunguza “*Ufasihi Simulizi unaojitokeza ndani ya Kusadikika na Adili na Nduguze*”. Katika kazi hiyo Salim (ameshatajwa) ameeleza dhamira mbalimbali zilizojitokeza. Miongoni mwa dhamira hizo ni ujasiri, umuhimu wa elimu, uongozi bora, malezi na ukombozi. Pia ametaja dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Matokeo ya utafiti wake Salim (ameshatajwa) anatujuza kuwa mapenzi yana ncha mbili, kwamba yapo mapenzi ya kweli na mapenzi ya uongo. Akifafanua dhana ya mapenzi ya kweli amesema, mapenzi ya kweli ni yale mapenzi ya dhati ya mtu kuwa tayari kumsaidia yule ampendae kwa lolote na kwa chochote, kwa hali na mali. Kwa upande wa mapenzi ya uongo ameyataja kuwa ni kinyume chake, kwamba mwenye mapenzi ya uongo huwa hajali chochote wala lolote dhidi ya yule ampendae. Kwa mnasaba huu basi, kwa vile Salim (ameshatajwa) ameainisha mapenzi ya dhati na mapenzi ya uongo, utafiti wake unakuwa dira iliyomwongoza mtafiti kuchunguza kwa kina dhamira ya mapenzi katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena* na kubaini ni kwa namna gani dhamira hii ya mapenzi ilivyojitekeza.

Msacky (2015) ametafiti mada: *Dhamira za Kijamii na Kisiasa, katika Riwaya ya Siri za Maisha*. Katika utafiti wake kwa upande wa dhamira za kijamii ametaja dhamira mbalimbali kama vile umaskini, ulevi, uvivu na uzembe na nyenginezo. Hata hivyo Msacky (ameshatajwa) katika kazi yake hakutaja dhamira ya mapenzi kuwa ni mionganini mwa dhamira za kijamii. Kwa mantiki hiyo utafiti wake umetoa msukumo mkubwa kwa mtafiti wa kazi hii kuweza kuchunguza dhamira hiyo kwa kina katika utafiti wake hasa tukitilia maanani kuwa, dhamira ya mapenzi ni mionganini mwa dhamira za kijamii ambazo huelezwa na waandishi wa fasihi kwa

namna mbalimbali kama walivyoeleza watafiti waliotangulia. Sambamba na hilo, dhamira ya mapenzi ndio msingi wa kufanikisha utafiti huu kwa mnasaba wa riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Mbarouk (2016) amefanya utafiti *Kuchunguza Matumizi ya Tamathali za Semi katika Riwaya ya Haini*. Katika tasnifu yake ameeleza kuwa matumizi ya tamathali za usemi huibua dhamira mbalimbali kwa sababu mionganini mwa kazi za tamathali katika sanaa ya fasihi ni kuifanya iwe na ladha na isionekane ovyo ama chapwa. Mbarouk (ameshatajwa) katika matokeo ya utafiti wake, amebainisha dhamira chomozi zinazotokana na tamathali za usemi kama vile dhamira ya ujasiri, woga na hofu, ulevi, udhalilishaji, mauaji, uongozi mbaya, uasharati na nyingi nyenginezo. Pamoja na dhamira hizo pia amedokeza dhamira ya mapenzi ya dhati. Kwa minajili hiyo utafiti wake umekuwa na manufaa kwa mtarufi katika kwenda kuichunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya iliyoteuliwa ambayo ni riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Hatimae Ali (2017) naye katika tasnifu yake yenye mada: *Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya Kiu*. Mtarufi anaeleza kuwa, dhamira ya mapenzi ni moja wapo ya dhamira inayojitokeza sana katika kazi ya fasihi andishi na fasihi simulizi kwa namna tofautitofauti. Anasema kuwa wapo watunzi wanaosawiri dhamira ya mapenzi ya kingono, mapenzi ya mtu na mtu, mapenzi ya mtu na nchi yake, mapenzi ya mtu na familia yake, mapenzi ya mtu na ndugu yake na mapenzi ya mtu na mali yake hutajwa kwa uchache. Katika tasnifu yake Ali (ameshatajwa) ameonesha mapenzi ya kingono tu mionganini mwa namna hizo tofauti ambazo amezitaja. Anasema kuwa mapenzi haya ni mapenzi yasiyo ya dhati na ameyaita mapenzi ya

kingono, mapenzi ya mtu kutosheleza hamu ya kimwili kutokana na kumpenda mtu kwa sababu ya kitu tu basi mfano mali, cheo na vyenye kufanana na hayo. Kazi ya Ali (ameshatajwa) nayo pia imemsadia mtafiti katika kufahamu namna dhamira ya mapenzi inavyosawiriwa katika kazi za fasihi na hivyo kutoa fursa ya kuzamia na kuchunguza kwa kina dhamira hii kwa upeo mpana kwa kurejelea riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Kwa muhtasari kazi tangulizi kuhusu dhamira katika riwaya zilizotafitiwa na wafafiti waliotangulia kiudhati zimemsaidia mtafiti katika kukuza uwelewa juu ya masuala mbalimbali yanayohusu jamii likiwemo suala nyeti la mapenzi. Hivyo basi dhamira ya mapenzi ndio suala ambalo utafiti huu unalenga kwenda kuchunguza kwa upana wake katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena*, kwa kurejelea mada ya utafiti huu: *Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali tena ya Said Ahmed Mohamed*.

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed

Prof. Said Ahmed Mohamed ni mionganini mwa waandishi mashuhuri sana wa kazi za fasihi ambaye ameandika kazi nyingi katika fani za riwaya, tamthilia, hadithi fupi, ushairi na hata makala za kitaaluma. Mtafiti alifanya utalii wa baadhi ya maandiko ya watafiti watangulizi, hususani katika utanze wa riwaya ambao ndio utafiti wetu umeangazia. Maandiko hayo yalimsaidia sana mtafiti kufahamu juhudii za watangulizi wake katika kazi za mwandishi na namna walivyotoa maoni yao kuhusiana na dhana ya mapenzi katika kazi zake. Mionganini mwa maandiko ya watangulizi hao ni pamoja na:

Aiello, (1999) katika makala yake yenyewe mada isemayo; *Mabadiliko ni maumbile yenyewe: The thematic and Stylistic Dynamism in Said Ahmed Mohamed's Novel Utengano*" anaeleza kuwa;

“....Mwishihi mwa riwaya kama ilivyo katika hadithi. Maimuna anakutana na Kabi mvuvi mdogo aliyekuwa na ulemavu. Wahusika wawili hawa uhusiano wao ulijikita katika mapenzi ya kweli na heshima na hakuwa na nafasi ya kuuvunja. (T.Y).

Mtafiti amenufaika na makala hii kutokana na kuelezwu ndani yake suala la mapenzi ya kweli baina ya wawili wapendanao. Mapenzi ya kweli yaliyojitokeza baina ya Maimuna na Kabi ambao walipendana kwa dhati katika mapenzi yao ambayo hatimae yalizaa ndoa imara na yenyewe heshima. Hali hii imeonesha wazi kuwa mwandishi Said Ahmed Mohamed, kazi zake zina mchango mkubwa kwa jamii katika nyanja mbalimbali za maisha ikiwemo kisasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Makala hii imetua mwanga kwa mtafiti na kumpa fursa ya kuiangazia dhamira ya mapenzi zaidi katika riwaya yake ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Ann (2013) ameangalia “*Usasa na Mwanamke wa Kisasa katika Nyuso za Mwanamke*”. Katika utafiti wake ameeleza kuwa mwanamke wa kisasa ni mwenye mapenzi ya dhati, mapenzi hayo ndio ambayo hatimae huibua ndoa bora iliyojengwa kwa misingi imara na madhubuti baina ya wapendanao. Utafiti wa Ann (ameshatajwa) kwa namna moja ama nyengine nao umemsaidia mtafiti katika kuchunguza dhamira hii ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* iliylengwa kufanyiwa utafiti.. Makusudio ya kufanya hivyo ni kubaini muktadha wa mapenzi uliojitokeza hasa tukizingatia kuwa, Saidi A. Mohamed katika kazi zake zote takribani anaisawiri/anaichora kwa kina dhamira ya mapenzi au kama

anavyoeleza Mbatia (1990) kuwa ni mwandishi ambaye kazi zake nyingi zinasawiri mazingira halisi ya jamii yake.

Said (2015) amefanya utafiti wenye mada: “*Matumizi ya Ndoto na Uhalisi wa Maisha katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed*”. Katika tasnifu yake anaeleza kuwa ujumbe na maana zinazopatikana katika ndoto huakisi uhalisi wa maisha ya jamii husika kwa namna fulani kutokana na vielelezo vya mandhari iliyotumika. Wahusika huhusishwa na matukio ya kindoto yanayosibu sifa na tabia zilizomo katika jamii. Katika utafiti wake Said (ameshatajwa) ametoa mfano wa ndoto katika riwaya ya *Asali Chungu*. Ndoto inayohusu Mzee Shaabani na Bwana Bopa, ndoto ambayo inaonesha Bwana Bopa akimfukuza mzee Shaaban na bunduki na kumtupia marisau na yote haya ni kwa sababu ya mapenzi. Kutokana na hali hiyo utafiti wake umetoa fununu katika suala la mapenzi na kumpa hamu mtafiti ya kuchunguza dhamira hiyo katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena*.

Wanyonyi (2015) ameandika makala isemayo; “*Ishara na Uashiriaji kama Nyenzo ya Mtindo, Maana na Kiwakilishi cha Itikadi katika Riwaya ya Nyuso za Mwanamke ya Said Ahmed Mohamed*”. Katika makala hiyo ameeleza kuwa, kuna ishara mbalimbali ambazo zinaashiria mapenzi ya dhati katika riwaya hiyo, ametoa mfano wa ishara ya kipepeo ambayo imejitokeza katika wimbo ambao ultungwa na muhusika Fesal ambaye anaonekana akiomboleza huzuni zake baada ya kunyimwa Bimkubwa msichana aliyempenda kwa dhati na hatimae kwenda kuozwa kwa bwana mwengine. Makala hii imemsaidia mtafiti kwa kiasi kikubwa katika

kuchunguza dhamira hiyo ya mapenzi kwa mawanda mapana katika riwaya teule ya *Kamwe si Mbali Tena.*

Fakih (2017) naye amechunguza “*Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena: Utafiti Linganishi*” Katika utafiti wake amemuonesha mwanamke katika usawiri tofautitofauti. Mionganini mwa usawiri huo amemueleza mwanamke kuwa ni mtu mwenye mapenzi ya dhati. Hivyo kutokana na mawazo ya Fakih (ameshatajwa) inatudhihirishia wazi kuwa Said A. Mohamed pamoja na dhamira mbalimbali ambazo anazieleza katika kazi zake, pia anazungumzia mapenzi ya dhati na yasiyo ya dhati. Hivyo utafiti wa Fakih (ameshatajwa) umekuwa ni dira iliyomuongozaji mtafiti katika safari ya utafiti huu unaohusu kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya mwandishi nguli Said Ahmed Mohamed

Jesse (2017) alitafiti kuhusu: *Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.* Riwaya alizozichagua katika utafiti wake ni *Asali Chungu, Kiza katika Nuru, Dunia Yao na Mhanga Nafsi Yangu.* Katika tasnifu yake amaeonesha itikadi ya mwandishi katika mifumo mbalimbali kama vile itikadi ya Kimwinyi, itikadi ya Kibepari, itikadi ya Mapinduzi na itikadi ya Utandawazi. Katika kazi hiyo ameeleza itikadi ya mwandishi kupitia riwaya zote nne (4) zilizotafitiwa, ambapo ndani yake kumejitokeza vipengele mbalimbali kama vile elimu, ndoa, utamaduni pamoja na mapenzi. Kwa mantiki hiyo utafiti wa Jesse (ameshatajwa) nao kwa kiasi kikubwa umempa mtafiti msukumo wa kuangazia dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* kwa mnasaba wa mada ya utafiti: *Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed.*

Kwa jumla kazi za watangulizi wote zilizotajwa zimetoa mchango mkubwa katika kuupeleka mbele utafiti huu kwa vile zimeeleza mambo ya msingi yanayohusiana na utafiti; ambayo pasi na shaka yejote yamemsaidia sana mtarafitii kuongeza maarifa hususani katika suala la mapenzi ambayo ndio msingi mkuu wa utafiti huu.

2.4 Pengo la Maarifa

Mapitio ya kazi tangulizi yanaonesha kuwa dhamira ya mapenzi ni mionganini mwa dhamira ambayo ina nafasi kubwa katika uga wa riwaya ya Kiswahili. *Kamwe si Mbali Tena* ni moja wapo kati ya riwaya ambayo imezungumzia mapenzi. Hata hivyo mapitio ya kazi tangulizi yameonesha kuwa hakuna mtarafitii aliyewahi kushughulikia kazi ya *Kamwe si Mbali Tena* katika kuchunguza dhamira hii ya mapenzi kama dhamira au kipengele pekee kinachojitegemea kimaudhui. Kwa mintarafu hiyo mtarafitii alishawishika kufanya utafiti huu ili kuchunguza dhamira hii ya mapenzi katika riwaya hiyo.

2.5 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni neno lenye mawanda mapana katika kazi mbalimbali za utafiti na uhakiki. Wataalamu kadhaa wamejadili kwa kina maana ya nadharia kwa mujibu wa mitazamo yao. Mionganini mwa waliojadili ni pamoja na: Buliba na wenzake (2014), ambao wanafafanua nadharia kuwa ni njia ya kutazama kitu katika taaluma yoyote. Wanaendelea kusema kuwa nadharia ni dira inayompa mtarafitii mwongozo wa kutafakari masuala maalum katika utafutaji wa maarifa kwenye taaluma. Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili; nazo ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji (Upokezi) na nadharia ya Simiotiki.

2.5.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji /Upokezi ni mionganini mwa nadharia zinazotumika katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Nadharia hii ni nadharia inayomlenga msomaji moja kwa moja na kumpa uhuru wa kutafsiri matini kutokana na muono, uwezo wa kitaaluma na uzoefu wake. Nadharia hii iliasisiwa mwishoni mwa miaka 1960 huko Ujerumani. Wamitila (2002) anawataja mionganini mwa waasisi wa nadharia hii kuwa ni pamoja na: Wolfgang Iser, Stanley Fish, James Tompkin na Haus Robert Jauss. Kuzuka kwa nadharia hii ni matokeo ya msuguano wa kifikra uliodumu kwa muda mrefu kuhusu dhana ya ujenzi wa maana ya matini ya kifasihi kuhusu kuwa na maana moja tu au kuwa na maana zaidi ya moja.

Waumini wa nadharia hii wanaamini kwamba kazi ya fasihi haina umbo wala sura moja iliyo maalum. Hii inatokana na hoja inayoichukulia kazi ya fasihi kama umbo lisilotimia daima. Kutokuwepo kwa ukamilifu katika matini za fashi ndio inayoifanya isiweze kuchanganuliwa kwa kutumia kanuni maaalumu za kimaabara kama ifanywavyo kwa dhana mbalimbali za sayansi asilia. Kwa vile fasihi siyo kipengele cha sayansi asilia ni sanaa ya maneno, ndipo wazo muhimu la kumuhitaji sana mtumiaji (hadhira) litokeapo ili akamilishe umbo la kazi ya fasihi. Hivyo wao humuweka msomaji katikati ya fanani na maana ya matini ili akamilishe maana. Hali hii inatokana na imani kuwa msomaji huwa na mawazo ya awali kuhusu matini anayoisoma. Mawazo hayo hutokana na uzoefu/tajriba ya kimaisha. Aidha wanaamini kuwa usomaji ni tendo linalofanyika na kutekelezwa kwa namna na wakati maalum na kwa hivyo, usomaji wa kazi ya fasihi huathiri maana ya matini hiyo. Licha ya hayo wananaadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya kifasihi inakuwa na

ishara na taswira mbalimbali. Kutokana na ishara na taswira hizo ndio maana matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja kwa mujibu wa upokezi au mwitiko wa msomaji wa kazi hiyo (Wamitila, 2002; Mushegenzi 2003; Wafula na Njogu, 2007).

Iser (1974) na Fish (1980), wamenukuliwa na Wamitila (2002) wakidai kuwa kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hulazimika kuyaziba kutokana na kutunga matini mpya ambazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa. Kinoti (2012), akimnukuu Adena Rosmarin katika Murfin (1999), naye anaeleza kuwa kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji holela. Anaendelea kusema kuwa nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi. Kwa hivyo msingi mkuu wa nadharia hii unajikita katika namna mbalimbali za ujengaji wa maana kutoka katika matini ya kifasihi kupitia hatua tatu hizo ambazo ni usomaji, msomaji na upokezi.

2.5.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kwamba nadharia ya Upokezi huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza. Maswali hayo ni kama yafuatayo:-

- i. Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?
- ii. Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia?

- iii. Kuna wasomaji ambao husoma na kutafsiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine?
- iv. Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Maswali haya yanarejelea hatua za kiupokezi zinazohitaji kufuatwa na kuzingatiwa na msomaji ili kupata maana ya kazi ya fasihi. Hatua hizo ni pamoja na:

- i. Kurejelea maana ya kazi inayosomwa kwa tafsiri ili kuthibitisha kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.
- ii. Kubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohuiana moja kwa maoja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.
- iii. Kutumia ithibati bayana kudhihirisha kuwa vijalizo (maoni ya msomaji yanayotokana na maarifa mbalimbali ya kimaisha) vinafungamana na vipengele muhimu vya kazi husika.

Pamoja na hayo Salim (2015) anasema kuwa, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inatajwa kuwa na mapungufu yake kutoptaka na kwamba kazi ya fasihi hupata maana yake pale tu itakapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa minajili hiyo basi, hali hii inaweza kupelekea msomaji wa kazi ya kifasihi kuipa maana finyu kazi husika kinyume na mwandishi alivyodhamiria. Hata hivyo licha ya mapungufu hayo, mtarufi anaamini kuwa nadharia hii ya Mwitiko wa Msomaji ni faafu katika uchambuzi wa utarufi huu kwa kuwa msingi wake mkuu unaangazia katika namna mbalimbali za ujengaji wa maana katika matini ya kazi ya fasihi. Kwa kuzingatia hilo, mtarufi ameamea kuitumia nadharia hiyo ili kuweza kufanikisha vyema lengo mahsus la kwanza sambamba na kujibu swali la kwanza la utarufi huu unaolenga

kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed akiwa na imani ya kukidhi mahitaji ya utafiti.

2.5.2 Nadharia ya Simiotiki

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) kietimolojia neno Simiotiki ni neno la lugha ya Kiyunani lenye maana ya ishara, ambalo hutumiwa kuelezea mielekeo ya makundi fulani ya kihakiki. Mielekeo na makundi hayo yamezuka na mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi ambazo huangazia zaidi matumizi ya ishara. Ishara ama alama zinazojitokeza katika kazi ya fasihi huundwa na mwandishi/mtunzi kwa kurejelea muktadha wa jamii husika katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni. Chandler (1992) anaeleza, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa ishara/alama tofauti ambazo huzitumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Watunzi na hadhira hutumia ubunifu wao kutafsiri ishara/alama wanazokutana nazo katika kazi za kifasihi. Kupitia ishara hizo wasomaji wa kazi za fasihi hutengeneza maana mbalimbali ambazo zinaweza kuwa katika mtindo wa picha, maneno, harufu /sauti, matendo na mtenda.

Vilevile wana nadharia hii wanaamini kuwa watu wa jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja huweza kuwasiliana kwa njia ya fiche, hivyo inapaswa kila usemi katika kazi ya fasihi kuangaliwa kwa jicho la ndani ili kupata maana iliyokusudiwa kwani ishara zote katika kazi ya fasihi huwa na maana ambayo hubeba ujumbe muhimu. Cobley (2001) anasema Simiotiki ni taaluma ya mfumo wa matumizi ya alama au ishara kwa nia ya kuwasiliana kati ya wanajamii na kuelewana baina yao. Nadharia ya Simiotiki imezuka katika miaka ya 1970. Mwasisi wake akiwa ni mwanaisimu miundo wa Ki-swiswi Ferdinand de Saussure na mwanafalsafa

wa Kimarekani Charles Pierce. Pierce anaamini kuwa kila ishara ina misingi yake mahasusi inayotegemezwa ili kufasiriwa kwake kuwe rahisi kwa msomaji. Misingi ambayo inazuwa aina tatu za ishara ambazo ni kielekezi, ishara tanakali na taashira.

2.5.2.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki

Nadharia hii inakamilika kwa kurejelea mawazo ya Barthes (1994) ambae ameainisha misimbo au mihimili mitano ya nadharia ya Simiotiki. Misimbo hii hutumika katika kuhakiki kazi za kifasihi na imeacha athari kubwa katika ishara na uashiriaji katika kazi hizo:

- i. **Msimbo wa Kiishara:** Huu ni msimbo muhimu wa usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi unaohusishwa na namna wasomaji wanavyovumbua maana za kiishara zinazotumika katika kazi za kifasihi.
- ii. **Msimbo wa Kimatukio:** Huu unahuusu matukio yanayosawiriwa katika hadithi jinsi yanavyofuatana, kuungana na kushonana na namna msomaji anavyoilewa na kuunda msuko wa kazi nzima kutokana na kuathiriana kwa matukio hayo katika kazi husika.
- iii. **Msimbo wa Kiurejelezi:** Msimbo huu hujengwa na viashiria vyenye kurejelea mambo mbalimbali yanayoeleweka na wasomaji yenye uhusiano na utamaduni wa jamii husika.
- iv. **Msimbo wa Kihementiki:** Huu ni msimbo ambao unahuusu tataruki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wakusimulia na kutamba hadithi. Msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi ya kifasihi.

v. **Msimbo wa Kiseme:** Neno “seme” huelezea elementi nasibishi za kisemantiki, elementi ambazo hutuwezesha kupata picha. Msimbo huu unahusiana na namna msomaji atakavyoishia kupata picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

Nadharia hii imetumika kama dira ya kumuongoza mtafiti katika kufanikisha lengo la pili la utafiti linalowiana na swali la pili la utafiti huu: Kwa muhtasari lengo na swali hilo linalenga kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Nadharia hii imetumika sambamba na misimbo yake kama vile msimbo wa kiishara, kimatukio, kiurejelezi na kihementiki.

2.6 Hitimisho

Sura hii ya pili kwa ujumla wake imewasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Awali imeanza na ufanuzi wa dhana/istilahi muhimu zenye uhusiano na utafiti huu, mbinu za kisanaa, chimbuko la riwaya, utalii wa kazi tangulizi kuhusu dhamira, utalii wa kazi tangulizi kuhusu riwaya za mwandishi, pengo la maarifa pamoja na mkabala wa kinadharia ambao umetaja nadharia ambazo zimetumika katika utafiti huu ambapo mtafiti amechagua nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Simiotiki kuititia misimbo iliyoinishwa. Sura inayofuata ni Mbinu za Utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mbinu mbalimbali ambazo zilitumika katika kufanikisha utafiti huu. Vipengele ambavyo vimefafanuliwa katika sura hii ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usamplishaji, mbinu za kukusanya data za utafiti, aina za data za utafiti, mbinu za uchambuzi wa data, mkabala uliotumika katika kuchambua data za utafiti, zana au vifaa vyta utafiti, pamoja na hitimisho.

3.2 Eneo la Utafiti

Hii ni sehemu mojawapo miongoni mwa kipengele cha mbinu za utafiti. Eneo la utafiti huainisha sehemu au mahali ambapo taarifa zinazohusiana na utafiti zitakusanywa. Enon (1998) anaeleza kuwa, eneo la utafiti kijiografia ni pahala ambapo mtarifi huenda au hutumia katika kukusanya data za utafiti wake. Utafiti huu ni wa maktabani na ulifanyika katika eneo la maktaba teule: Maktaba kuu Zanzibar, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika matawi yake yaliyoko kisiwani Pemba. Mbali na hayo, mtarifi aliperuzi kwa kina katika mitandao/wavupepe au wavuti/tovuti kwa lengo la kujipatia taarifa/data za kutosha kuweza kukamilisha utafiti wake, wenye mada isemayo *Kuchunguza dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed.*

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu ni mpango mahususi ambao hutumiwa na mtarifi katika mchakato mzima wa kukusanya, kuchambua na kuzitumia data ili kuweza kupata taarifa zilizo na

usahihi. Robson (2007) anafasili usanifu wa utafiti kuwa, ni mchoro au ramani inayoonesha picha kamili namna utafiti utakavyofanyika kuanzia ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data, hadi kuandika ripoti ya utafiti. Kothari (2008) anasema usanifu wa utafiti ni ramani inayotoa taswira kamili ya namna utafiti ulivyofanyika tangu katika kukusanya data mpaka kufanya uchambuzi wa data. Utafiti huu unahu uchunguzi kifani (*case study*). Uchunguzi kifani ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti huteuwa eneo maalumu ambalo hulishughulikia kwa kina na kupata data za kutosha kufanikisha malengo ya utafiti. Cresswell (2009) anaisifu mbinu hii na anaeleza kuwa, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ambayo humuwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kutokana na kushughulika na kile kinachohusika. Kwa mintarafu hiyo, riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ndio ambayo imeteuliwa kufanyiwa utafiti wa kuchunguza dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza. Baadhi ya mbinu za kisanaa kama vile wahusika, lugha na mandhari zilitumika ili kuibua dhamira hiyo katika riwaya teule.

3.4 Kundi Lengwa

Ni jumla ya vitu au watu wote ambao mtafiti huwatumia katika utafiti. Bryman (2004) anaeleza kuwa kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhuishwa katika utafiti Williman (2011) anasema kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti. Kutokana na fasili za wataalamu hao, kwa ujumla kundi lengwa ni jumla ya vitu au watu ambao humwezesha mtafiti kupata matokeo ya jumla yanayohusiana na utafiti wake. Kwa mantiki hiyo, kundi lengwa ambalo limehusika na utafiti huu ni riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*

ambayo mtafiti ana imani kuwa ilimwezesha kupata data za kutosha na kumpa matokeo ya utafiti wake kwa usahihi.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

3.5.1 Sampuli ya Utafiti

Sampuli ni wawakilishi ambao huteuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kutoa taarifa ambazo zitawakilisha kundi zima (Robson, 2007). Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa sampuli ya utafiti ni sehemu ya watafitiwa ambao huteuliwa ili kuwa wawakilishi ambao hufanywa kuwa kundi lengwa la utafiti. Kwa ujumla sampuli ni kiwakilishi cha watu au vitu vilivyochanguliwa vitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi kubwa. Kwa mnasaba huo, sampuli ya utafiti haiwezi kupatikana pasi na kufanyika kitendo cha usampulishaji. Riwaya teule moja (1) ya *Kamwe si Mbali Tena* ndio sampuli ya utafiti huu mionganini mwa riwaya zaidi ya kumi (10) za mwandishi Said Ahmed Mohamed. Riwaya ambayo imeweza kumpatia mtafiti wa kazi hii data za kutosha kukamilisha malengo ya utafiti.

3.5.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo itawakilisha watafitiwa wote wanaolengwa katika utafiti unaotarajiwa kufanyika (Cresswell, 2009). Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji lengwa kupata sampuli ya utafiti wake.

Usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ambayo kwa makusudi mtafiti huteua sampuli akiwa anaamini kwamba sampuli hiyo ndio pekee inayoweza kumpatia data anazozihitaji. Cohen na Marrion (2000) wanaeleza kuwa, mbinu ya

usampulishaji lengwa ni nzuri kwa sababu humsaidia mtafiti kupata data za uhakika na kwa urahisi. Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* iliweza kukidhi haja ya mahitaji ya kukamilisha malengo mahasusi na kuweza kujibu maswali ya utafiti husika.

3.6 Aina za Data

Katika utafiti huu data zilizokusanywa ni za aina mbili: Data za Awali (Msingi) na data za Upili (Fuatizi).

3.6.1 Data za Awali

Data za Awali ni zile data ambazo zimekusanya kwa mara ya kwanza na mtafiti mwenyewe katika vyanzo husika. Furlong (2000) anafafanua data za msingi ni zile ambazo zinakusanya kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanya na mtafiti mwengine yejote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza. Virtania (2011) anasema data za msingi ni data ambazo zinakusanya na mtafiti kwa kutumia mbinu kama vile hojaji, mahojiano, vikundi lengwa, uchunguzi au mbinu nyengine. Mtafiti katika kukusanya data zake za awali ametumia mbinu ya usomaji makini matini kupitia riwaya husika iliyoteuliwa ya *Kamwe si Mbali Tena*.

3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni taarifa ambazo zimekwisha kusanya na watafiti wengine kwa lengo la kutimiza malengo ya tafiti zao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbalimbali (Creswell, 2009). Data hizi hupatikana katika vyanzo mbalimbali kama vile tasnifu, makala, magazeti, majarida, wavuti na vyanzo nyenginevyo. Mtafiti

aliperuzi/alisoma kwa kina katika vyanzo husika ambavyo vimetajwa hapo juu kwa lengo la kupata taarifa sahihi zinazohusiana na utafiti wake katika kukazia maarifa taarifa/data za awali ili kufanikisha lengo la utafiti husika.

3.7 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data ni msingi katika kufanya utafiti wa kitaaluma. Kutohana na mbinu hizo ndio utafiti huweza kufanywa kisayansi. Zoezi la ukusanyaji wa data ni muhimu sana ili kuweza kupata taarifa zinazohitajika kulingana na mada ya utafiti husika. Zaidi ya hayo, hatua za uwasilishaji na uchambuzi wa data haziwezi kufanyika kabla ya hatua ya ukusanyaji wa data.

Williman (2005) anaeleza kuwa ziko mbinu za aina mbili ambazo mtafiti anaweza kuzitumia kwa kukusanya data. Mbinu ya aina ya kwanza ni mbinu ya kukusanya data uwandani na aina ya pili ni ile za kukusanya data makkabani. Kwa kuwa utafiti huu ni wa makkabani, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini na mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Mbinu hizi zimemwezesha mtafiti kupata taarifa sahihi za utafiti huu kama zilivyowasilishwa na kuchambuliwa katika sura inayofuata sura ya nne.

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kusoma matini aliyoichagua kwa utulivu na umakini wa hali ya juu ili kupata data za utafiti wake. Newman (2006) anasema kuwa, usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi au za awali kwa kusoma matini zinazohusiana na mada husika kwa umakini na kuzifanyia uchambuzi ili ziweze kujibu maswali ya utafiti. Kwa hivyo mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini kwa ajili ya kukusanya data za awali/msingi kutoka katika riwaya

teule ya *Kamwe si Mbali Tena*. Mtafiti alianda daftari maalumu la kuandika data /taarifa zote muhimu zilizohitajika kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti kulingana na mada ya utafiti.

3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka

Mbinu ya upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambapo data hukusanywa kupitia katika maandiko mbalimbali ya kazi zilizokwishafanywa na watu wengine waliotangulia yanayohusiana na utafiti husika (data za upili). Upitiaji wa nyaraka huhusu kazi kama vile makala za kitaaluma, tafiti tangulizi, magazeti na tahakiki mbalimbali ambazo humsaidia mtafiti kutilia nguvu hoja katika uchambuzi wa data za awali/msingi. Katika utafiti huu, mbinu ya upitiaji wa nyaraka imetumika vyema kwa mnasaba wa mada ya utafiti: *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*.

3.8 Uchambuzi wa Data za Utafiti

Uchambuzi wa data ni hatua muhimu sana katika utafiti ili kuhakikisha kwamba malengo yanafikiwa kwa usahihi kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti unaohusika. Kothari (2008) anasema uchambuzi wa data za utafiti ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Kwa hivyo, data zilizokusanywa wakati wa utafiti ndio ambazo hufanyiwa uchambuzi wa kina kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti na kukamilisha malengo yaliyokusudiwa. Kitendo hiki ndio ambacho humwezesha mtafiti kutathmini nadharia za utafiti husika. Mtafiti alitumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika uchambuzi wa data.

3.8.1 Mkabala wa Kimaelezo

Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti hufanya uchambuzi wa data zake kwa kuzitolea maelezo ya kina. Kwa kawaida mbinu hii ya kimaelezo hutumika katika uchambuzi wa data unaohusiana na taaluma ya fasihi. Katika utafiti huu mtafiti alijikita zaidi katika mkabala wa kimaelezo ambapo data zilizowasilishwa zilichambuliwa na kutolewa maelezo ya kina kwa namna ambayo ilimwezesha mtafiti kutimiza lengo kuu, malengo mahsus ya utafiti huu na kujibu maswali ya utafiti yaliokusudiwa. Mbinu ya mkabala wa kimaelezo ndio muhimili wa uchambuzi wa data za utafiti huu.

3.9 Zana za Utafiti

Zana ama vifaa vya utafiti ni muhimu katika kufanikisha zoezi zima la utafiti. Vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti husika. (Kothari 2004) anaeleza maana ya vifaa vya utafiti kuwa ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wake wa data. Hivyo mtafiti alitumia vifaa mbalimbali katika kufanikisha utafiti huu. Miongoni mwa zana/vifaa vya msingi ambavyo vilitumika ni pamoja na Kompyuta, kalamu na karatasi.

3.9.1 Kompyuta

BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusanifu taarifa zinazoingizwa ndani yake. Kwa asilimia kubwa mtafiti alitumia zana hii katika kuandika na kuweka kumbukumbu zote zinazohusiana na utafiti husika, sambamba na kuperuzi machapisho kupitia tovuti mbalimbali.

3.9.2 Kalamu na Karatasi

Hizi ni zana ambazo hutumika sambamba katika suala zima la uandishi, Zana hizi zimemsaidia mtafiti kwa kiasi kikubwa katika uandishi. Kupitia mbinu ya usomaji makini matini maktabani, mtafiti aliandika na kuhifadhi taarifa/data mbalimbali zenyehusiano na mada ya utafiti: *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed.*

3.10 Hitimisho

Sura hii kwa jumla imeeleza kwa kina dhana nzima ya mbinu za utafiti. Sambamba na vipengele vyote muhimu vinavyohusika ambavyo ni pamoja na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, data za utafiti, ukusanyaji wa data za utafiti, aina za data za utafiti, uchambuzi wa data za utafiti, mkabala wa kimaelezo, zana /vifaa vilivyotumika katika utafiti na hitimisho. Sura inayofuata ni Uwasilishaji na Uchambuzi wa data za utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data ambazo zimekusanywa kutoka maktabani ili kutimiza lengo la utafiti huu. Uwasilishaji na uchambuzi wa mjadala umefanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti ambapo lengo la kwanza limelenga kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*, na lengo la pili ni kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Vile vile malengo mahususi ya utafiti huu yaliongozwa na maswali yafuatayo: Ni kwa namna gani dhamira ya mapenzi imejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? na Ni mbinu ziipi za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena*? Uchambuzi wa data za utafiti uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kwa lengo la kwanza na nadharia ya Simiotiki kwa lemgo la pili.

4.2 Muhtasari wa Riwaya Teule ya *Kamwe si Mbali Tena*

Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ni mionganini mwa riwaya za mwandishi mashuhuri Prof. Said Ahmed Mohamed ambayo imeandikwa katika miaka ya hivi karibuni (2014). *Kamwe si Mbali Tena* ni jina la riwaya ambalo limesadifu yale yaliyomo kutokana na kuakisi pamoja na kusawiri uhalisia wa maisha katika nchi ya Visiwa vya Viungo (Zanzibar). Masuala mbalimbali yanyohusiana na nyanja zote za maisha kama vile kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni yamejadiliwa kwa kina

kutokana na mwandishi kuwa na tajriba /uzoefu wa mambo mbalimbali yatokeayo katika jamii.

Kwa muhtasari riwaya hii inaelezea hali ya maisha ya familia ya Bi Chani, mama wa familia ya watoto tisa, nane aliowazaa mwenyewe amba ni Abuu, Salila, Yasir, Jokha, Sele (Msurupwete), Zaharani, Samira na Tambo. Na mtoto wa tisa ni mwanawe wa kulea anayeitwa Mwavile ambaye alijitolea kwa moyo wake wote kumtunza na kumlea mama yao (Bi Chani) kwa mapenzi makubwa na huruma baada ya watoto wake wote kuondoka nyumbani. Awali familia ya Bi Chani na mumewe Bwana Mansour ilikuwa ni familia iliyoishi katika maisha yaliyojaa furaha tele, neema, utononofu na mapenzi ya hali ya juu yaliyoambatana na utajiri mkubwa sana kama si ukwasi hasa. Maisha haya yaliendelea hadi pale baba wa familia hii (Bwana Mansour) alipouwawa kikatili na kisha utajiri wao wote likiwemo shamba kubwa la (Bi Chani) kuchukuliwa na wale walioshika hatamu na hatimae kubakishiwa kiasi cha pesa kidogo tu za kujikimu. Hali hii ndio ambayo ilipelekea familia kusambaratika kutokana na watoto wake kuhajiri nyumbani kwao, wengine kwa ndoa na wengine kuselemea nchi za Magharibi kwa ajili ya kutafuta maisha bora. Huko baadhi yao walifanikiwa kusoma akiwemo Zahran, Tambo, na Samira. Zahran alisomea biashara na uhasibu, Tambo alisomea sheria, Samira naye alisoma na kushika Uprofesa wa somo la *Media* na *Information Technology* katika Chuo Kikuu cha Sydney. Baada ya muda kupita watoto hao walirudi nyumbani Visiwa vya Viungo wengine wakiwa na mafanikio makubwa. Kwanza alianza kurudi Tambo ambaye aliamua kuja kushirikiana na dada yake wa kulelewa pamoja (Mwavile) kumlea mama yao. Wengine waliofuatia ni Abuu na Yasir wao walirudi wakiwa na

hali duni kimaisha (hohe hahe) Jokha naye alirudi baada ya kupata misukosuko katika ndoa yake. Sele, Zaharani na Samira nao walirejea wakiwa na mitazamo mipyä, hivyo waliamua kushirikiana na wananchi wenzao wenye mapenzi na nchi na kuanzisha vuguvugu la fikra za mabadiliko za kubadilisha mwenendo wa uongozi uliojikita katika misingi ya dhulma na uonevu uliodumu kwa miaka mingu. Harakati hizi hatimae zilizaa matunda pale mahakama ilipoamuru kwamba mashamba na ardhi zote ilizochukuliwa na waheshimiwa na serikali yarejeshwe kwa wananchi wanaomiliki ardhi hizo. Baada ya matokeo hayo watu waliamini kwamba huo ulikuwa mwanzo wa ushindi wa vita vyao vyta kupigania haki kwa wote.

4.3 Usuli wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed

Said Ahmed.Mohamed alizaliwa mnamo mwaka wa 1947 kisiwani Unguja - Zanzibar. Alisoma shule ya msingi ya Darajani mjini Zanzibar. Alijiunga na shule ya upili ya Gulioni ambayo kitambo ilijulikana kwa jina la KG VI. Baadae alijiunga na Chuo cha Ualimu Nkurumah mwaka 1966. Alifaulu na kuanza kufundisha kama mwalimu wa shule ya msingi katika shule ya Kizimbani na baadae shule ya sekondari ya Utaani. Huko alifundisha masomo ya Biolojia, Kemia, Hesabati na Kiswahili. Wakati huo pia alikuwa akiandika hadithi fupi katika kituo cha BBC na DW. Mohamed alihitmu shahada ya Kwanza (B.A) katika Isimu na Fasihi mwaka 1976 katika Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam (UDSM). Baada ya hapo alirejea Zanzibar na kuwa mwalimu mkuu wa shule ya msingi na upili ya Hamamni kwa muda wa miaka mitano. Alihitimu shahada ya Uzamili (M.A) katika Chuo Kikuu cha Dar - es Salaam ambapo alisomea Isimu Tekelezi. Baadae alijiunga na Chuo Kikuu cha Leipzig nchini Ujerumani ambako alihitimu shahada ya Uzamivu

(PhD) mwaka 1985. Baadae alirudi nyumbani Zanzibar ambapo aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa pili katika Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI). Kutoka hapo alihamia nchini Kenya kufundisha Kiswahili katika Kitivo cha Elimu katika Chuo Kikuu cha Moi mwaka 1987 akiwa Mwenyekiti wa kwanza wa Idara ya Kiswahili nchini humo. Mwaka 1990 alijiunga na Chuo Kikuu cha Masomo ya Kigeni kule Osaka nchini Japani ambapo alipata Uprofesa. Mnamo mwaka 1997 alijiunga na Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani hadi alipostaa fu na kurudi Zanzibar. Prof. Mohamed akiwa Zanzibar aliendelea kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa ngazi ya Uzamili na Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA).

Katika tasnia ya utunzi Mohamed alianza kutunga mashairi na hadithi fupi tangu akiwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Kwa mujibu wa King'ei (1997) Mohamed amefanikiwa katika utunzi wa tanzu tofauti kama vile Ushairi, Riwaya na Tamthilia jambo ambalo ni nadra sana kutokea katika taaluma ya fasihi kwa sababu wasanii wengi hufungika katika utanze mmoja peke yake. Baadhi ya kazi zake za ushairi ni diwani ya *Sikate tama* (1980) *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002). Kazi zake za riwaya ni *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001) *Dunia Yao* (2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012), *Mkamandume* (2013) *Kamwe si Mbali Tena* (2014) na *Wenye Meno* (2018). Pia ametunga tamthilia kama vile *Pungwa* (1988) *Amezidi* (1995) *Kivuli Kinaishi* (1990), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), *Janga la Werevu* (2011), *Posa za Bikisiwa* (2008) akishirikiana na Kitula King'ei. Na katika

uga wa Hadithi fupi, Mohamed ametoa mchango wake katika mikusanyiko ya hadithi mbalimbali kama vile *Sadiki Ukipenda* na *Hadithi nyengine* (2002). *Arusi ya Buldoza* na *Hadithi nyengine* (2007) Aidha kazi zake hazikukomea hapo ameandika *Kunga za Nadharia ya Kiswahili, Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi* (1995). Ametunga pia *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi* (1990).

4.4 Kubainisha Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*

Mada ya utafiti huu, *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*. Lengo mahsus la kwanza la utafiti lilihusu kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Lengo mahsus hilo limekwenda sambamba na swalii la kwanza la utafiti lisemalo: Ni kwa namna gani dhamira ya mapenzi imejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? Kwa kuzingatia lengo mahsus la kwanza na swalii la kwanza la utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa katika riwaya hii dhamira ya mapenzi imeweza kujitokeza katika namna tofauti. Dhamira hizo zimebainishwa na kuorodheshwa kwa muhutasari katika jedwali namba moja kama inavyoonekana hapo chini na hatimae ilifuutiliwa na uchambuzi uliorejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji /Upokezi.

Jadweli 01: Muhtasari wa Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*

Na.	Dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena	Maelezo
1	Dhamira ya Mapenzi ya Nchi / Uzalendo	✓
2	Dhamira ya Mapenzi ya Familia	✓
3	Dhamira ya Mapenzi ya Ndoa	✓
(i)	Dhamira ya Mapenzi ya Dhati	✓
(ii)	Dhamira ya Mapenzi ya Uongo	✓
4	Dhamira ya Mapenzi ya Udugu	✓
5	Dhamira ya Mapenzi ya Urafiki	✓
6	Dhamira ya Mapenzi ya Dini / Imani	✓
7	Dhamira ya Mapenzi ya Mazingira	✓
8	Dhamira ya Mapenzi ya Kazi	✓
9	Dhamira ya Mapenzi ya Pesa / Mali	✓
10	Dhamira ya Mapenzi ya Elimu	✓
	Jumla	12

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Oktoba 2018

4.4.1 Dhamira ya Mapenzi ya Nchi/Uzalendo

Nchi ni eneo la ardhi lenye utawala na mamlaka yake kamili. (BAKIZA, 2010).

Uzalendo ni hali ya mtu mwenyewe kwa hiari yake pasi na kulazimishwa huamua kujitolea kwa hali na mali kwa ajili ya kusaidia nchi yake katika masuala mbalimbali kama vile kisiasa, kiuchumi na kijamii. Dhamira ya mapenzi ya mtu na

nchi yake imeweza kujitokeza katika kurasa mbalimbali za riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* kwa mfano katika nukuu ifuatayo:

“Tambo alitaka sana abaki nyumbani na kushirikiana na wananchi wenzake kuisafisha nchi yake kwanza kabla hawajajiunga kuisafisha dunia yao. Hakutaka kulazimishwa aende ugenini. Na kwanini Tambo akimbiye?” (uk.6).

Data hii imetumika kuonesha dhamira ya mapenzi ya dhati ya mtu kupenda nchi yake, yaani mtu kupenda kwao. Tambo hakutaka kuhama kwao, katika nchi yake ya Visiwa vya Viungo pamoja na idhilali ya hali ngumu ya maisha, ukosefu wa haki, dhulma na uonevu uliopindukia ambao ulipelekea kuuliwa kikatili kwa baba yao, bado hakuwa tayari kuondoka nchini alikataa katakata. Licha ya kushawishiwa sana na dada yake Mwavile kuwa aondoke nchini kama ambavyo wenzake wote waliamua kuondoka na kuelekea Ulaya kwa ajili ya kwenda kutafuta maisha aliona ni bora abaki tu nyumbani. Mwandishi hapa anaonesha dhahiri mapenzi ya mtu na nchi yake, mtu kupenda kwao katika hali na mazingira yejote ile iwayo hata kama kuna shida na dhiki kiasi gani anapaswa kukuthamini na kukupenda kwa raha au karaha.

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo inampa uhuru msomaji wa kazi ya fasihi kutafsiri kazi ya fasihi kwa mujibu wa muono wake, mtafiti amebaini kuwa katika jamii, wako wazalendo wenye mapenzi na nchi. Mfano hata katika riwaya ya *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert, tunaona jinsi wajumbe sita Burhani, Auni, Kabuli na wenzao walivyojitoa muhanga kwenda katika nchi ngeni kutalii mambo mbalimbali ya maendeleo, kwa manufaa ya nchi na wananchi wake walijitolea kufa kupona katika safari zao na hatimaye walirudi kwao na mafanikio makubwa. Pamoja na juhudhi hizo watawala hao hawakuwa na mapenzi ya dhati

kwasababu matokeo yake walisekwa gerezani hadi pale kijana mwengine mwenye mapenzi na nchi (Karama) alipojitokeza na kuanzisha elimu ya uanasheria kwa lengo la kuikomboa nchi yake ikiwa ni pamoja na kuwa sababu kubwa ya kuachiwa huru wajumbe hao sita (6) kutoka gerezani. Huu ndio huitwa uzalendo na ndio takrima kubwa kwa mtu mwenye mapenzi na nchi yake, kwasababu kila mtu ni kama mti imara unaotoa mizizi katika nchi yake iwe toopeni au jangwani hapaswi kukimbia.

4.4.2 Dhamira ya Mapenzi ya Familia

Familia ni jumla ya baba, mama na watoto waliozaliwa na wazazi hao. Mapenzi ya familia ni mapenzi ambayo yanajikita zaidi kwa wazazi kupenda watoto wao na vile vile watoto kupenda wazazi wao. Robert (1958) anasema, mapenzi kwa mwanadamu ni kama mshipa na damu au mti na mzizi. Kwa hivyo wazazi katika jamii wana wajibu wa kuwapenda watoto wao, kuwatunza na kuwapa malezi bora yatakayowawezesha kuinukia kuwa watoto wema wenyewe maadili mazuri katika jamii na taifa kwa ujumla. Sambamba na hilo watoto nao wana wajibu wa kuwapenda wazazi wao, kuwatii, kuwaheshimu na kuwahurumia hasa wakati wanapokuwa katika hali ya uzee. Mwandishi ameonesha mapenzi ya familia kupidia familia mbalimbali kama vile familia ya Bwana Toba, familia ya Bwana Mansour na familia ya Bwana Hassani. Familia zote hizi ni mfano wa familia ambazo ziliishi kwa mapenzi makubwa, data ifuatayo inaonesha mfano wa mapenzi ya familia kwa mzazi na mtoto wake.

“Mapenzi ya Mansour kwa wazazi wake ni ya kikanda cha halua.Yaani kwa kawaida mtu haonji halua mara moja bali mara milioni moja. Kila mtu akichokoa halua kwenye kikanda na kutia kinywani, hutamani kuchokoa na kuila tena na tena wazazi wake wakawa tayari kumpa au kumlisha si halua tu, bali dunia mzima asiyotosheka nayo Mansour. Mapema Mansour alitambua apendwaye akajua haachi kujizuzua. Kwa namna hiyo tokea utoto wake alibadilisha itifaki ya nyumba kwa kufanya mageuzi ya utawala mpya. Yeye ndiye aliyekuwa mtawala mkubwa ndani na nje ya nyumba kubwa hiyo. Alibadilisha mwenendo mzima wa nyumba ile na kila kitu chake” (uk. 113-114).

Katika data hiyo hapo juu mwandishi ameonesha dhamira ya mapenzi ya familia, mapenzi ya mzazi kumpenda mwanawe. Mansour alipendwa sana na baba na mama yake, na huu ni mfano wa mapenzi katika familia nyingi za Kiafrika. Watoto katika familia zao hupewa mapenzi katika malezi na makuzi yao mpaka pale na wao wanapokuwa na familia zao, yaani wanapooa au kuolewa. Bado hapo si mwisho wa safari ya mapenzi katika familia, hali huendelea hadi kwa vizazi vijavyo (vijukuu, vitukuu, vilembwe na vinyinginya). Mapenzi yanahusisha mambo mengi kama kuashiria, kuongea, kuchochea na kudumisha upendo wa dhati baina ya pande mbili kama vile mke na mume, mzazi na mtoto, kiongozi na raia, mja na Mola wake na nyinginezo (Rajab, 2016). Mansour tangu akiwa mtoto mdogo alipendwa sana na wazazi wake, mapenzi ambayo hayakuwa na kifani, mapenzi yaliyopindukia na kuvuka mipaka. Mapenzi ambayo mwandishi anayaita kuwa ni ya *Kikanda cha Halua*. Mapenzi haya yalimfanya adeke kupita kiasi na kufanya vituko mbalimbali na mambo ya ajabu ajabu ili kuwapima wazazi wake ambao kwao mtoto huyu hakuwa na baya.

Kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amegundua kuwa katika familia zetu mapenzi ya mzazi kwa mtoto wake ni kitu cha maumbile. Ingawa katika mazingira yasiyo ya kawaida wapo baadhi ya wazazi wenyewe roho ngumu wanaofikia hatua ya kuwauwa au kuwatupa watoto wao, lakini kiuhalisia hakuna mzazi asiyempenda mtoto wake. Bwana Toba na mke wake Bi Badria wanajitosa katika kumpenda mtoto wao kiasi cha kutomkataza lolote lile hata baya kwa kuhofia mtoto wao asikasirike. Sambamba na mapenzi hayo ya mzazi kwa mtoto, upande wa pili wa shilingi ni mapenzi ya mtoto kwa mzazi wake nayo pia yameonekana kupitia data ifuatayo:

“Asubuhi mpya na siku mpya. Kulikuwa na ishara kwamba Bi Chani alikuwa pia mpya siku hiyo. Kila siku mpya ilikuwa na utata kwenye uso wa Bi Chani, Nae Tambo aliweza kumtabiri Bi Chani mara tu alipomwona katika uchangamfu au simanzi zake. Kwa vyovyote vile alitaka ashikane na mamake hadi kifo kitakapowatenganisha. Kamwe asingweza kumtupa kama walivyomtupa watoto wake wengine walioelemea Ughaibuni na kubaki huko mpaka sasa” (uk.36).

Data hii imeonesha mapenzi ya dhati ya mtoto kwa mzazi wake. Kama anavyoonekana Tambo ni kigezo cha kutosha katika mustkbali wa watoto wanaowapenda wazazi wao katika jamii zetu. Tambo alimpenda sana mama yake na alitamani kubaki naye maishani hadi pale kifo kitakapowatenganisha. Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa msomaji kupitia nukuu iliotangulia hapo juu, mtafiti amebaini dhamira ya mapenzi ya familia mtoto kumpenda mzazi wake ni jambo linalostahiki kupewa nafasi ya mwanzo katika jamii kwa sababu wao wazazi ndio ngazi tuliyoshukia kuja duniani. Tambo hakutaka kumuacha mama yake katika hali ambayo hajiwezi mguu wala mkono. Hakuchoka kumbeba katika kigari chake cha ulemavu cha maringi matatu na kumpeka pwani kila siku, kitu ambacho alikipenda

ndani ya nafsi yake. . Hii ni dalili tosha ya mapenzi aliyokuwa nayo kwa sababu katika mazingira halisi tunashuhudia vijana wengi zama hizi wakikumbwa na wimbi la kuacha familia zao na kwenda sehemu wanazodhani kuna maisha yaliyojaa neema, ukamilifu, utulivu na anasa mbalimbali hasa Ulaya ya Magharibi, USA, Canada, Japani, Australia na hata China, huku nyuma wakiziacha familia zao (wazazi) wakiwa katika mazingira magumu. Hakuna anayesubiri amvishe nguo mzazi wake anapokuwa mahututi kitandani. Ni wale wenye moyo wa mapenzi ya dhati na wanaotambua wajibu wa mtoto kwa mzazi mfano wa Tambo ndio ambao wanakaa na kusubiri wawahitimishe wazazi wao kwa kuwashika mikono wanapokuwa wagonjwa na kuwastiri wakati watapofikia mwisho wa maisha yao (kufariki).

4.4.3 Dhamira ya Mapenzi ya Ndoa

Ndoa ni mkataba wa kuishi pamoja kati ya mume na mke kwa kufuata utaratibu uliowekwa na jamii au dini husika. Kwa mfano hapa Tanzania mume na mke watatambulika kuwa wameoana kisheria pale watakapokuwa wamefunga mkataba wa kuishi pamoja mbele ya Mkuu wa Wilaya, mbele ya Sheikh (Kadhi) au mbele ya Padri Kanisani (IPC, 2004). Ndoa ni kitu cha thamani sana kutokana na umuhimu wake katika kujenga na kuiendeleza jamii kwa mambo mbalimbali kama vile, kuihifadhi jamii na masuala ya zinaa, kujenga mapenzi na huruma katika familia, kukilea kizazi katika maadili mema, kukuza uhusiano mwema na udugu katika jamii, kuwafanya watu wawajibike ipasavyo nakadhalika. Kimsingi ndoa hujengwa na mapenzi, huruma na mashirikiano baina ya mke na mume. Suala la mapenzi ya ndoa ni mionganoni mwa mambo yanayozungumzwa sana katika kazi za fasihi, ni nadra

sana kusoma kazi ya fasihi ukaimaliza usikute suala la mapenzi ya ndoa likielezwa hii ni kutokana na umuhimu wake kwa jamii kama tulivyotangulia kueleza. Mtafiti amebaini kuwa, mwandishi wa riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ameonesha dhamira ya mapenzi ya ndoa na anayaangalia mapenzi hayo katika sura mbili tofauti nazo ni mapenzi ya dhati na mapenzi ya uongo.

4.4.3.1 Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni mapenzi ya kweli yanayotoka chini ya mvungu wa moyo wa mtu anayependa kwa anayempenda, mapenzi yasiyokuwa na chembe ya ulaghai wala udanganyifu ndani yake. Mapenzi ya dhati ni kitu chenyeh thamani kubwa kwani huzaa upendo, heshima na uaminifu. Khamis (2007) anasema, mapenzi ya dhati ndio yanayofanya maisha yawe mazuri, na kuwepo kwa maisha mazuri ndiko kunakolifanya penzi liweze kustawi kwani maisha mazuri ni rutba ya mapenzi. Mtafiti anakubaliana sana na mawazo ya Khamis (ameshatajwa) lakini anasisitiza zaidi mapenzi hayo yawe mapenzi ya dhati/ ukweli. Mapenzi ya dhati katika riwyatule yamebainika katika data ifuatayo:

“Bwana Toba alipenda sana wanawake kwa hiyo aliowa wanawake wanne na wengine aliwafanya masuria. Matumizi ya nyumba yake aliyachukua kwa ukamilifu juu ya mgongo wake. Aliwapa wake zake kila kitu walichokitaka aliwapa suria wake chochote walichotamania. Aliwapa ushujaa wake. Aliwapa huruma yake, pia aliwapenda na kuwajali watoto wake” (uk.159).

Data hii imeonesha wazi mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo bwana Toba kwa wake zake wote wanne na wale alioraweka masuria pamoja na watoto wake. Mapenzi ya dhati hujengwa kwa watu kuthaminiana, kuenziana, kushibana, kukinaiana na kusabiliana kwa hali na mali katika mapenzi yao (Rajab, 2016). Mwandishi

ameonesha kwamba Bwana Toba alikuwa na mapenzi ya dhati, na ndio yaliyomsukuma kuwapa wake zake huduma zote na mahitaji ya nyumba kama vile chakula, mavazi, mapambo na kila walichotaka katika matumizi yao, sambamba na hilo aliwapenda sana na kuwahurumia. Lengo la ndoa ni kupata utulivu, kupandikiza mapenzi, huruma na ushirikiano kati ya mume na mke. Allah (SW) katika sura ya thelethini aya ya ishirini na moja amasema kuwa:

Na katika ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mpate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu (Quran, 30:21).

Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, kutokana na uzoefu wa mtafiti imebainika kuwa mapenzi ya dhati yapo na yana nafasi kubwa kwa sababu ndio ambayo huleta kitulizo cha moyo mionganoni mwa wapendanao na kwamba yanayopaswa kuendelezwa katika jamii. Mapenzi ya dhati yalioambatana na huruma ndio muhimili ambao hupelekea kupata utulivu na amani baina ya wanandoa, familia, jamii na taifa ili kuleta umoja na mshikamano. Pale panapokuwa na mapenzi ya dhati majonzi na fadhaa hukosa nafasi na wahusika huishi maisha ya raha mustarehe (Hassan, 2016). Mapenzi ya ndoa huleta heshima na nidhamu katika jamii. Katika jamii nyingi ulimwenguni sheria, imani za kidini na hata mila na desturi za jamii husika huthamini, kuheshimu na kulinda kwa gharama yejote suala hili la ndoa. Kwa hivyo, mume pamoja na mke waliofungamana katika misingi ya ndoa wanapaswa kuishi kwa kupendana kwa dhati, kuthaminiana, kuhurumiana kushirikiana na kusaidiana kwa hali na mali na kama hii haitoshi pia katika kukileta kizazi na kukilea katika misingi ya maadili mema.

4.4.3.2 Mapenzi ya Uongo

Kwa upande mwengine mwandishi amejadili suala la mapenzi ya uongo. Mapenzi ya uongo ni kinyume cha mapenzi ya dhati ni mapenzi ya ulaghai au udanganyifu. Mapenzi ya uongo husababisha mizozo na mitafaruku katika jamii. Khatib (2012) anaeleza kuwa mapenzi ya uongo hayana faida ye yeyote isipokuwa mateso makali kwa mhusika au wahusika. Mapenzi ya uongo yamedhihirishwa katika data ifuatayo:

“Kumezidi nini Jokha? Kuna nini? Mbona unanijia hivyo mwenzangu?. Mwavile alisema hivyo huku akimnyanya Jokha hapo chini mara alipokwisha kumnyanya alishtuka alipomwona Jokha kavimba uso na chini ya macho yake mawili kumepiga weusi wa damu- fuiza. Kanipiga Mzima. Kanipiga vibaya vibaya kanivimbisha uso na kunitoa meno mawili. Kisha kama hilo ndio basi alinisukumizia teke kwenye kitovu cha mimba ya miezi mitatu alishtakia Jokha” (uk. 183-184).

Data hii imeonesha wazi mapenzi ya uongo kwa kile kilichomtokea Jokha baada ya kuingia mikononi mwa mtu ambaye hakuwa na mapenzi. Jokha hakujuua mapenzi ni nini, aliona mapenzi ni vitu vya thamani kama vile nyumba, gari na mali nyengine nyingi ambazo Mzima alizitumia kama chambo cha kumnasa. Mapenzi kama yalivyokwisha kuelezwu hapo awali kuwa, ni ile hali ya watu kuthaminiana, kujaliana, kuhurumiana, kuheshimiana na vitu vyenye kufanana na hayo yaani dalili za kuwa watu hao wana mapenzi na wanapendana.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti kuitia dondo hili amebaini dhamira ya mapenzi ya uongo kwa wanandoa. Na huu ni ukweili usiopingika kuwa katika jamii wapo baadhi ya wanandoa ambao wanaishi katika ndoa wakiwa hawana mapenzi ya dhati kwa wenza wao. Kitendo cha Mzima kumpiga mke wake Jokha kiasi cha kumtoa meno na kumsukumizia teke la tumbo

akiwa na mimba ya miezi mitatu kinaonesha dhahiri kuwa hakuwa na mapenzi ya dhati. Ackerman, (1994) anasema ndoa nyingi zimekuwa zikivunjika mara kwa mara kwa sababu ya kukosekana mapenzi ya dhati kwa walengwa. Kwa mantiki hiyo inaonesha kwamba nyumba ambayo ina ukame wa mapenzi, ina njaa ya mapenzi, ina uhaba wa mapenzi hukosa amani, furaha na utulivu kwa wanandoa. Mbali na wanandoa suala la mapenzi ya uongo pia hujitokeza kwa baadhi ya viongozi wengi ambao baada ya kushika nyadhifa huwa hawana mapenzi ya dhati kwa raia zao, suala ambalo husababisha sintofahamu baina ya watawala na watawaliwa.

4.4.4 Dhamira ya Mapenzi ya Udugu

Udugu ni uhusiano mwema wa watu wanaotokana na uzawa mmoja au kulelewa pamoja kwa ujamaa (TUKI, 2010). Udugu unaweza kuwa wa damu au udugu wa kupanga, na wakati mwengine udugu wa kupanga unaweza kuwa na nguvu zaidi kushinda hata udugu wa damu. Tukiangalia familia nyingi katika jamii mapenzi ya udugu yanaonekana kushamiri kwa kiasi kikubwa hali ambayo hupelekea kukuza uhusiano mwema na udugu katika jamii. Mapenzi ya udugu katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* yamedhihirika kupitia data ifuatayo:

“ Mara Mwavile, dadake mpenzi Tambo alitoka katika tope za bahari na kumwona nduguye amesimama kumngojea atoke huko alikokuwa kuvua pweza. Tambo alikuwa kabogojoka na kipaji chake cha uso kimefunga nyuzi. Mwavile aliekuwa amesawijika na kuhuzunika alimwambia Tambo kwa sauti iliyojaa hisia...“Nenda, Tambo. Nenda. Nenda pamoja na kaka na dada zako, mimi nitabaki hapa kumlea na kumtunza mama yetu. Nitamtunza kwa viganja viwili” (uk .6).

Katika data hii mwandishi ameonesha mapenzi ya hali ya juu kwa ndugu waliolelewa pamoja. Mwavile hakuzaliwa na Bi Chani mama yao akina Tambo

lakini alikuwa na mapenzi makubwa na huruma kwa mlezi wake na ndugu zake kama vile wamezaliwa na mama na baba mmoja. Mbali na hayo mtafiti anaporejelea tarikh au historia katika Uislamu inaonesha kwamba wakati Mtume Muhammad (SAW) alipohama Makka na kuhamia Madina aliunganisha udugu baina ya Ansari (wenyeji wa Madina) na Muhajirina (wageni wa Makka). (IPC, 2004) Inaelezwa kuwa udugu huu ulipelekea pande mbili hizo *Ansari* na *Muhajirina* kuishi kwa mapenzi makubwa na kuhurumiana kuliko udugu wa damu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti kuitia nukuu hiyo amebaini kuwa mapenzi ya udugu yana nafasi kubwa sana karibu sawa na yale ya udugu wa damu. Mwavile huku akiwa na masikitiko na huzuni iliyomjaa moyoni mwake ya kuachana na ndugu yake mpenzi, anamnasihi Tambo kuwa aambatane na kaka na dada zake waondoke nchini Visiwa vya Viungo na kwenda kutafuta maisha nje ya nchi kutokana na hali yao kuwa ngumu baada ya tukio la kuuliwa kwa baba yao (Bwana Mansour). Licha ya hayo anatoa ahadi kuwa yeye atabaki nyumbani kumlea na kumtunza mama yao kwa mapenzi na huruma kama ambavyo yeye alilelewa na mama huyo. Kutokana na kuwa na nafasi mapenzi ya udugu yanaweza kutanuka kutoka katika familia moja, kisha kwenye ukoo, kisha kwenye kabila hadi kufikia kitaifa na kimataifa. Inatosha kusema kuwa sisi sote ni ndugu tunaotokana na familia au kizazi cha *Adam* na *Hawa* hivyo tunapaswa kuishi kwa kupendana, kushirikiana, kusaidiana na kuhurumiana.

4.4.5 Dhamira ya Mapenzi ya Urafiki

Urafiki ni uhusiano mwema au wa kindugu baina ya watu au nchi. Mapenzi ya urafiki ni mapenzi yanayoensiwa sana duniani. Mapenzi ya urafiki hupelekea

uhusiano na maelewano mema mionganini mwa watu na hata baina ya nchi na nchi. Nchi huweza kuwa na urafiki na nchi nyengine katika kufanya shughuli zao mbalimbali za kimaendeleo. Kwa mfano United Arab Emirates (UAE) ni muunganiko wa nchi marafiki ambazo ziliungana pamoja na kuunda taifa moja kubwa mwaka (1971). Nchi hizo ni pamoja na Abu Dhabi, Dubai, Sharjah, Ajman, Umm Al Quwain na Fujairah. Hatimae Ras al Khaimah mwaka 1972 kukamilisha jumla ya nchi saba (7) zilizoungana kuunda taifa hilo ([https://en.m.wikipedia.org>wiki](https://en.m.wikipedia.org/wiki)). Mapenzi ya urafiki katika riwaya teule yamebainika kama mwandishi anavyotuthibitishia katika data ifuatayo:

“Muda ulipita. Chai ilikwishanyiwa. Ikabaki chai ya maneno ambayo Janet alihisi ni tamu zaidi kuliko chai zote alizowahi kuzinywa. Kusema kweli Janet huja kumtembelea Tambo kwa maneno na mizaha yake kwani ishara za mapenzi alikwisha mwonesha Tambo, lakini Tambo hajakubali mpaka sasa kuleweshwa na mwili wala heba ya Janeti. Jambo hilo analielewa vizuri Janeti. Kwa kweli lijemkatisha tamaa. Aliposhindwa na hayo aliona bora apatane nae Tambo kuliko kuachana nae” (uk.22-23).

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaoipa maana kazi ya fasihi kutokana na uzoefu wa msomaji, katika data hii mtafiti amebaini dhamira ya mapenzi ya urafiki usiozingatia masuala ya ngono kinyume na vile ilivyozoleka katika jamii kwamba urafiki baina ya mwanamke na mwanamme unaangalia masuala ya kingono tu. Mapenzi ya urafiki sio lazima yafungamane na mahusiano ya kingono. Ingawa mara nyingi marafiki wa jinsia mbili tofauti mapenzi yao huambatana na hisia na mihemko ya kimwili. Tambo alimpenda Janet, msichana aliyekutana naye na kusoma katika chuo kimoja huko Ulaya kwa mapenzi ya kirafiki tu na si vyenginevyo.

Licha ya Janet kuonekana mrembo sana katika hali zote za mwili yaani umbo, sura, mavazi na mambo mengine yanayompelekea mwanamme avutiwe na mwanamke kwa kupatwa na mhemko wa hisia za mapenzi ambazo hupelekea kupanda kwa pepo wa ngono. Tambo kamwe hakuathiriwa na uzuri huo na kumtamani kimahaba Janet, hakujali uzuri wala heba yake. Wataalamu wa masuala ya Saikolojia na Mahusiano wanaanini kwamba mapenzi ya urafiki husaidia sana kutoa tamaa ya kimwili na kuzingatia kufahamiana zaidi kwa marafiki na dunia kwa jumla. Kwa mnasaba huo Tambo alisuhubiana na Janet kama rafiki tu wa kawaida na kuwa pamoja nae katika masuala yao ya masomo, maongezi na kubadilishana mawazo wakati wanapokutana nyumbani kwake..

4.4.6 Dhamira ya Mapenzi ya Dini/Imani

Dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya mwanadamu na mola wake (BAKIZA, 2010). Dini ni imani juu ya kuwepo Mungu muumba aliye muweza na mwenye nguvu juu ya kila kitu. Mmiliki wa ulimwengu, ambae amempa binadamu roho ambayo huendelea kuishi baada ya kifo cha mwili (Hornby, 2005). Imani ni kuwa na yakini au uhakika moyoni juu ya kuwepo kitu au jambo fulani lisiloonekana machoni lakini kuna dalili za kuthibitisha kuwepo kwake. Kwa hivyo ili mtu awe na imani juu ya jambo lolote lile asiloweza kuliona, hana budi kuwa na ujuzi wa kina utakaompa hoja au dalili za kutosha zitazomkinaisha moyoni kuhusu kuwepo kwa jambo. Aidha dini ni mfumo au utaratibu wa maisha anaofuata binadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinagsi na kijamii (IPC, 2004) Kwa maana hii basi mwanadamu hawezi kuishi pasi na kuwa na dini. Mapenzi ya dini nayo yanaonekana kujitokeza kupitia data ifuatayo:-

“Warida alipenda kujitambulisha na Mungu na dini yake pia kwa njia ya vitendo kuliko maneno matupu yasio na mashiko katika maisha ya mwanadamu. Alijifundisha kitabu cha Mungu kwa idili. Akahifadhi juzuuthelathini za kitabu hicho na tafsiri yake kwa muda usiokuwa mrefu. Kisha akaingia katika hadithi za mtume kisha alifundishwa kuhifadhi na kusoma maulidi ya barazanji, pia alishiriki kwa nia na ari katika maulidi ya homu na dhikiri, pia alijitia katika kuvuta nyuradi za matamko baada ya kuswali kila swala” (uk 108-109).

Kwa mijibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa msomaji wa kazi ya fasihi kutafsiri kazi hiyo kwa mujibu wa muono na uzoefu wake kwa jamii kupitia data hiyo hapo juu, mwandishi ameonesha mapenzi ya dini. Dini kama inavyoelezwa kuwa ni mfumo au utaratibu wa maisha anaofuata mwanadamu katika kuendesha maisha yake ya kila siku, hapana shaka yoyote kuwa mwanadamu katika harakati zake zote za maisha yake ya kila siku atakuwa anao mfumo au utaratibu wa maisha anaofuata na hiyo ndio dini. Mtafiti amebaini dhamira ya mapenzi ya dini ambayo imejikita katika misingi ya dini ya Kiislamu. Warida moja kwa moja ameonekana kuwa karibu sana na mambo yanayopendezesha kwa Mola wake, mwandishi anavyothibitisha kuwa alihifadhi juzuuthelathini za kitabu cha Quran na tafsiri yake, hadithi za Mtume, ibada ya swala pamoja na mambo mengine mengine ya dini ni dhahiri kuwa yote haya hakuyafanya kibubusa tu (kufuata mkumbo) bali ni kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo juu ya dini yake. Mapenzi ya dini/imani pia yameweza kubainika kwa mwalimu wa Warida wa chuoni mwalimu Mwandoa (uk. 108).

4.4.7 Dhamira ya Mapenzi ya Mazingira

Mazingira ni jumla ya mambo yanayomzunguka kiumbe pahali alipo. (BAKIZA, 2010) Mazingira yana nafasi katika maisha ya mwanadamu ya kila siku hasa ikizingatiwa kuwa mwanadamu mwenyewe ni sehemu ya mazingira hayo. Kwa minaji hiyo basi ndio maana suala hili limepewa kipaumbele katika kuhifadhi, kulinda na kusimamia kikamilifu utunzaji wake ili yasiharibiwe. Uharibifu wa mazingira hupelekea athari kubwa ikiwemo suala la mabadiliko ya tabia nchi kitaalamu inajulikana kama “*climate change*” tatizo linalokumba nchi nyingi duniani. Miiongoni mwa njia kuu za utunzaji wa mazingira ni pamoja upandaji wa miti kwa wingi, utunzaji wa vyanzo vya m aji pamoja na utumiaji mzuri wa maji hususani katika shughuli za kilimo ili kuepuka tatizo la ukame katika nchi. Mazingira ambayo yanamzunguka mwanadamu yanaweza kuwa mazingira ya asili ambayo huhusisha vitu kama misitu, milima, maziwa, mito, bahari, mabonde nakadhalika. Mazingira ya kutengeneza yasiyo ya asili ni kama vile majengo ya kuishi, viwanda, na mengineyo. Mapenzi ya mazingira katika riwaya inayotafitiwa yameonekana kujitokeza kuititia data ifuatayo:

“Kila siku Bi Chani alipopata kumbikizi, hata za muda mchache, alichagua kumsimulia Tambo kitindamimba chake kadhia yake na kadhia ya ye ye na rafiki yake wa utotoni na ukubwani, Bwana Mansour mumewe na babake Tambo. Bi Chani alimwambia Tambo kuwa kila siku yao ilikuwa siku iliyokamatana vyema na pwani. Yaani wawili hao walikuwa na mapenzi makubwa ya pwani na pwani ilikuwa na mapenzi kwao kupita kiasi” (uk.74).

Data hii inaonesha dhahiri mapenzi ya mazingira ya bahari/pwani. Bi Chani na mume wake tokea enzi walikuwa na mapenzi mno na pwani katika maisha yao yote tangu utotoni mpaka walipoona bado walikuwa na hamu na mapenzi na mazingira

ya pwani. Mapenzi hayo ndio yaliyompelekea Bi Chani kupelekwa pwani kila siku hata wakati akiwa yuko katika hali ya uzee uliochanganyika na upotevu wa kumbukumbu bado ana hamu ya kufika pwani na kuangalia mazingira kitu ambacho alichokipenda sana.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa mwandishi anaitaka jamii ithamini na kupenda mazingira. Mazingira husaidia mwanadamu kuishi katika hali ya utulivu furaha na amani kwa sababu hupendezesha nafsi, hurutubisha afya na hufurahisha moyo. Dunia leo hii inapiga kelele katika suala zima la kuboresha mazingira kutokana na umuhimu wake mkubwa kwa mwanadamu. Bi Chani na mume wake walipenda sana mazingira ya pwani kitu ambacho kimekuwa urithi mpaka kwa watoto wao Tambo na dada yake Mwavile nao kuwa na mapenzi na pwani katika maisha yao.

4.4.8 Dhamira ya Mapenzi ya Kazi

Kazi ni shughuli yoyote ya halali anayofanya mtu kwa ajili ya kupata riziki ya kuendesha maisha yake ya kila siku. Kazi ni sehemu muhimu ya maisha ya binadanu hivyo ina nafasi kubwa katika mustakabali mzima wa maisha. Aidha kazi inafafanuliwa kuwa ni utendaji unaotumia nguvu ya akili au ya mwili ili kufikia lengo fulani, ambalo mara nyingi ni faida ya kiuchumi ili kuweza na kuwezesha kuendelea kuishi. (<http://sw.m.wikipedia.org>wiki>) Kwa mantiki hiyo kazi ni wajibu na vilevile ni haki ya msingi ya kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anapaswa kufanya kazi. Pasi na kuwa na kazi mtu huwa na msongo wa mawazo, hunyong'onyea na kujiona hana maana hasa kama ukosefu wa kazi unachukuwa muda mrefu na kumzuia asiweze kupanga mipango mbalimbali ya maisha yake kwa

sababu ya kukosa kujitegemea. Mapenzi ya kazi vilevile yamebainika kupitia data hii ifuatayo:

“Ibada ya mwanzo katika maisha yetu ni kazi. Kazi ni ibada pana. Hasa kujilisha na kulisha familia yako. Kazi ni kujiona wewe ni binaadamu kamili. Kazi ni heshima ya daraja la kwanza . Kazi huipa nchi yako fahari. Kazi pia inajenga mshikamano wa mtu na mtu, uhusiano ambao lazima uwepo. Iwapo mshikamano huo umekimbia lazima urudi...” (uk.47- 48).

Data hii imeonesha kuwa kazi ndio msingi wa maendeleo na ndio kipimo cha maisha ya mwanadamu kwa mnasaba huo jamii iwe na mapenzi ya kufanya kazi katika suala zima la maendeleo. Tambo anaamini kwamba suala la ibada ya sala lazima ifuatane na dunia na sio kwa akhera tu pekee, kwa maana kwamba watu wakishamaliza kufanya ibada wasipweteke bali watawanyike na kufanya shughuli za kujipatia rizki za halali. Katika maandiko ya dini inaelezwa kuwa hata Mitume na Manabii walifanya kazi mfano Nabii Daudi (AS) alikuwa anafanya kazi ya kutengeneza mavazi ya vita kwa kutumia chuma. (Quran 21: 80). Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo inampa uhuru msomaji wa kazi ya fasihi kutafsiri kwa mujibu wa muono wake kutokana na uzoefu wa jamii husika kupitia dondo ya hapo juu mtafiti amebaini kuwa mwandishi anaihamasisha jamii kuwa na mapenzi ya kufanya kazi ili kuweza kuondokana na utegemezi. Jamiii ambayo watu wake ni wavivu hawapendi kufanya kazi daima huwa na maendeleo duni.

4.4.9 Dhamira ya Mapenzi ya Pesa/Mali

Mali ni kitu ambacho kimo katika mamlaka ya mtu katika vitu vya thamani kama vile nyumba, gari, mashamba nakadhalika. Mtaalamu wa masuala yanayohusu Sosholojia Ritzer (2008) anasema kuwa mwanadamu ni mtu mwenye tamaa ya mali

na kila mara hutaka kuwa ndiye mtu mwenye mali kuliko wanajamii wote. Data ifuatayo inathibitisha hilo mwandishi anasema

“Lakini bwana wangu huyu anapenda sana pesa, hatosheki na pesa wala mali. Yumo katika mvuto wa hiki na kile, mikutano, semina, makongamano, mazungumzo na mipango ya biashara ambayo vikao vyake huendelea zaidi ya wiki... Yote hayo yanakamatana na pesa. Hakai nyumbani vya kutosha. Hakai hata kidogo nyumbani. Hana hata nafasi ya kulala kitandani na mimi ” (uk.165).

Kupitia data hii mwandishi ameonesha kwamba wanadamu wana mapenzi makubwa ya kupenda pesa/mali na hili linadhihirika wazi katika maisha tunaona wakati mwengine watu hufikia hadi kutoana roho kwa sababu ya mali tu. Maburuki mume wa Salila alikuwa na mapenzi ya pesa/mali kupita kiasi hatosheki na mali, hali ambayo ilipelekea mke wake kukosa raha katika maisha ya ndoa. Licha ya Salila kutimiziwa kila kitu na mumewe ikiwemo chakula, mavazi na magari ya kifahari ili afurahi lakini hakuwa na furaha kutohana na kuwa mbali na mume wake. Baadhi ya haki zake hazikuweza kutimizwa wakati mume akiwa katika harakati za kutafuta pesa huku na kule.

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amebaini kuwa katika jamii wapo watu wenye mapenzi na pesa/mali kuliko kitu chochote. Maburuki ni kiwakilishi cha watu hao. Tamaa ya pesa ilimfanya atokwe na imani na huruma kwa sababu aliweza hata kushawishi mke wake wakubali kuliiza shamba lao la urithi kwa rafiki yake Mwingereza. Shamba ambalo mama yao (Bi Chani) alilipigania kwa muda wa miaka kumi na tatu (13) anapanda na kushuka mahakamani kulidai hadi pale alipolitia mikononi wakati vuguvugu la mabadiliko lilipopamba moto.

4.4.10 Dhamira ya Mapenzi ya Elimu

Elimu ni ujuzi ulioambatana na matendo unaomtoa mtu katika hali duni na kumpeleka katika hali bora na ya ufanisi zaidi. Kwa maana hii elimu ni ujuzi ambao hauishii kwenye kujuu tu lakini hukamilika pale itakapomwezesha mwenye kuwa nayo kubadilika na kutenda kwa ufanisi zaidi kuliko yule asiyekuwa nayo kwa sababu hawi sawa mwenye elimu na asiyekuwa na elimu. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza elimu ni kitu adhimu sana inapopaliliwa. Haifai kutumiwa kama nyenzo ya utabaka na ukabila. Chini ya elimu ni utu na huo ndio unaopaswa kutiliwa maanani na kupaliliwa kwa udi na uvumba. Elimu ndio takrima ya kwanza aliyokirimiwa mwanadamu na Mola wake. Katika Qurani inaelezwa kuwa, jambo la kwanza alilitotunukiwa Adam mara tu baada ya kuumbwa ni kupewa elimu. *Na akamfundisha Adam majina ya vitu vyote* (2:31). Majina ya vitu vyote inaashiria fani zote za elimu ambazo anahitajia mwanadanu hapa duniani ili afikie kwa ufanisi lengo la kuubwa kwake. Ili jamii yoyote ile iweze kuendelea na kuwa na ustawi uliotukuka elimu ndio jambo la kwanza linalostahiki kupewa kipaumbele. Data inayofuata inatuthibitishia mapenzi ya elimu.

“Mansour tayari alikuwa darasa la tano shulenii lakini akili yake ilikuwa kubwa na fahamizi kuliko akili ya mwanafunzi wa darasa la nane. Alipenda sana kusoma. Alipenda sana vitabu. Alipenda sana kuuliza maswali na kupima majibu yake. Alipenda sana kuwachokoza makusudi wazazi wake ili tu apate nafasi ya mjadala fulani, Alipenda sana kuuliza maswali ya kidini, kiutamaduni na kisiasa” (uk.117).

Data hii imesadifu na kudhihirisha wazi mapenzi ya hali ya juu katika suala la elimu. Kwa mantiki hiyo suala la kujielimisha ni muhimu katika jamii kukosekana kwake ni kuiangamiza jamii na taifa kwa ujumla. Kuangamia kwa jamii au taifa lolote lile si lazima kutumia silaha za maangamizi kama vile nyuklia na mabomu ya

atomiki la hasha. Njia nyepesi ya kuiangamiza ni kuviza na kudumaza mfumo wa elimu tu basi. Wasomi mbumbumbu watakapokabidhiwa dhamana katika sekta mbalimbali hapo ndio ambapo wagonjwa watafia mikononi mwa madaktari, majengo yataanguka mikononi mwa wahandisi, pesa zitapotea mikononi mwa wachumi, haki itapotea mikononi mwa mahakimu, mapenzi na utu nao pia utapotea mionganoni mwa wanajamii kutokana na ukosefu wa elimu.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa dhamira hii haikutokea kimzaha bali mwandishi anaitaka jamii iamke na iwe na mapenzi ya elimu. Elimu ni muhimu katika mustakabali wa mtu mmoja mmoja, jamii na taifa kwa ujumla. Mfano mzuri nchini Tanzania mara baada ya kupatikana kwa uhuru mwaka (1961) serikali chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere iliona ni jambo la busara kuhakikisha kuwa kila eneo katika nchi linakuwa na shule ili watu wake wapate haki ya elimu. Kama hiyo haitoshi iliamuliwa kuwa elimu ya msingi iwe ni ya lazima na itolewe bure ili kusaidia kupunguza adui ujinga. Hamu na shauku ya kupenda elimu na kujifunza vitu mbalimbali ndio kunakoifanya akili iweze kufunguka na kuwa na upeo wa hali ya juu katika kufahamu mambo mengi zaidi katika njanya mbalimbali za maisha.

Kwa ujumla mtafiti anakubaliana na Robert (1958) aliposema kuwa, *Mapenzi kwa mwanadamu kama mshipa na damu au mti na mzizi kwamba ni vitu visivyoweza kutenganishwa kama ilivyo damu na mshipa katika mwili wa mwanadamu au mti na mzizi ndio yalivyo mapenzi kwa mwanadanu hayawezi kuepukika*. Kwa mantiki hiyo mtafiti amebaini dhamira ya mapenzi imejitokeza kupitia miktadha tofauti kama

ilivyoonekana. Kwa hivyo ni vyema yale mapenzi mazuri yaendelezwe na yale mabaya yaepukwe kwa lengo la kujenga jamii iliyobora.

4.5 Kuchambua Mbinu za Kisanaa Zilizotumika Kuwasilisha Dhamira ya Mapenzi

Lengo mahsusilishi la pili la utafiti huu lililenga kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Lengo hilo liliendana na swali lisemalo: Ni kwa vipi mbinu za kisanaa zimetumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? Mtafiti amebaini kuwa Prof. Said Ahmed Mohamed ni mmoja wa waandishi waliobobea katika matumizi ya mbinu za kisanaa katika kazi zake. Katika utafiti huu kuna mbinu kuntu za kisanaa ambazo zimetumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Mbinu hizo zimeorodheshwa katika jedwali hapo chini na kisha kuchambuliwa kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia baadhi ya misimbo ililiyoanishwa katika sura ya pili ya tasnifu hii.

Jedwali 02: Muhtasari wa Mbinu za Kisanaa katika Riwaya ya *Kamwe si*

Mbali Tena

Nambari	Mbinu za kisanaa katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena	Maelezo
1	Mbinu ya Matumizi ya Wahusika	✓
	i. Tambo	✓
	ii. Mwavile	✓
	iii. Janet	✓
	iv. Bwana Hassan na Bi Halima	✓
	v. Sele (Msurupwete)	✓
	vi. Jokha	✓
2	Mbinu ya Matumizi ya Lughya	✓
(i)	Matumizi ya Tamathali za semi	✓
	i Matumizi ya Tashbiha	✓
	ii Matumizi ya Tash hisi	✓
	iii Matumizi ya Sitiari	✓
	iv Matumizi ya Misemo	✓
	v Matumizi ya Methali	✓
	v Matumizi ya Taswira	✓
(ii)	Matumizi ya Mbinu nyengine za Kisanaa	✓
	i Matumizi ya Mubalagha/Chuku	✓
	ii Matumizi ya Takrir	✓
3	Mbinu ya Matumizi ya Mandhari	✓
	i Mandhari ya Pwani/Ufukweni	✓
	ii Mandhari ya Nyumbani	✓
	Jumla Kuu	21

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Oktoba 2018

4.5.1 Mbinu ya Matumizi ya Wahusika

Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mwandishi kubeba na kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi. Katika kazi ya Fasihi, wahusika wanaweza kuwa

wanadamu, wanyama na viumbe vyengine. Wamitilla (2008), anaeleza kuwa wahusika ni nyenzo kuu ya fasihi kwa sababu wahusika ndio dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi. Matendo hayo ni nguzo kuu ya dhamira katika kazi inayohusika. Wahusika wanaotumiwa katika kazi ya sanaa ikiwemo riwaya, ni mionganini mwa mbinu za kisanaa ambayo mwandishi huitumia kupaza sauti yake kufikisha ujumbe alioukusudia kwa hadhira. Mwandishi Said Ahmed Mohamed ametumia mbinu ya matumizi ya wahusika wake katika kuwasilisha dhamira aliyokusudia. Hivyo mtafiti aligundua kuwa, dhamira ya mapenzi imewasilishwa kuitia mbinu hii ambapo wahusika mbalimbali wamaechorwa kisanaa ili kuwakilisha dhamira ya mapenzi kama ifuatatyoy:

4.5.1.1 Tambo

Muhusika Tambo, huyu ni muhusika mkuu wa riwaya hii ambaye ni mtoto wa mwisho wa familia ya Bi Chani. Tambo ni mhusika ambaye ametumiwa na mwandishi kuwasilisha dhamira ya mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo. Tambo alikuwa na huruma na mapenzi makubwa kwa nchi yake, mama yake na dada yake wa kulelewa pamoja (Mwavile) ambaye walipendana sana tangu wakiwa wadogo katika mapenzi ya udugu. Katika kudhihirisha mapenzi aliyokuwa nayo Tambo, mwandishi ametuchorea picha ya muhusika huyu akiwa tayari kumkabili mama yake na kumuhudumia kama mtoto mdogo. Mwandishi anasema:

“Mwanzo aliamua kujifunga kitambaa cheusi kuziba macho asimuone mama yake wakati alipokuwa akimvua nguo na kumpangisha lindini mamake. Kisha alimsafisha na kumnadhifisha. Tena alimvisha nguo safi. baadaye alizifua nguo chafu kwa mikono yake. Baada ya muda mrefu wa kutekeleza jukumu hilo, Tambo alivua kitambaa alichojifunga machoni ili kuukabili ukweli wa mambo wa kumuhudumia mama yake” (uk.73).

Data hii inadhihirisha dhamira ya mapenzi ya dhati ambayo mwandishi anataka kuiwasilisha kwetu kwa kutumia muhusika huyu. Katika mazingira tuliyozoea katika jamii ni nadra sana kuona mtoto wa kiume anabeba jukumu zito kama hilo la kumuhudumia mama na hasa ikizingatiwa kuwa yupo mtoto wa kike ambaye aliahidi kumtunza na kumlea mama huyo kwa mapenzi na ulinzi mkubwa. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kimatukio, mwandishi amemtumia mhusika huyu kisanaa kwa madhumuni ya kufikisha ujumbe kwa msomaji ambapo moja kwa moja inaonesha dhamira ya mapenzi ya dhati. Tambo kwa hiari yake anaamua kurudi nyumbani kwao kutoka Ughaibuni na kuja kuungana na dada yake Mwavile kumuuguza mama yao jukumu alilojipa mwenyewe kutokana na mapenzi yake. Kama hii haitoshi katika kuonesha mapenzi aliyokuwa nayo muhusika huyu mwandishi anasema kwamba Tambo alimjali mamake kuliko anavyojijali yeze mwenyewe (uk. 36).

4.5.1.2 Mwavile

Ni muhusika mwengine mkuu, mtoto aliyelelewa na Bi Chani na mumewe Bwana Mansour tangu akiwa mdogo wakati mjomba wake Bwana Kitwana alipomchukuwa kihadaa na kumleta katika nyumba hii. Baada ya kupewa pesa aliondoka na kumuacha Mwavile katika mikono ya wawili hao na kumwambia kuwa angekaa hapo milele kwenye watu wazuri na nyumba nzuri. Hii ilitokea baada ya wazazi wake wote kufariki na hapo ndio ukawa mwanzo wa Mwavile kuishi katika familia ya kina Tambo ambapo alilelewa kwa mapenzi, na uangalizi wa hali ya juu kama mtoto wao wa damu. Naye pia akawa na mapenzi makubwa kwa walezi wake na

ndugu zake (watoto wa Bi Chani). Mwandishi vile vile amemtumia muhusika huyu kuwasilisha mapenzi ya dhati kupitia data ifuatayo na anasema:

“Kwa ufundu wa uganga aliourithi Mwavile kwa mamake wa kulea, Bi Chani. Abuu alianza kupewa madawa ya miti shamba na mchanganyiko wa vyakula vyenye rutba. Kila siku mchana alilishwa mponda wa shelisheli uliochanganyishwa na vitunguu maji, vitunguu thomi, lozi na kunyunyizwa asali ili kusafisha damu na kuupa nguvu moyo, mapafu na mafigo yake. Jioni alilishwa ama wali wa kunde au wali wa ngano ili kuchangamsha sehemu zote za kiwiliwili chake. Kisha alikandwa kwa mafuta ya uto na kusingwa kwa vidole .kabla ya kulala alinyweshwa bakuli la uji wa mtama uliotiwa asali ya Pemba na pilipili manga ili arudishe nguvu zake zilizokwisha potea...”(uk.138).

Data hii haihitaji tochi, mwandishi ameonesha dhahiri shahiri mapenzi aliyokuwa nayo muhusika. Mwavile kwa mapenzi yake baada ya kumuokota Abuu kichakani akiwa hali mbaya kiafya wakati aliposhindwa maisha huko Ulaya na kurudi kwao. Anamchukuwa na kumpeleka nyumbani kumuhudumia kama mtoto mdogo kwa kumpatia madawa ya aina mbalimbali, kumpa vyakula vyenye virutubisho na kumkanda mwili kwa mafuta maalumu hadi pale alipopata nafuu na hali yake kuimarika. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure ambayo inasema kwamba kazi ya fasihi hupata maana kutokana na ishara zilizotumika kupitia msimbo wa kimatukio unaonesha matukio katika hadithi. Mwandishi amemtumia muhusika Mwavile kuonesha mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa ndugu yake. Licha ya Abuu kurudi Ughaibuni akiwa hohe-hahe hana chochote pamoja na hali yake kuwa tete kutokana na kuishi katika mazingira magumu huko alikotoka Mwavile hakumuacha tu hivi hivi aendelee kuteseka bali alijitolea kwa moyo wake wote kumuuguza ndugu yake na kumsaidia kwa hali na mali. Pasi na Mwavile kuwa na mapenzi ya dhati asingeweza kumshughulikia Abuu

kwa kumpa huduma muhimu hasa ikizingatiwa kuwa alikuwa na mgonjwa mwengine mama yao ambaye hakujimudu kwa lolote. Mapenzi ndio yaliyomsukuma kuyafanya haya yote.

4.5.1.3 Janet

Huyu ni musika mwengine ambaye ni Mzungu lakini inasemekana kuwa bibi yake wa mbali mno alikuwa Mwfrika mweusi aliyezaliwa katika Visiwa veya Viungo. Janeti alipenda na kuvutiwa sana na Tambo siku alipopiga goti kwa hushui na adabu kamili kumuokotea rundo la vitabu vilivyomdondoka alipokuwa akitoka maktaba kujisomea na huku pole nyingi zikitoka kinywani wakati ameinama chini anamwokotea Janet vitabu. Mwandishi anaeleza kuwa:

“Ilionekana kwamba Janet alitaka arambishwe weusi ili aondoe ugaga wake” (uk.26).

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara mwandishi amemtumia muhusika Janet kuwasilisha dhamira ya mapenzi yake dhidi ya Tambo. Kiudhati Janet alimpenda Tambo mapenzi yaliyojaa hisia za kimwili yaani mwanamke kumtamani mwanamume kimahaba kiasi ambacho mwandishi anaeleza kuwa Janet alitaka arambishwe weusi ili aondoe ugaga wake. Hii inamaanisha alitaka aonje mapenzi ya Tambo, mapenzi yaliyopindukia mipaka ya kiurafiki.

4.5.1.4 Bwana Hassani na Bi Halima

Hawa ni wahusika wawili wazazi wa Mwana Mkisi kwa jina jengine Warida. Bwana Hassani na Bi Halima walikuwa na mapenzi makubwa mno kwa mtoto wao huyo wa pekee kiasi cha kumdekeza kupita kiasi. Wazazi hawa walimpa jina la Mwana Mkisi mtoto wao kwa sababu alifananishwa na somo yake yaani malkia wa Mvita ya

zamani ambaye allikuwa mzuri wa sura, na mwenye kuwajali na kuwapenda sana raia wake kwa moyo wa dhati. Mwana Mkisi alikuwa mzuri sana, kiasi ambacho mbali na kupendwa na wazazi wake, uzuri na heba yake pia ulimfanya awe kipenzi cha kila mtu katika jamii yake. Kwa hivyo alihisi kwamba hawezi kufanya makosa bila ya kusamehewa na ndio maana alifanya kila alilopenda pasi na hofu yoyote ile.

Katika hali hii mwandishi anaeleza:

“Mapenzi na deko la wazazi wake waliompenda kwa mizani isiyokuwa ya kawaida yalimkoroga akili yake” (uk. 93).

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kuitia msimbo wa ishara unahusishwa na jinsi wasomaji wa kazi ya fasihi wanavyovumbua ishara, nukuu hii imeonesha mapenzi waliyokuwa nayo wahusika hawa kwa mtoto wao wa pekee. Imeonekana wazi kwamba Mwana Mkisi alipotambua kuwa wazazi wake wanampenda sana kuliko roho zao alianza kufanya vituko, alifanya lolote alilolipenda nafsini mwake bila ya kujali mila na desturi za watu wa jamii yake na bila ya kujali maumivu ya wazazi wake. Matumizi ya wahusika hawa si ya bure bure bali wametumika kwa lengo la kuonesha dhamira ya mapenzi. Mapenzi yaliyopelekea kuathiri tabia na mwenendo mzima wa mtoto kiasi cha kujipa kiburi na uhuru wa kufanya apendavyo bila woga.

4.5.1.5 Sele (Msurupwete)

Ni muhusika mwengine ambaye ni mionganoni mwa watoto wa Bi Chani na Bwana Mansour waliondoka Visiwa vya Viungo baada ya kuangushwa uluwa wa baba yao. Muhusika huyu naye ametumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika miktadha tofauti. Kwanza Sele anaonekana kuwa na mapenzi makubwa na nchi yake, hii inadhihirika pale alipoishi nje bila ya kubadilisha uraia

wake kama ambavyo hufanywa na watu wengine. Pamoja na hayo vile vile hakuisahau nchi yake kwa sababu baada ya miaka mingi kupita na mambo kutulia katika nchi yake, aliamua kurejea nyumbani kwao na kuja kushirikiana na wenzake kuijenga nchi. Wakati akiwa nyumbani jambo la mwanzo alianzisha vugu vugu la fikra za kubadilisha mwenendo mzima wa uongozi katika nchi. Kudhihirisha hili mwandishi anaeleza kupertia muhusika Sele akisema.

“Unajua hii nchi ni yetu sote. Ikirudi nyuma na kuangamia, sisi sote tutarudi nyuma na kuangamia pia. Tuondoe fikra ya huyu ana kabilia au asili gani na yule anatoka wapi katika historia ya nchi hii. Aliye bora mionganoni mwetu si yule tu anayechukuwa madaraka ya nchi hii bali ni yule anayeipenda sana nchi hii. Kuipenda nchi hii ni kuipa nchi yenyewe mfumo mpya unaojali haki, sheria na maendeleo ya kweli” (uk.192).

Data hii inadhihirisha mapenzi ya muhusika katika kuikomboa nchi yake. Sambamba na hilo pili, muhusika huyu pia alikuwa na mapenzi makubwa na mama yake. Sele mbali na kuishi jijini lakini hakuacha hata siku moja kwenda kijijini kumzuru ama kumtembelea mama yake ambaye bado alikuwa na ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu *memory gape* na kumshughulikia kwa kila hali. Hali hii pia inaashiria mapenzi. Kama hii haitoshi muhusika Sele pia anaonekana kuwa na mapenzi na Mwavile ambaye ni dada yake waliyelelewa pamoja ambapo alimuenzi na kumpenda kutokana na ushujaa wake wa kujitolea kumlea mama yao wakati yeye na wenzake wote wakiwa nje ya nchi. Kwa kupertia nadharia ya Simiotiki kwa kurejelea msimbo wa matukio unaohusu jinsi matukio yanavyofuatana kiathari na kiusababishi na jinsi matukio yanavyopatikana katika hadithi muhusika Sele ameonesha mapenzi aliyokuwa nayo kwa nchi yake, mama yake na pia dada yake. Mfano mwengine wa

wahusika walitumiwa na mwandishi kuibua dhamira ya mapenzi kama haya ni muhusika Zahran (uk. 199) na Samira (uk.201).

4.5.1.6 Jokha

Jokha ni muhusika ambaye ametumiwa na mwandishi katika kusawiri dhamira ya mapenzi wakati alipotaka kuolewa na Mzima mtu ambaye mama yake hakumpenda. Lakini kwa vile yeye ndiye aliyekuwa chaguo la moyo wake hakujali wala hakumsikiliza mama yake. Alifikia hadi kuhasimiana na mama yake ilimradi tu atimize kiu yake ya mapenzi kwa kuolewa na mtu aliyempenda. Katika mazingira kama haya mwandishi anaonesha wazi mapenzi aliyokuwa nayo Jokha kama inavyodhihirika kuitia nukuu ifuatayo:

“Nitaolewa na ninayempenda. Nitaolewa tu ukitaka usitake. Wallah nitaolewa na Mzima ukipenda usipende. Kwani wewe nani? Jokha alimfokea mama yake” (uk.182).

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kuitia msimbo wa kihementiki, unaojulikana kama msimbo wa kutamba na kusimulia kuitia nukuu hii, muhusika huyu anaashiria dhamira ya mapenzi mazito yaliyovuka mipaka ya kupenda mpaka kumfokea mama yake aliyemzaa kwa maneno makali pasi na kujali lolote kwa sababu ya kuathirika na mapenzi. Katika hali isiyokuwa ya kawaida Jokha anayafanya haya lakini tunaweza kusema kuwa si kwa amri au hiari yake bali ni kutokana na kuathirika kimapenzi kusikomithilika. Mapenzi yana taathira kubwa sana katika maisha ya mwanadamu. Masuala ya mapenzi ni moja kati ya mambo yenyewe uwezo mkubwa wa kuichanganya akili ya mtu na kumfanya mithili ya kichaa (Selhub, 2009). Hivyo moto wa mapenzi ulikwishalipuka katika moyo wa Jokha na kupelekeea kushindwa kuuzima na tayari akili ilikwisha kumvurugika akawa hasikii wala haoni.

4.5.2 Mbinu ya Matumizi ya Lugha

Matumizi ya lugha ni namna ya kuifinyanga lugha na kuwa tofauti na matumizi mengine yasiyo ya kifasihi ili iwe na mguso na kuvutia kisanaa. Katika kazi ya fasihi matumizi ya lugha huhusisha tamathali za semi, nahau, misemo na methali, matumizi ya picha, ishara au ujenzi wa taswira na mbinu nyengine za kisanaa. Waandishi katika kazi zao hutumia lugha teule iliyosheheni vionjo mbalimbali kwa lengo la kuzipamba na kutia nguvu maana pamoja na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kuwa matumizi ya tamathali za semi mbalimbali kama vile: Tashbiha, tashhis, sitiari, misemo, methali na mbinu nyengine za kisanaa mfano, mubalagha/chuku na takriri zimetumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi.

4.5.3 Matumizi ya Tamathali za Semi

Tamathali za semi kama ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vyta maana na mpangilio wa maneno hutumika ili kuleta maana mpya au msisitizo. Uhamishaji wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria (neno, fungu nakadhalika) kutokana na maana ya kiashiria kingine. Wamitila (2008) anatoa maelezo kwa kusema kuwa, tamathali za usemi ni kauli fupi fupi ambazo hutumiwa kisanaa na watanzi wa kazi za fasihi kulinganisha na kufananisha vitu viwili au zaidi vyenye sifa na tabia tofauti kama kwamba ni vitu vinavyofanana kabisa. Katika utafiti huu mtafiti amebaini kuwa kuna utajiri mkubwa wa matumizi ya tamathali za semi ambazo zimetumika katika kuibua dhamira ya mapenzi. Tamathali hizo za semi ni pamoja na:

4.5.3.1.1 Matumizi ya Tashbiha

Mulokozi (2002) na Senkoro (2011) wanaeleza tashbiha kuwa ni usemi unaotoa mfanano wa vitu, ni tamathali ambayo watu/ vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu/ vitu vengine kwa kutumia vilinganishi *kama, mithili, kama kwamba, mfano* wa nakadhalika. Kwa ujumla tashbiha ni tamathali ya semi inayoltinganisha vitu vyenye kushabihiana kwa sifa au tabia kwa kutumia maneno mahsus kama vile *kama, sawa na, mithili ya, mfano wa* na yanayofanana na haya. Kimsingi aina hii ya tamathali hutumika kulinganisha wakati ambapo kuna vitu viwili vinavyoltinganishwa vyenye mshabaha fulani wa sifa au tabia mfano kusema, *Ana upara kama jangwa la sahara*. Katika mfano huu kuna mlinganisho wa vitu viwili vyenye kushabihiana katika sifa au tabia, vitu hivyo ni *upara na jangwa*. Katika utafiti huu, mtafiti amebaini mwandishi Said Ahmed Mohamed katika riwaya hii ya *Kamwe si Mbali Tena* ametumia tashbiha kuipamba kazi yake na pia kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Miiongoni mwa tashbiha hizo ni:

“Utoton **walishikana kama chanda na pete**, nyumbani na nje. Nje michezoni au nje njiani walipokwenda shule au popote pale. Kila siku Tambo alifuatana na Mwavile mpaka alipomfikisha skuli yake ya wasichana. Kisha Tambo akaelekea skuli ya wavulana. Waliporudi nyumbani kutoka skuli, walingojeana kurudi pamoja. Walipokwenda machakani (tabia waliyoipenda) kula matunda walikwenda pamoja. Pwani pia kuvua samaki na vinyama vyengine na kisha kuburudika na utulivu wa bahari walikuwa pamoja” (uk.12).

Katika nukuu hii mwandishi ametumia tashbiha hii kulinganisha vitu viwili ambavyo kitu cha kwanza ni kitendo cha kushikana na kitu chengine ni chanda na pete. Kushikana ni hali ya kukamatana na kushirikiana katika kila jambo. Chanda ni kidole cha nne kutoka kidole gumba cha mkono. Pete ni pambo lenye umbo la duara ambalo huvaliwa kidoleni aghlabu hutengenezwa kwa madini kama vile dhahabu au fedha.

Mwandishi ametumia tashbiha muafaka kuonesha ishara ya mapenzi namna Tambo na Mwavile walivyokuwa wanapendana. Tukichunguza dondo hii kwa makini tutagundua kuwa wawili hawa walikuwa na mapenzi makubwa kiasi cha kushabihishwa kwao ni kama chanda na pete. Kwamba pete ikishawekwa katika kidole si rahisi kudondoka hadi pale itakapovuliwa.

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiurejelezi unaojengwa na viashiria vya kiutamaduni. Tashbiha hii imetumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi ya dhati baina ya Mwavile na Tambo namna walivyopendana tokea wakiwa wadogo ni mfano pete na kidole. Tunaona kuwa katika ndugu wote wa familia hiyo, wao ndio walioandamana pamoja kila wakati na kila mahali, hawakuachana popote pale walipokwenda iwe nyumbani na hata nje ya nyumba yao walikuwa pamoja hawatokani.

Pili, Aidha mwandishi Said Ahmed Mohamed ametumia tashbiha nyengine mbili sambamba kama ifuatavyo:

“Hatimaye Bi Halima hubaki amebogonyoka. Na mwisho hujikuta anafungua moyo wake **kumbembeleza Warida kama vile akimchombeza kitoto kichanga**. Kisha humtaka Warida samahani kwani **Warida ni jicho lake moja kama chongo**. Hivi ndivyo mama aliyofikia katika ukomo wa kupenda- sadiki usisadiki” (Uk. 100).

Kupitia dondo hii mwandishi ametumia tashbiha kulinganisha vitu. Tashbiha ya kwanza inalinganisha kubembelezwa kwa Warida na kuchombezwa kama kitoto kichanga. Tashbiha ya pili nayo inalinganisha Warida na chongo yaani mtu aliye na jicho moja lisiloona ambapo imesadifu kwani Warida ni mtoto wa pekee, mmoja tu kwa wazazi wake aliyepata mapenzi ya kupindukia. Mwandishi hakutumia

tashbiha hii katika kuisana kazi yake tu bali kwa madhumuni ya kufikisha ujumbe aliokusudia. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara unaohusu namna msomaji anavyovumbua maana za kiishara katika kazi ya fasihi, tashbiha hizi zinaashiria dhamira ya mapenzi ya kweli. Warida ambaye ni mtu mzima kubembelezwa kama kitoto kichanga hasa pale ambapo huangua kilio pindi mama yake anapomuelekeza juu ya jambo bay a ilolifanya ni ishara ya mapenzi ya mama kwa mtoto wake.

Tatu, Matumizi ya tashbiha yameendelea kujitokeza katika kudhihirisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* kama mwandishi anavyoeleza:

“Hata kama Mansour asingeonesha nguvu, ufundi na uhodari wake wa michezo, basi **Mwana Mkisi angemfuata tu Mansour kama mkia michezoni au bila ya michezo.** Kusema kweli Mwana Mkisi mwenyewe alikuwa mbioni kila siku na kila wakati kumfuata Mansour...” (uk 128).

Tashbiha hii imetumika kwa lengo la kuwasilisha dhamira ya mapenzi baina ya Mwanamkisi na Mansour, kwa kulinganisha vitu viwili ambavyo ni kufuata na mkia. Kufuata ni kitendo cha kwenda nyuma ya mtu na mkia ni sehemu ya mwisho ya mwili wa mnyama, ndege, samaki nakadhalika. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara unaohusishwa na jinsi msomaji wa kazi ya fasihi anavyofumbua maana za kiishara, tashbiha hii imeonesha mapenzi aliyokuwa nayo Mwana Mkisi kwa mpenzi wake kiasi cha kufananishwa na mkia kutokana na kumfuata kila mahali alipokwenda iwe michezoni au sehemu nyengine yoyote ile alikuwa pamoja nae. Mwandishi hakuitumia tashbiha hii burebure isipokuwa kwa madhumuni ya kumtaka msomaji afikiri na kujiuliza akilini mwake iwapo Warida alimfuata Mansour kila sehemu kama mkia kuna dhamira gani hapa ambayo

anataka kuiwasilisha kwa msomaji. Bila ya shaka yeote tunagundua kuwa ni mapenzi aliyokuwa nayo moyoni mwake kiasi cha kuandamana naye kama mnyama anavyoandamana na mkia wake popote pale anapokuwa.

Nne, Vile vile katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi mwandishi ametumia tashbiha inayoendana na dhamira hii tashbiha ifuatayo inatuthibitishia hilo.

“Swali la Mansour kupenda vitabu halikuwakera wazazi wake. Walimpa shehena nzima iliojaa maktaba yake kubwa kuliko mtoto yeote aliyewahi kununuliwa vitabu katika jamii hiyo. **Yeye alisoma vitabu vyote hivyo kama mdudu anayekula vitabu haraka haraka** – vitabu vya shule, vya kwao au vya nje ya darasa lao” (uk.117).

Katika dondo hii tashbiha hii inalinganisha usomaji wa vitabu na mdudu anayekula vitabu. Tashbiha hii nayo haikutumiwa na mwandishi kimzaha isipokuwa kwa nia ya kuibua dhamira ya mapenzi, jinsi Mansour alivyopenda sana kujielimisha kwa kusoma fani mbalimbali. King'ei na Amata (2001) wanaeleza kuwa Tashbiha pia huitwa tashbihi au mshabaha. Ni lugha ya ulinganishaji wa vitu halisi viwili vyenye mshabaha fulani. Kwa mantiki hiyo mwandishi anashabihisha usomaji wa Mansour wa vitabu na mdudu anayekula vitabu. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara tashbiha hii inaashiria mapenzi makubwa ya kusoma aliyokuwa nayo Mansour kiasi cha kumjenga kiakili na fahamu yake kupanuka zaidi kutokana na kusoma sana vitabu. Yote haya hayakutokea kwa bahati nasibu ni kutokana na mapenzi ya kujielimisha. Mapenzi ndio yanayoamsha ari na hamu ya mtu kutenda lile alilolipenda. Alipenda sana kusoma vitabu vinavyohusu mambo mbalimbali alisoma kila kitabu ambacho alinunuliwa na baba yake au aliagizwa na mwalimu wake awambie wazazi wake wamnunulie alifanya hayo kwa mapenzi pasi na kulazimishwa.

Mwisho, Tashbiha nyenginezo zilizotumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi ni:

- i. Walishikana **kama pete za mnyororo** zisizokatika (uk. 13).
- ii. Miondoko ilikuwa ya polepole **kama maarusi** pale alipofuatana na Mwana Mkisi mpenzi wake (uk.130).
- iii. Sele alibaki kugandamana na mama yake **kama nyama na mfupa** (uk. 189).
- iv. Jokha alisimama **kama nguzo kuitetea haki ya mapenzi** yake kwa Mzima (uk. 181).

4.5.3.1.2 Matumizi ya Tashhisi

Tashhisi ni tamathali ya semi ambayo hutumika kuvipa vitu visivyo na uwezo wa kutenda matendo ya kibinaadamu kutenda matendo hayo. Tashhisi ni tamathali ambayo vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo (Senkoro, 2011).

Tashhisi ni kukipa kitu kisichokuwa na uhai mkamilifu sifa ya kitu chenyе uhai kinachojitegemea mazingirani mwake (Mulokozi, 2003). Fasili hizo zinatubainishia kuwa tashhisi ni aina ya tamathali ambayo huvipa uhai na uwezo wa kibinadamu vitu ambavyo havina uhai wala si binadamu mfano *Mvua iliyonyesha imeitafuna na kuimeza ardhi yote*. Mfano huu wa tashhisi unaipa mvua sifa ya kibinadamu ya kutafuna na kumeza wakati haina uwezo huo. Mwandishi Said Ahmed Mohamed katika riwaya yake ya *Kamwe si Mbali Tena* ametumia tashhisi ambazo kimsingi zimesadifu kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Miongoni mwa tashhisi hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

“Hilo si jambo kubwa kwangu kuliko kukutupeni nyinyi wawili. Mama na wewe” alijibu Tambo kwa hamasa huku machozi yakianza kumlengalenga tena. **Moyo wa Mwavile ulikuwa unapiga beni.** Aliathirika kumuona Tambo anavyotiririkwa na machozi. Polepole alikwenda kumkumbatia na kumbusu shavu hili na hili...” (uk. 10).

Katika dondoo hii mwandishi ametumia tashhisi kwa lengo la kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Tashhisi ni mionganini mwa tamathali inayogusa zaidi hisia kwa kutumia picha hapa anaonesha moyo ambao unapiga beni. Kiuhalisia moyo hauwezi kupiga beni. Beni ni ngoma kubwa na pana iliyoambwa pande zote mbili na hupigwa upande mmoja kwa rungu na upamde wa pili kwa mkono kwa maana hiyo mwenye uwezo wa kupiga beni ni mwanadamu. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki inayohusu ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi moyo unaopiga beni ni ishara inayoashiria mapenzi jinsi Mwavile alivyopata mshtuko uliopelekea moyo wake kupiga mapigo ya nguvu na kasi baada ya kumuona ndugu yake mpenzi Tambo anatiririkwa na machozi anapofikiria kumwacha mama yake na dada yake wakati atakapoondoka na kwenda kutafuta maisha nchi nyengine. Kitendo cha Tambo kutokwa na machozi ndio jambo ambalo liliuathiri moyo wa Mwavile na kufanya mapigo ya moyo wake yapige kwa nguvu.

Sambamba na tashhisi hiyo mwandishi ametumia tashhisi nyengine ambayo inaakisi dhamira ya mapenzi. Kwa kuthibitisha hilo mwandishi anasema:

“Hapohapo uso wa Janet, wenyewe huzuni ukakunjuka. Uso ukatoa mwanga wa furaha katika ule wekundu wa damu yake iliyoonekana wazi wakati wa huzuni ya mtu mweupe. **Akatabasamu Janet!** **Tabasamu iliyojaa harufu ya mapenzi na ukweli.** Nani mwengine kama si Tambo? Aliwaza Janet. Tambo amesoma. Anajua. Anafahamu. Anapanga maneno. Anasafisha huzuni kwa braso ya matamko. Nani kama si Tambo, enh? (uk 26).

Katika mazingira ya kawaida tabasamu haiwezi kuwa na harufu lakini mwandishi ametumia tashhisi hii kuwasilisha dhamira ya mapenzi kwa hadhira yake. Janet na Tambo walikuwa marafiki tu wa kawaida ingawa awali Janeti alimpenda Tambo,

mapenzi zaidi ya urafiki. Kiudhati Janet alimpenda Tambo kutokana na mambo mengi ikiwemo uwelewa wake wa mambo mbalimbali kuhusiana na maisha ya watu, ukarimu, heshima pamoja na usemajii wake wa ufasaha ambaa anausifia kuwa hajapata kuuona kwa mtu yejote. Hali hii ndio iliyomfanya Janet kuwa pamoja kwa kumtembelea mara kwa mara, kufanya maongezi na kubadilishana mawazo.

Mwandishi pia katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi ametumia tashhisi ambayo moja kwa moja inaakisi dhamira ya mapenzi, anasema:

“Alipofika hapo Mansour aligeuka. Akapiga hatua za haraka na kutoweka . hakuonekana mpaka siku ya tatu. Wazazi wake walimtafuta kwa uvumba na udi, lakini hawakumwona. **Roho zao zilifanya vidonda kwa hofu ya kupoteza kitindamimba wao**” (uk. 121).

Roho ni kitu kisichoonekana ambacho kinaambatana na mwili ili kuuwezesha kuwa na uhai. Kidonda ni sehemu ya mwili iliyoumia kama vile kwa kujikata, kuchunika, kuungua nakadhalika. Kitindamimba ni mtoto wa mwisho kuzaliwa kwa mama ambaye kwa kawaida huwa anapendwa sana na wazazi. Kupitia tashhisi hii mwandishi anaonesha umahiri wake katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Dhamira ambayo inadhihirika katika tashhisi iliyokolezwa wino ni dhamira ya mapenzi. Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara unaohusu ishara na uashiriaji katika kazi ya fasihi, tashhisi hapa haikutumika kwa bahati nasibu tu bali ni ishara ya mapenzi yenye mnasaba na wazazi. Tashhisi hiyo imeashiria namna roho za wazazi hao zilivyoteseka kwa hofu na wasiwasi baada ya mtoto wao kutoweka nyumbani kwa muda wa siku tatu.

Matumizi ya tashhisi nyenginezo ambazo zimetumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi pia zimejitokeza katika kurasa zifuatazo:

- i. Akasubiri na kupigana na huzuni zake (uk. 7).
- ii. Yale maneno ya Mwavile na ule mkumbatio wake ulichemsha damu ya Tambo (uk. 11).
- iii. Sijui itakuwaje pesa hizo zikizima pumzi (uk.18).
- iv. Alijihisi nafsi yake inasafishwa kwa sabuni ya *lifebouy* (uk. 36).
- v. Ufukwe ulijivua na kujipambanua na maji ya chumvi ukawa uchi kama ulivyozaliwa (uk. 61).
- vi. Mara tu walipofika pwani, pwani iliwafungulia michezo ambayo wawili hao waliichangamkia (uk. 75).
- vii. Mapenzi yalilipua moto ndani ya moyo wa Tambo (uk.215).

4.5.3.1.3 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni mbinu ya matumizi ya lugha inayotumika kulinganisha vitu pasi na kutumia viunganishi kama ilivyo tashbiha mfano *Maisha ni safari au Elimu ni nuru.*

Mulokozi (2002) anaeleza kuwa sitiari ni tamathali ya senmi inayotumika kuumba picha fulani inayotoa athari fulani au inayoamsha mwitiko fulani. Ni kilinganishi cha kuhusisha vitu viwili au zaidi vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile. Maana hiyo ya kitu kimoja huhamishwa kwenye kitu kingine bila ya kutumia maneno yanayoashiria ulinganishaji kama mithili ya, mfano wa, kama kwamba nakadhalika (Madumulla, 2009). Sitiari ambazo zimetumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi ni kama zifuatazo:

- Kazi ni ibada (uk. 48).
- Kazi ni heshima (uk. 48).
- Maisha yetu ni kazi (uk..48).

Mwandishi ametumia sitiari hizi kwa madhumuni ya kusisitiza suala la kazi katika jamii ili kuepukana na hali ya duni ya maisha. Mulokozi (ameshatajwa) anasema

sitiari inatoa athari au mwito fulani ni sahihi kutohana na mwandishi anaposema kuwa “*Kazi ni heshima*” (uk 48). Heshima ni thamani ya utu wa mtu ama staha yake. Heshima ya mtu inapaswa kutunzwa na kulindwa. Kwa hivyo haikutumika kama mzaha tu isipokuwa inatupa taswira fulani kuona kwamba kazi ni kitu chenye thamani kwa kule kulinganishwa kwake na heshima.

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara, mtafiti moja kwa moja amegundua kuwa sitiari hii inawasilisha dhamira ya mapenzi kwa maana kwamba kila mtu anapenda heshima. Kazi pia inalinganishwa na *ibada*, kazi inalinganishwa na *maisha*. Kiuhalsia hakuna mwanadamu asiyependa heshima hata kama yeche atakuwa haheshimu wengine. Kwa hivyo sitiari hizi zimetumika katika kuamsha ari na hamu ya mtu kupenda kazi kama anavyopenda heshima, ibada na maisha yake yote kwa ujumla.

4.5.3.1.4 Matumizi ya Misemo

Matumizi ya misemo ni mbinu ya kisanaa ambayo hutumiwa na msanii wa kazi ya fasihi katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Senkoro (2011) anafasili misemo kwa kusema kuwa misemo ni maneno yanayotumika mara kwa mara yaliyo katika mazingira maalumu na kuleta maana maalumu. Misemo ni neno lenye upana na hutumika kuelezea matamko au kauli zinazoelezea ukweli fulani (Wamitila, 2003). Mtafiti anakubaliana na Senkoro (ameshatajwa) kuwa misemo ni kauli zinazoshabihiana na methali. Tofauti yao kubwa ni kwamba misemo huwa na upande mmoja na methali huwa na pande mbili kimuundo na kimpangilio. Ngole na Honero (2002) wanakitaja kigezo kinachotumika kutofautisha methali na misemo, ni uzito wa agizo au adili analolipata mwanadamu. Wanasema kwamba usemi amba

hautoi agizo au adili maalumu unaitwa msemo na ule ambao unatoa agizo au adili kwa mwanadamu unaitwa methali. Mfano wa methali ni kama *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Mchama ago hanyele huja akawia papo.* Mwandishi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ametumia misemo mbalimbali katika kazi yake ambayo lengo lake ni kusaidia kufikisha ujumbe aliokusudia. Misemo ambayo imetumika ni kama ifuatayo:

“Mansour alikuwa mwenzi wa Warida **nipe nikupe**. Ufundishaji wa madarasa yake yaliyuminika kwa vile wawili hawa walikuwa **chanda na pete**. Hawakutengana wala kubaguana kwa sababu ya ujuu au ya uchini wa ngazi ya jamii yao. Ulipowaona uliwaona pamoja kila kipembe na kila wakati. Walikuwa hawajali chochote ila nafsi zao” (uk.95).

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kuititia msimbo wa kiurejelezi unaohusu viashiria vyta kiutamaduni wa jamii husika *chanda na pete* ni ishara ya mapenzi inayoashiria mapenzi baina ya wapendanao. Tunashuhudia katika kumbi mbalimbali za sherehe za arusi wanandoa wakivishana pete, kuonesha kuwa wawili hao wanakuwa pamoja katika safari ya maisha yao ya ndoa pasi na kuachana. Mwandishi aidha anaendelea kutumia msemo mwengine ambao katika nukuu ifuatayo moja kwa moja inatudhihirishia dhamira ya mapenzi anaposema kuwa:

“Arusi ya Mwavile na Tambo ilifanywa miezi mitatu iliyopita. Kwa ajabu ya kila mtu arusi hii ilichanganyika na arusi ya Janet na Sele Msurupwete. Usiulize ilikuwaje kuhusu mapenzi ya Janet na Sele Msurupwete. Labda chanzo kilikuwa Tambo. Kwa vyovyote vile **jicho halina pazia na moyo ndio mchaguzi**. Arusi mbili hizo zilihudhuriwa na ndugu na marafiki ili kuwashongera maarusi hao” (uk. 215).

Jicho ni kiungo katika uso wa kiumbe hai kinachotumika katika kuona. Pazia ni kitambaa ambacho hufungwa sehemu kama vile mlangoni au dirishani ili kuzuia

kuona upande wa pili. Moyo ni kiungo muhimu cha ndani chenyé kufanya kazi ya kusukuma damu mwilini. Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia nukuu iliyotangulia, mwandishi ametumia msemo wa *jicho halina pazia na moyo ndio mchaguzi* kuonesha dhamira ya mapenzi ambayo yalipelekea kufungwa kwa ndoa baina ya Mwavile na Tambo na Janet na Sele (Msurupwete). Kiudhati ni kwamba jicho halina kizuizi wala mipaka katika kuona, linaweza kuona popote pale na moyo ndio hufanya maamuzi sahihi juu ya kile ambacho jicho limeona. Hali hii inaonesha kuwa katika mazingira ya kawaida viungo hivi huenda sambamba katika ufanyaji kazi wake (kuona na kupenda). Kwa hivyo jicho la Tambo liliona wengi lakini chaguo la moyo wake lilikuwa ni Mwavile na hivyo hivyo kwa Sele na Janet.

Vile vile matumizi ya misemo yenyé kuonesha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya

Kamwe si Mbali Tena yameonekana kupitia kurasa zifuatazo:

- i. *Kukaa sako kwa bako* (uk.69).
- ii. *Raha mustarehe* (uk.69).
- iii. *Mapenzi hayafichiki* (uk. 83).
- iv. *Nipe nikupe* (uk. 95).
- v. *Walimtafuta kwa uvumba na udi* (uk.121).
- vi. *Liwalo naliwe* (199).
- vii. *Tukutane mwambani sisi wavuvi wa pweza* (199).
- viii. *Mapenzi hayachagui ukubwa wala udogo* (uk.215).

4.5.3.1.4 Matumizi ya Methali

Methali ni semi fupi zenyé maana iliyofichika zinazokubalika na kutumika kufafanua ukweli wa maisha katika jamii. Senkoro (1982) anasema methali ni maelezo kuhusu matukio yadhihirishayo mfumo wa amali za kiutamaduni za jamii husika. Pamoja na kutumika kutolea maadili katika kazi za fasihi, methali pia hutumiwa kama njia moja

wapo ya kujenga mandhari ya kitamaduni. Methali hufuatana na mazingira, mila, desturi, silka za watu na utamaduni wao. Kutokana na hayo maneno au ufumbuzi wa methali si rahisi kupatikana kwa mtu ambaye hana uasili na sehemu ambayo methali hiyo imetoka. Kwa kawaida methali zina matumizi mengi yanayotajirisha fani na maudhui ya kazi ya fasihi. Matumizi ya methali katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* yametumika kama ifuatavyo:

Mama mwadilifu hamtupi mwanawe (uk.187).

Methali hii imetumika kwa madhumuni ya kuonesha dhamira ya mapenzi. Hii imekuja baada ya Jokha kupata misukosuko na matatizo katika ndoa yake. Jokha alilazimisha kuolewa na mume ambaye mama yake hakumridhia, kwa sababu kiudhati hakuwa na mapenzi ya kweli isipokuwa alitaka akate kiu yake ya mapenzi kutokana na ugonjwa aliokuwa nao wa kutamani wanawake weupe tu basi. Na ndio maana baada ya kwisha kumtia mikononi mume huyo alianza kumnyanyasa na kumpiga mke wake hadi kumtoa meno. Jokha aliamua kurudi nyumbani na kumuomba msamaha mama yake kwa yale yote aliyotenda. Naye mama kama kawaida ya mama ye yote mwenye mapenzi na mtoto wake, alimsamehe mwanawe bila ya kinyongo kwa kusema *Mama mwadilifu hamtupi mwanawe*. Licha ya mtoto huyo kumshambulia na kumfokea mama yake kwa maneno makali.

Kimsingi methali huwa na dhima ambazo hujitokeza kwenye masuala mbalimbali katika jamii. Mfano katika malezi methali hutumika kwa lenngo la kuonya, kuusia, kutoa maadili, kushauri na kufunza mambo mbalimbali ambayo humsaidia mwanadamu na kumuongoza katika misingi bora na imara. Kwa mintaarafu hiyo methali hii inatoa ujumbe kuwa mama ni mama hana kinyongo na mtoto wake hata

kama atamkosea. Hivyo ni wajibu wa watoto kufuata yale wanayoelekezwa na wazazi, wao wameshaona mengi na wanajua mengi. Vilevile methali nyengine inayorejelea dhamira ya mapenzi ni ile isemayo:

Kupenda kwingi na kuviza huwa (uk.109).

Methali hii pia imetumika kuonesha dhamira ya mapenzi. Kama tulivyokwisha kuona kwamba wazazi wa Mwana Mkisi ama Warida walikuwa na mapenzi makubwa mno kwa mtoto wao. Hata hivyo licha ya kumpenda kwao mapenzi yasiyopimika kwa mizani hawakumuacha tu hivi hivi afanye vyovyote vile atakavyo kama vile kuva mavazi yasiyokuwa ya heshima, kucheza nataki mbele ya hadhara ya watu, kusuhubiana na kijana wa kiume (Mansour) na mambo mengine yanayokwenda kinyume na mila, silka, desturi na utaratibu wa jamii na dini yake.

Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kimatukio, msanii hapa ametumia methali hii kwa nia ya kuwasilisha dhamira ya mapenzi kwa maana kwamba pamoja na mama kumpenda mwanawe kuliko roho yake lakini hakuacha kumuasa/kumuonya, kufunza pamoja na kumpa nasaha hata kama atakasirika ili kumlinda na kumuepusha asitumbukie katika dimbwi la upotevu wa maadili. Mzazi ambaye anampenda mtoto wake na anapenda awe muongofu anaweza hata kumchapa kwa bakora pindipo atatenda jambo linalokwenda kinyume na maadili. Na sio kama inavyoonekana sasa hivi kwamba mzazi anaogopa kumgomba mtoto wake kwa kuhofia atakasirika.. Mapenzi ya aina hii si mapenzi ya kweli na hivyo yanayoweza kuleta maviza badala ya kumjenga mtoto yanaweza kumviza na kumfanya kuwa zao bovu la jamii inayohusika.

Methali nyengine ambayo mantiki yake inakaribiana sana na hii ni ile isemayo:

(i) *Apendwaye akajua haachi kujizuzua* (uk. 114).

4.5.3.1.5 Matumizi ya Taswira

Taswira ni matumizi ya lugha yanayotoa picha fulani inayofikirika kimawazo kwa msomaji. Senkoro (1982) anaelezea taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi za fasihi. Anaendelea kusema kuwa kuna aina tatu za taswira nazo ni taswira za hisia, taswira zioneukanazo na taswira za mawazoni. Njogu na Chimerah (1999) nao wanasema taswira hutumika kuleta picha au hali fulani akilini mwa msomaji au msikilizaji. Anaweza kuona, kusikia, kuonja, kunusa, kupenda, kuchukizwa au kudharau kilichosawiriwa kutegemea nguvu ya taswira wenyewe. Mawazo ya wataalamu wote yanaonesha kuwa taswira ni matumizi ya picha yanayopambanuliwa kwa uteuzi mzuri wa maneno kutoa maana ya dhamira zilizojitokeza katika kazi ya fasihi. Matumizi ya taswira yameonekana mwandishi aliposema:

“...Mwavile hakusema kitu. Alitupa macho yake chini kutazama mchezo wa miguu yake alipokuwa akiitembeza kutekenya maji ya futi ufukweni. Alikaa hivyo kwa muda kidogo huku kapuza maneno ya Tambo na kumpuuza Tambo mwenyewe. Halafu alinyanyua uso kumtazama Tambo ndani ya ute wa machozi yaliyokuwa yanamlengalenga. Kisha alibanduka pale. Akamsogelea Tambo. Alimsogelea kiasi cha nusu inchi tu hivi kukosa kugusana naye. Alimtazama Tambo kwa namna ambayo Mwavile hajawahi kumtazama. Alimtazama kwa mapenzi na shauku kubwa. **Mapenzi yaliyolipua moto ndani ya moyo wa Tambo.** Ghafla Mwavile alinyoosha mkono kuukamata mkono wa Tambo. Kisha aliunyanyua mkono wa Tambo akauweka kifuani pake. **Pale penye moyo wake, uliokuwa ukidunda kama ujiti wa saa.** Kisha Mwavile akasema. “Nani mwengine ambaye ningemtaka kama si wewe? Nani kuliko wewe? (uk. 214-215).

Katika dondoo hili mwandishi ameonesha taswira ya mapenzi yaliyoshamiri baina ya wawili wapendanao, mapenzi ambayo yanaamsha hisia nzito nyoyoni mwao. Hii inatokana na picha inayojengeka akilini mwa msomaji ambayo kiudhati inaonesha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Taswira mara nyingi huambatana na matumizi ya tamathali za usemi hasa *sitiari* na *tashbiha* kama inavyoonekana katika nukuu iliyotangulia inayomfanya msomaji aweze kuona jinsi ambavyo mapenzi yanaathiri moyo wa mtu mwenye kupenda na kuufanya upige mapigo yake kwa kasi isiyo ya kawaida.

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kwa kutumia msimbo wa kiishara, mtafiti amegundua kuwa taswira hii ni ishara ya mapenzi ya kweli. Mwavile kunyanya mkono wa Tambo na kuuweka kifuani pake sehemu ya moyo ni ishara ya kuwa anampa moyo wake mapenzi ya dhati kutoka moyoni na sio mdomoni. Moyo ndio fichio la siri. Kwa hivyo kitendo hiki ni dalili tosha ya kuonesha mapenzi. Tambo na Mwavile walipendana tangu wakiwa wadogo wakati wakiwa nyumbani kama ndugu.

4.5.3.2 Matumizi ya Mbinu Nyengine za Kisanaa

Katika kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya teule, mtafiti amebaini uwepo wa mbinu kadha za kisanaa ambazo zimeongeza ladha na kudhihirisha wazi ujumi na uzuri wa pekee wa kazi ya mwandishi katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Mbinu hizo ni Mubalagha/Chuku na Takriri.

4.5.3.2.1 Matumizi ya Mubalagha/Chuku

Mubalagha ama chuku ni utiaji wa chumvi katika masimulizi. Njogu na Chimerah (1999) wanaielezea mubalagha kuwa ni kutia chumvi katika kueleza jambo ili kulipa uzito. Hali hii pia hujitokeza katika kazi za kifasihi ili kuzipamba kisanaa, kuongeza utamu wa lughu na kuleta athari fulani. Mulokozi na Kahigi (1979) wanafasili mubalagha/chuku kuwa ni mbinu ya kisanaa ambapo kitu, mtu, au jambo hukuzwa zaidi ya uwezo wake. Mfano mtu anaweza kusema: “*Alivuta mdomo hadi kufikia karibu urefu wa nusu mita.*” Hapa kuna mubalagha ama kutia chumvi kwa sababu si jambo la kawaida kwa binaadamu kuweza kuvuta mdomo hadi kufikia urefu wa nusu mita. Mwandishi katika kazi yake ametumia mubalagha zifuatazo:

Mwavile alikuwa tayari kumuokoa yeyote aliyekuwa anazama hata kama ingembidi kuogelea bahari saba (uk.13).

Alikuwa tayari kumpigia Tambo magoti na kumuomba samahani elfu moja (uk.13).

Kwa kawaida mtu haonji halua mara moja bali mara milioni moja (uk. 143).

Ghafla tena alimvaa mama yake kifuanaki akambusu mashavuni mara milioni ngapi sijui (uk. 187).

Katika mifano hiyo tunaona kuwa kuna mubalagha ndani yake, mwandishi anaonesha uwezo wa kupindukia wa binadamu katika kutenda mambo. Massoud (2013) anasema moja ya sifa kubwa ya chuku ni kwamba inatia mkazo katika maana. Kwa mnasaba huu matumizi ya mubalagha yaliyotumika katika mifano hiyo yanaonesha wazi dhamira ya mapenzi. Katika (uk.187) mwandishi anasema:

“*Ghafla tena alimvaa mama yake kifuanaki akambusu mashavuni mara milioni ngapi sijui*” (uk.187).

Mwandishi kupitia nukuu hii ameonesha mapenzi yaliyokithiri kwa Jokha wakati aliporudi kwa mama yake kumuomba msamaha baada ya kupatwa na mateso na mashaka makubwa katika ndoa yake. Kwa mintaarafu hiyo kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara, mubalagha/ chuku hii imeafiki kusawiri dhamira ya mapenzi. Busu (kiss) ni mguso wa mdomo juu ya shavu au mkono wa mtu ambao huashiria furaha, heshima au mapenzi. Kitendo hiki kinadhihirisha utii na mapenzi ya hali ya juu ya Jokha wakati anaomba msamaha kutokana na masahibu/ mitihani iliyomsibu wakati alipokataa maamuzi ya mama yake ya kuolewa na mume ambaye hakumridhia.

4.5.3.2.2 Matumizi ya Takriri

Takriri ni mbinu ya utumiaji wa lugha ambapo neno au maneno hurudiwarudiwa kwa nia ya kutia mkazo au kusisitiza jambo fulani. Molokozi na Kahigi (1979) wanaeleza takriri kuwa ni uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata sentensi katika kazi za kifasihi. Senkoro (1982) anasema takriri ni marudio kwenye sentensi au kwenye usemi ambao huleta msisitizo. Anaendelea kusema takriri ziko za silabi, neno, sentensi nakadhalika. Maelezo ya wataalanu hawa wote yanaonesha kuwa takriri ni mbinu ya kifani ambayo hutumiwa na wasanii katika kutoa msisitizo wa maudhui iliyokusudiwa katika kazi za sanaa. Mwandishi Said Ahmed Mohamed ametumia takriri kama zifuatazo:

Kinachotakiwa ni pesa. Pesa. Pesa tu!! (uk.166).

Nitaolewa na ninayempenda, nitaolewa tu , wallahi nitaolewa. (uk. 182).

Lazima nchi hii iwe yetu sote. Lazima, lazima, lazima (uk.201).

Katika sentensi hizo kuna takriri neno, maneno ambayo yamerudiwa rudiwa kuonesha msisitizo wa jambo fulani. Kwa hakika takriri hizo zimetumika kwa lengo maalumu la kufikisha ujumbe kwa hadhira kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Tukiangalia mifano hiyo hapo juu ya takriri tunaona kwamba mwandishi anatilia msisitizo wa kile anachotaka kukiwasilisha kwa jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kimatukio takriri hizo zimetumiwa na mwandishi kuonesha dhamira ya mapenzi. Mfano katika (uk. 182) msanii anasisitiza mapenzi ya ndoa, Jokha anadai haki yake ya mapenzi ya kuolewa na mume anayempenda. Pamoja na hayo msisitizo unaonekana kutumika katika mapenzi ya mali/pesa na mapenzi ya nchi.

4.5.4 Mbinu ya Matumizi ya Mandhari

Kazi ya fasihi haina budi kuhusishwa na mandhari. Mandhari ni ile sehemu ambayo matukio ya hadithi au masimulizi yanafanyika. Ni mazingira ya kazi ya fasihi, ni hali ya maumbile ilivyo na inavyoonekana ambayo hutumika katika kujenga masimulizi ya riwaya, tamthilia, ushairi au hadithi fupi (Senkoro, 1982). Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa mandhari ni nyenzo muhimu sana katika kazi ya sanaa ya fasihi kwa vile matendo mbalimbali husawiriwa ndani yake. Ufundi wa kuchora mandhari utajitokeza kwa jinsi msimulizi anavyotupa picha halisi, picha inavyoonekana waziwazi juu ya mandhari iliyohusika. Kwa mfano kama mwandishi anataka kuonesha dhamira ya ulevi, basi hutumia mandhari ya kilabuni ambayo husadifu vyema dhamira iliyokusudiwa na hivyo hivyo kwa dhamira myengine.

Katika kazi ya fasihi mandhari huweza kuwa ya kidhahania (kubuni) au halisi. Mandhari dhahania ni mandhari ya mawazoni ya kufikiria ambayo hutupatia taswira

fulani akilini mwetu juu ya mambo yanayotokea katika ulimwengu halisi mfano mandhari ya *Kufikirika* na *Kusadikika* yaliyochorwa kutoka katika riwaya za Shaaban Robert. Mandhari halisi ni ile mandhari ambayo tunaweza kuiona, kuitembea na kadhalika (Nyangwine 2002). Mwandishi Said Ahmed Mohamed amefanikiwa kutumia mandhari halisi ambayo ndani yake tunakutana na mienendo na matendo mbalimbali ya wahusika. Kwa hivyo mtafiti amegundua kuwa katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* zipo mandhari halisi ambazo zimetumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Baadhi ya mandhari hizo ni kama zifuatazo:

4.5.4.1 Mandhari ya Pwani/Ufukweni

Ndungo na Mwai (1991) wanasema kwamba mandhari kama vile bahari, mito, na misitu ni mionganoni mwa mandhari ambazo hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi. Pwani ni eneo linaloanza ufukweni hadi baharini katika usawa wa bahari. Ufukwe ni mahali ambapo maji ya bahari hufika yanapojaa na huwa pakavu yanapotoka (BAKIZA, 2010). Fukwe ni sehemu nzuri yenyewe utulivu na kivutio. Kwa mfano katika visiwa vya Zanzibar mionganoni mwa mambo ambayo yanachangia pato la uchumi wa nchi ni pamoja na suala la utalii, ambapo wageni kutoka sehemu mbalimbali za dunia huja kutembelea sehemu nyingi zikiwemo fukwe za bahari kama vile, Kizimkazi, Nungwi, Jambiani, Paje, Bwejuu na nyenginezo. Mbali na wageni hata wenyeji pia hufika katika sehemu hizo pamoja na ndugu, jamaa, wapenzi na marafiki na kufurahia. Mfano wa hayo unadhihirika katika dondo hii ifuatayo:

“Walipochoka kuketi majabalini, Tambo na Mwavile walishuka ufukweni kupakana mchanga miilini mwao. Walicheza mchezo huo mpaka wakatosheka. Mwishowe walijitupa majini kuiogesha na kuisuuza mili yao kwa furaha kubwa zaidi. Huo ulikuwa mchezo wao katika mapenzi yao ya kitoto tu. Ambao haukuwa na hatia wala

dhambi yeote. Ilikuwa bado tutumko la maumbile yao halijawachangamkia. Bado hisia changa hazijawachochea. Akili hazijaanza kuzingatia maana ya uke na uume. Walikuwa wamejjaza tu ureda wa michezo ya kitoto...”(uk. 66).

Mwandishi kupitia dondo hii ameonesha mapenzi ya dhati baina ya Tambo na Mwavile wakiwa baharini. Wapenzi walipendana kwa dhati tokea wadogo walipokuwa wakiishi katika mapenzi ya udugu mpaka kufikia kuooana na kuwa mke na mume. Kwa kawaida wapenzi hupendelea sana kukutana katika sehemu zenyet ulivu kuzungumza masuala muhimu yanayohusu maisha ikiwemo suala la mapenzi. Mandhari ya ufukweni imetumika vilivyo kuwasilisha dhamira ya mapenzi wakati wapenzi hao wakicheza michezo mbalimbali pamoja na kurushiana michanga kimzaha wakiwa katika hali ya furaha na mapenzi. Mapenzi ya udugu ambayo bado yalikuwa hayajaamsha hisia na mihemko ya kimwili.

4.5.4.2 Mandhari ya Nyumbani

Nyumbani ni pahala pa kuishi au palipo na uasili wa mtu kama ule msemo usemao “*nyumbani ni nyumbani*” ni sehemu ya makazi ambayo inaonekana na kufahamika ambapo watu wenye uhusiano wa udugu, ujamaa au urafiki huishi pamoja. Nyumba ni sehemu muhimu katika maisha ya mwanadamu kwa sababu katika mambo ya msingi kwa mwanadamu baada ya chakula na mavazi ni sehemu ya kuishi. Mwandishi ametumia matumizi ya mandhari ya nyumbani kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Miongoni mwa mandhari hayo inaonekana katika mfano ufuatao :

“Mlezi wangu tokea mimi na yeye tulipokuwa wadogo aliungama komyakimya Tambo. Alinilea lakini nilicheza naye. Nikacheka naye. Nikagombana naye. Nikaona raha kuwa naye. Nilipokuwa mtoto, tena mtoto wa nyumba kubwa, nililelewa na yeye hapo nyumbani. Nililelewa naye na kufanyiwa kila kitu. Nililishwa kwa kijiko. Nikarambishiwa asali kwa vidole. Nikapangishwa na kufanyishwa shii na nyunu na yeye. Halafu nikaoshwa na yeye. Wakati wa kulala nilibembelezwa na kuchombezwa ili nitulie niweze kulala. Niliweza kuachana na mamangu Bi Chani na babangu Bwana Mansour, lakini si Mwavile hata dakika moja” (uk 82- 83).

Kwa mnasaba wa nadharia ya Simiotiki, nukuu hii inathibisha kuwa suala la malezi hufanyika nyumbani. Mwandishi hakutumia mandhari hii kwa bahati mbaya isipokuwa ni katika kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Katika mandhari hii yameonekana matukio mbalimbali ambayo kimsingi yanadhihirisha dhamira ya mapenzi, matukio hayo hayakufanyika sehemu nyengine yoyote ile isipokuwa ni ndani ya nyumba yao waliokuwa wakiishi mtoto na mlezi wake, kama vile kulishwa kwa kijiko, kurambishiwa asali kwa kidole, kuogeshwa, kubembeleza wakati wa kulala na mengine mengi yenye mshabaha wa hayo.

Kama wanavyoeleza Msokile (1992) na Senkoro (2011) kwamba fani na maudhui ni sura au pande mbili za sarafu moja na si rahisi wala sahihi kuvitenga na kuvielezea katika upweke wake bila kuhusisha na nyingine. Mtafiti anakubaliana na wataalamu hawa kwamba fani na maudhui hutegemeana na kusaidiana katika kufikisha ujumbe na hili limethibitika kupitia uchambuzi wa mbinu za kisanaa/kifani ambazo zimetumika kuwasilisha dhanira ya mapenzi. Mbinu hizi kwa ujumla zimetumika katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi kama ilivyoonekana katika utafiti huu.

4.6 Hitimisho

Sura hii ilihusika na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Utafiti ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo yamefanyiwa uchambuzi uliopelekea kukamilika kwa lengo kuu la utafiti huu ambalo ni *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*. Katika lengo mahsususi la kwanza mtafiti alibainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitekeza katika aina tofauti. Mtafiti alibaini kwamba, yapo mapenzi ya nchi, mapenzi ya familia, mapenzi ya ndoa, mapenzi ya udugu, mapenzi ya urafiki, mapenzi ya dini/imani, mapenzi ya mazingira, mapenzi ya elimu, mapenzi ya pesa /mali, na mapenzi ya kazi. Fauka ya hayo katika lengo mahsususi la pili mtafiti alichambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuibua dhamira ya mapenzi. Mbinu zilizojadiliwa na kuchambuliwa katika utafiti huu ni mbinu ya ujenzi wa wahusika, mbinu ya matumizi ya lugha na mbinu ya matumizi ya mandhari.

SURA YA TANO

HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inahusiana na Hitimisho la utafiti huu kwa kutoa majumuisho ya jumla juu ya mada iliyofanyiwa utafiti na yaliyojitokeza. Aidha sura hii imetoa Muhtasari na Mapendekezo yanayofaa kwa tafiti za baadae katika viwango vytaaluma ya uzamili na ngazi nyenginezo.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umehusu mada: Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ya Said Ahmed Mohamed. Vile vile utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambapo uliongozwa na malengo mahsusini mawili. Lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni Kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Lengo hili limekwenda sambamba na suali la kwanza la utafiti linalosema: Ni kwa namna gani dhamira ya mapenzi imejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? Uwasilishaji na uchambuzi wa lengo na swalii hili la kwanza la utafiti huu lilijibiwa baada ya mtafiti kuchunguza na kugundua kuwa kuna dhamira mbalimbali za mapenzi zilizojitokeza. Dhamira hizo ni pamoja na mapenzi ya nchi, mapenzi ya familia, mapenzi ya ndoa, mapenzi ya udugu, mapenzi ya urafiki, mapenzi ya dini, mapenzi ya mazingira, mapenzi ya kazi, mapenzi ya mali na mapenzi ya elimu. Kwa hakika dhamira ya mapenzi ina nafasi kubwa katika maisha ya jamii hasa kwa vile mapenzi ni sehemu ya maisha ya mwandanamu.

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa: Kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe Si mbali Tena*. Vile vile lengo hili nalo liliandamana na swali la pili la utafiti lisemalo: Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena?*. Mtafiti amebaini mbinu tofauti kama vile mbinu ya matumizi ya wahusika, mbinu ya matumizi ya lugha ambayo ndani yake kuna matumizi ya tamathali za semi mbalimbali pamoja na mbinu ya matumizi ya mandhari ambazo zimetumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi. Kwa hivyo, malengo haya mahsusi pamoja na masuali yake yamejibowi katika sura ya nne iliyohusu: Uwasilishaji na Uchambuzi wa data za utafiti husika. Utafiti huu una sura tano kuu zifuatazo:

Sura ya kwanza inahusu Utangulizi wa Jumla: Hivyo basi sura hii imejikita zaidi katika kuelezea mada husika ya utafiti huu, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vile vile sura imeelezea umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

Sura ya pili ni Mapitio ya kazi tangulizi na Mkabala wa Kinadharia: Katika sura hii vipengele vya msingi vilivyojadiliwa ni pamoja na: Ufanuzi wa Istilahi muhimu zinazohusiana na mada ya utafiti, Historia na Chimbuko la riwaya na Pengo la Maarifa. Licha ya hayo, sura imefafanua kwa kina Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu dhamira kwa ujumla katika riwaya na Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za mwandishi Said Ahmed Mohamed. Mwisho sura imeelezea Mkabala wa Kinadharia ambapo nadharia zilizofafanuliwa ni Mwitiko wa Msomaji/Upokezi pamoja na nadharia ya Simiotiki na mwisho ni Hitimisho.

Sura ya tatu imeeleza Mbinu za utafiti. Katika utafiti huu sura hii imetaja eneo lilitotumika, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji wa data pamoja na mbinu za uchambuzi wa data, mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti pamoja na zana / vifaa vya utafiti na Hitimisho.

Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi data za utafiti. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kwa kuongozwa na malengo mahsus i mawili ya utafiti yanayokwenda sambamba na maswali mawili ya utafiti. Vilevile katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji kwa lengo mahsus i la kwanza na swali la kwanza la utafiti. Nadharia ya Simiotiki imetumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa lengo mahsus i la pili na swali la pili la utafiti.

Sura ya tano nayo imehusu Hitimisho, Muhtasari na Mapendekezo. Sura hii imeanza na utangulizi wa utafiti kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya mwisho. Sambamba na hilo Sura hii pia imeelezea Muhtasari, matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ambayo yanafaa kwa watafiti wanaotarajiwa katika tafiti zijazo.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Katika uchambuzi wa data za utafiti huu mtafiti alibaini kuwa, katika riwaya ya *Kamwe Si Mbali Tena* dhamira ya mapenzi imeweza kubainishwa katika miktadha/aina mbalimbali. Matokeo hayo kwa muhtasari yameonesha kuwa mapenzi ni dhana pana sana tofauti na baadhi ya watu wanavyodhania kwa maana finyu ya kingono tu. Hivyo matokeo ya utafiti huu yamebainika kama ifuatavyo:

5.3.1 Lengo la Kwanza

Lengo mahsusili la kwanza la utafiti huu lilikuwa: *Kubainisha dhamira ya mapenzi namna ilivyojitokeza katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena*. Lengo hili likwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti lisemalo: Ni kwa namna gani dhamira ya mapenzi imejitokeza katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, baada ya uchunguzi wa kina lengo mahsusili hilo na swali hili la kwanza limefanikishwa vyema wakati mtafiti alipogundua kuwa katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*, dhamira ya mapenzi imebainishwa katika aina tofauti ikiwemo mapenzi ya nchi, mapenzi ya familia, mapenzi ya ndoa ambayo yapo ya dhati na yale ya uongo, mapenzi ya urafiki, mapenzi ya dini/imani, mapenzi ya mazingira, mapenzi ya elimu, mapenzi ya mali/pesa na mapenzi ya kazi.

5.3.2 Lengo la Pili

Lengo mahsusili la pili la utafiti huu lilihusi: Kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*. Lengo hili nalo liliongozwa na swali lisemalo: Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena*? Lengo mahsusili hilo na swali lake la pili la utafiti huu lilichambuliwa na kuwasilishwa vyema. Mtafiti alibaini kuwepo kwa mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika riwaya teule. Mbinu hizo za kisanaa zilizochambuliwa ni pamoja na matumizi ya wahusika, matumizi ya lugha, na matumizi ya mandhari.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu *Kuchunguza dhamira ya Mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Saidi Ahmed Mohamed*. Kwa hivyo baada ya kukamilika kwa tasnifu hii ambayo inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa kwa watafiti wajao., wasomi pamoja na wahakiki wa kazi za fasihi ya Kiswahili maoni na mapendekezo yafuatayo yametolewa na mtafiti kama ifuatavyo:

Kwanza, pamoja na kufahamu dhamira ya mapenzi kwa mawanda mapana kupitia riwaya ya *Kamwe si Mbali Tena* ni vyema kwa watafiti wajao kufanya tafiti za kazi za wandishi wengine kama vile Shaaban Robert, Shafi Adam Shafi na Mohamed Suleiman ili kubaini namna dhamira hii ya mapenzi ilivyojitekeza. Aidha ni jukumu la wanajamii kuyaenzi, na kuyadumisha mapenzi kwa gharama yoyote ili kujenga jamii iliyo bora na kuepusha mifarakano kwa jamii hususani kwa wanandoa, familia na marafiki kwa sababu mapenzi kwa ujumla huleta mshikamano, furaha, utulivu, amani, upendo, na huruma

5.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa ufupi sana yale yote yaliyojitekeza katika mada ya utafiti huu ambayo imehusu: *Kuchunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya ya Kamwe si Mbali Tena ya Said Ahmed Mohamed*. Dhamira ya mapenzi ni moja ya dhamira adhimu inayojitekeza sana katika kazi za fasihi. Hata hivyo si aghalabu kusoma kazi ya fasihi pasi na kukumbana na dhamira hii itategemea tu na jinsi mwandishi alivyoisawiri. Matokeo ya utafiti huu yalibaini, mapenzi ni dhana pana kutokana na namna yalivyojitekeza katika riwaya teule pamoja na mbinu za kisanaa zilizotumika kuwasilisha dhamira hii.

MAREJELEO

Ackerman, D. (1999). *A Natural History of Love*. New York: Randon House.

Adam, O. A. (2014). Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya ya Kiswahili Mifano kutoka *Kuli na Vuta N'kuvute*. Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Aiello, F. (1999). Mabadiliko ni maumbile: The Thematic and Stylistics Dynamism in S.A. Mohamed's Novel. *Utengano AAP*, 60, 59-65.

Al-Farsy, A.S.(1993). *Qur-an Takatifu* The Islamic Foundation Nairobi:

Ali, A. R. (2015). Kuchunguza Dhana Zilizobebwa na Wahusika Zinavyolandana na Majina yao katika Riwaya ya *Kiu na Kiu ya Haki*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ali, J. A. E. (2017). Kuchunguza Dhamira katika riwaya ya *Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ann, S. S. (2013). Usasa na Mwanamke wa Kisasa Katika *Nyuso za Mwanamke* ya Said Ahmed Mohamed.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi Kenya.

BAKIZA (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi Oxford University Press.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge Berkely*. California: University of California Press.

Bible Society of Tanzania (1997). *Biblia yenye Itifaki – Agano la kale na Agano Jipyा*. Nairobi: Africa Regional Service Centre.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*. New York: Oxford University Press.

Buliba na wenzake (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Tanzania Serengeti Educational Publishers (T) ltd.

Chandler, D. (1992). *Semiotics, The Basics*. London: Routledge Press.

Cobley, P. (2001). *The Routledge Companion to Semiotics and Linguistics*. London.

Cohen na wenzake (2000). *Research Methods in Education* 5th, ed. London: Routledge Falmer.

Cresswell, J. W. (2009). *Research Design, Qualitative Quantitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

Enon, J.C. (1998). *Educational Research Statistics and Measurement*. Kampala Makerere University.

Fakih, S. J. (2017). *Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya Utengano na Kamwe si Mbali Tena*: Utafiti Linganishi. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Furlong, N. (2000). *Research Methods and Statistics An Integrated Approach*. New York: Harcourt Colledge Publishers.

Haji, G. A. (2015). Upande wa Pili wa Riwaya Teule za Shafi Adam Shafi; Dhamira Zilizofichama.Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hassan, A. M.(20016). Kuchunguza Falsafa ya Mapenzi katika Diwani ya Mapenzi Bora. Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Hornby, A. S, (2005) *Oxford Advanced Learners Dictionary*. Oxford Universtiy Press. (<https://www.psychologytoday.com/blog/hide-and-seek/201606/the-7-types>).

(<https://thoughtcatalog.com/rania-naim/2016/02/the-7-kinds-of-love-and-how-they-can-help-you-define-yours-according-to-the-ancient-greeks/>).

(<http://www.yourdictionary.com/love>).

IPC. (2003). *Lengo la Maisha ya Mwanadamu* Juzuuy ya 1. Islamic Propagation Centre: Dar es Salaam.

IPC. (2004) . *Familia ya Kiislamu* Juzuuy ya 4. Islamic Propagation Centre: Dar es Salaam.

IPC (2004) *Historia ya kuhuisha Uislamu* Juzuuy ya 6. Islamic Propagation Centre: Dar es Salaam.

Jesse, M, J. (2017) Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Jilala, H. (2014). Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka katika Matini za Kitalii katika Makumbusho ya Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1976). Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Khamis ,S. (2007) .Versalitiy of The Taarab Lyris Locaral Aspects andaGlobal Influemce in Kiswahili Vo.70. Dar es Salaam: The Institute of Kiswahili Reseach.

King'ei, J. na Amata, J. K. (2001).*Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Kinoti, M. (2012) Nadharia ya Upokezi /Mwitiko wa Msomaji. Imepakuliwa 10/2/2019,10:00am kutoka kiswahilimamboleo.blogspot.com

Kombo, D. K. na Tromp, D.L (2006). Proposal and Thesis Writing, An Introduction. Nairobi: Paulines Puplicatoin Africa.

Kothari, R.C. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kotahri, R. C. (2008). *Research Methedology and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misini ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

- Msebo, J. A. (2009). *Mwongozo wa Kujibu Maswali ya Vitabu Teule vya Fasihi Kidato cha 5 na 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.
- Mbarouk, M. A. (2016). *Kuchunguza Matumizi ya Tamathali za Semi katika Riwaya ya Haini*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Mlacha, S.A.K. na Madumulla , J. S.(1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam University Press.
- Mohamed, S. A. (2014). *Kamwe si Mbali Tena*. Nairobi: Oxford University Press.
- Msacky, E.Y. (2015). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kisiasa katka riwaya ya Siri za Maisha*.Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: DUP.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP Ltd.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Saalam: TUKI.
- Mushegenzi, A.(2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Makerere University.
- Mwanjoka, G. (2011). *Harakati za Bongo Fleva Mapinduzi*, Dodoma: H.M.
- Ndungo, C. (1991). *Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: University of Nairobi.
- Ndungo, C.na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies Part Two, Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi.

Ndungo, C. na Wafula, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi.

Ngole, S na Honero, L. (2002). *Fasihi Simulizi ya Mtanzania* Kitabu cha Pili. Dar es Salaam.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Fasihi. Augustana College, Rock Island, IL 61201.

Nyangwine, N. (2002). *Usanifu wa Maandishi. Kidato cha 5 na 6*. Afroplus Industries LTD, Dar es Salaam.

Omar, S. (2012). *Mulika NO.31. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam.

Rajab, F. H. (2016) *Chango za Kimapenzi katika Nyimbo za Taarab Asilia za Seif Salim*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Robert, S. (2007). *Mapenzi Bora*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd. Dares-salaam.

Robson, C. (2007). *How To Do A Research Project: A Guide for Undergraduate Students*. Blackwell Publishing Cariton Victoria.

Said, A. S. (2015). Matumizi ya Ndoto katika Riwaya ya Kiswahili Ulinganisho wa Riwaya ya Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Salim, M. A. (2015). Kuchunguza Ufasihi Simulizi Unaojitokeza ndani ya Hadithi za *Kusadikika na Adili na Nduguze*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Selhub, E. (2009). The Love Response. New York: Randon House.

Senkoro, F. E. M.K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro. F.E. M. K. (2011). *Fasihi andishi* Dar es Salaam: KAUTTU L.t.d.

Sternberg, R. J. (1986) A Triangular Theory of Love. Psychological Reviews 93:119-135.doi 10.107/0033-295X,93.2.119.

TUKI (2010). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford.

Wamitila, K.W.(2002). *Uhakiki wa Fasihi, Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Litho Limited.

Wamitilla, K. W. (2003). *Kamusi ya Kiswahili, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication.

Wamitila, K. W.(2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Puplication Limited.

Wamitilla, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi. Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vidde-Muwa Publishers L.t.d.

Wanyonyi, M. (2015). Ishara na Uashiriaji kama Nyenzo ya Mtindo, Maana na Kiwakilishi cha Itikadi katika Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. SF, 22, 104-118.

Williman, N.(2005). *Your Research Project 2nd Edition*. London: SAGE Publication Ltd.

Williman, N. (2011). *Your Research Project A Step By Step Guide For the first Time*. London: Sage Publication

Zick, R. (1970). Measurement of Romantic Love Journal of Personality and Social Psychology 16:265-27.doi 10, 103/h00 29841.